# Nipashe

Jumamosi Septemba 28, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580035

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Bashe aibua ripoti ya wizi mabilioni vyama ushirika

UKURASA 3




UKURASA 13


## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**MAJERUHI AJALI JWTZ WAPELEKWA MUHIMBILI**
ASKARI 11 wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kikosi cha 24 KJ ambao walijeruhiwa baada ya gari walilokuwa wakisafiria kuacha njia na kupinduka eneo la...

UKURASA WA 3

**AZAKI ZAIBUKA NA ILANI UCHAGUZI MKUU, MITAA**
ASASI zisizo za kiserikali (Azaki), zimeibuka na ilani yenye vipaumbele 10 vya wananchi kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 na wa serikali za mitaa....

UKURASA WA 4

**WAZIRI MPANGO ATWISHA M ZIGO UONGOZI WA IFM**
WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mipango, amelitaka Baraza la Uongozi la Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) kusimamia utoaji mafunzo ya ubunifu...


# Tenga, wenzake wataka ‘yaishe’

**WAOMBA** kukaa mezani ili wakiri makosa, aliyemwomba DPP ahukumiwa kulipa mil. 10/- ... *Endelea ukurasa wa 2*



DPP Biswalo Mganga

Dk. Ringo Tenga

## Magari chakavu ‘stop’ kubeba kitoweo

UKURASA 3

## Fedha uchaguzi mitaa zageuka kaa la moto

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA: TUPO TAYARI KUPINDUA MEZA LEO UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

# Majeruhi JWTZ wapelekwa MNH

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

ASKARI 11 wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kikosi cha 24 KJ ambao walijeruhiwa baada ya gari walilokuwa wakisafiria kuacha njia na kupinduka eneo la Hifadhi ya Katavi mkoani Katavi, wamehamishiwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kwa matibabu zaidi.

Kaimu Mganga Mkuu Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa Maweni, Dk. Lameck Mdengo, alisema majeruhi ambao wamepelekwa Muhimbili ni Peter Kibasa, Brght Chuma, Said Iddi, Selemani Mohamed, Hamisi Bakari, Ezekieli Kiginya, Jackson Mlelwa, Ntahidi Bakari, George Aloice, Rubeni Mpanda na Gefrey Kalinga.

Alisema majeruhi hao walisafirishwa jana majira ya saa 12 asubuhi kwenda Muhimbili kwa ndege ya JWTZ.

Dk. Mdengo alisema waliotibiwa na kuruhusiwa kurudi nyumbani ni Shabani Lyimo, Oscar Lyimo, Ramadhani Ally na Abduel Shabani. Aidha, alisema maiti mbili zilizotokea kwenye ajali, zimechukuliwa na kusafirishwa kwenda jijini Dar es Salaam.

Baada ya majeruhi hao kupewa rufani na wengine kuruhusiwa, Dk. Mdengo alisema kwa sasa hospitalini hapo hakuna majeruhi wanaoendelea na matibabu.

Ajali hiyo ilitokea juzi mkoani Katavi wakati askari hao wakienda kwenye shughuli zao za kikazi kutokana na gari waliokuwamo kufeli breki na kuacha njia hatimaye kupinduka.

# Dk. Tenga, wenzake wataka yaishe

**Na Hellen Mwango**

VIGOGO wa Kampuni ya Mawasiliano ya Six Telecoms Limited, akiwemo Wakili wa Kujitegemea Dk. Ringo Tenga na wenzake wanne wanaokabiliwa na tuhuma za kutakatisha fedha, wamemwandikia barua Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP) wakitaka wakae mezani kuzungumzia kesi hiyo.

Wakati vigogo hao wakiomba 'yaishe', mtuhumiwa wa kwanza aliyeandika barua kwa DPP, raia wa Sri Lanka, AbdulAzeez Amaan (26), amehukumiwa kulipa faini ya Sh. milioni 10 au kwenda jela miaka mitatu baada ya kukiri kosa la kusafirisha madini yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 36 kinyume cha sheria.

Dk. Tenga na wenzake wakabaliwa na mashtaka ya kutoza malipo ya kimataifa kwa tozo ndogo kwa lengo la kujipatia faida, kutakatisha fedha na kuisababishia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) hasara ya Dola za Marekani 3,748,751.22 (sawa na Sh. bilioni nane).

Jana kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba.

Wakili wa Serikali Jacqueline nyantori, alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa jana kwa ajili ya kutajwa na kwamba mara ya mwisho upande we utetezi uliwasilisha ombi la ahirisho fupi kwa kuwa wana hoja wakazungumze na wateja wao.

Wakili wa Utetezi, Bryson Shayo, alidai kuwa baada ya kushauriana na wateja wao, tayari washtakiwa wamemwandikia DPP barua kutokana na ushauri wa Rais John Magufuli, alioutoa Jumapili Septemba 22, mwaka huu.

Upande huo wa utetezi ulidai kuwa Septemba 26, mwaka huu, waliandika barua yenye maombi mbalimbali kuhusiana na kesi hiyo kwenda kwa DPP ikiwapo ahirisho la siku 14 ili wapate majibu ya barua hiyo.

Hakimu Simba alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Oktoba 11, mwaka huu.

Mbali na Dk. Tenga washtakiwa wengine ni Hafidhi Shamte au Rashidi Shamte ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa kampuni hiyo, Mfanyabiashara na Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Peter Noni, Mkuu wa Fedha Noel Chacha na Kampuni ya Six Telecoms.

Dk. Tenga na wenzake wanadaiwa kuwa kati ya Januari 1, 2014 na Januari 14, 2016 jijini Dar es Salaam, walitoza malipo ya mawasiliano ya simu za kimataifa chini ya kiwango cha Dola za Marekani 0.25 kwa dakika kwa lengo la kujipatia faida.

Pia katika kipindi hicho, wanadaiwa kuhujumu miundombinu ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa kutoza gharama chini ya kiwango na kushindwa kulipa kiasi cha Dola za Marekani 3,282,741.12 kwa TCRA, kama malipo ya mapato.

Pia wanadaiwa katika kipindi hicho walishindwa kulipa ada za udhibiti za Dola za Marekani 466,010.07 kwa TCRA.

Vilevile, washtakiwa hao wanadaiwa kuwa waliisababishia TCRA hasara ya Dola za Marekani 3,748,751.22 (sawa na Sh bilioni nane).

BARUA YAJIBU

Mtuhumiwa wa kwanza kuandika barua kwa Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP), Raia wa Sri Lanka, AbdulAzeez Amaan (26) baada ya Rais kutoa ushauri, amehukumiwa kulipa faini ya Sh. Milioni 10 au kwenda jela miaka mitatu baada ya kukiri kosa la kusafirisha madini yenye thamani

INAENDELEA UK. 8



Ndugu, jamaa na marafiki wakiwa wamelibeba jeneza lenye mwili wa Gabriel Gaudens Mgunda aliyekuwa msambazaji wa magazeti The Guardian na Nipashe, yanayochapishwa na kampuni ya The Guardian Ltd, baada ya kuuaga katika Kanisa la Katoliki Kimara Mwisho, jijini Dar es Salaam jana na baadaye kusafirishwa kwenda Morogoro kwa mazishi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Fedha uchaguzi serikali za mitaa kaa la moto

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UCHAGUZI wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu. Utatumia zaidi ya Sh. bilioni 82 huku serikali ikionya kuwa ni moto kuliko maelezo na watakaothubutu kuzifuja 'watazitema'.

Sambamba na hilo, mkurugenzi yeyote atakayebainika kukwamisha au kuhujumu uchaguzi huo hataonewa huruma kwa kuwa atawajibishwa.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo, alisema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifungua kikao kazi cha Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi wa Halmashauri na wasimamizi wa uchaguzi huo.

Aliwatahadharisha kuwa fedha hizo zimepelekwa kwa ajili ya uchaguzi na si vinginevyo.

"Fedha hizi ni kwa ajili ya uchaguzi, naomba mtu asidanganyike wala kurubunika kwa lolote katika mchakato huu wa uchaguzi. Fedha hizi ni za moto kuliko maelezo naomba niwaambie," alisema.

"Fedha hizi ziende zikatumike kwa ajili ya ajenda hiyo hiyo ya uchaguzi lakini iende ikatumike kwa wakati unaotakiwa. Hatutarajii ucheleweshaji wa aina yoyote wala matumizi yasiyokusudiwa."

Alisema anaamini watatumia vyema fedha hizo kama ambavyo anatarajia na Rais John magufuli anaokusudia hivyo na hatarajii jambo lolote kukwama katika uchaguzi huo.

Jafo alisema fedha hizo tayari zimeshapelekwa kwenye halmashauri kulingana na ukubwa wa maeneo na idadi ya vituo husika na kuwaonya wakurugenzi watakaobainika kufelisha au kuhujumu uchaguzi watawajibika.

"Sasa wewe mkurugenzi wa halmashauri ukafanye jambo lingine lolote kuhujumu mchakato mzima wa uchaguzi. Naomba niwaambie huu uchaguzi ni uchaguzi mgumu sana lengo letu demokrasia itamalaki. Sisi tuliopewa dhamana ni jukumu letu kubwa kuhakikisha hiyo demokrasia kwenda kufanya kazi yake kila mmoja wetu aende akatimize wajibu wake," alisema.

Waziri Jafo alisema Rais anatamani waende kutekeleza demokrasia vizuri kwenye uchaguzi huo ndiyo maana ametoa uwezeshaji kwa kila eneo.

"Lakini ninyi wasimamizi wa uchaguzi mna jukumu na mzigo mkubwa sana huko kwenu. Jambo la kwenda ni kuhakikisha uchaguzi unakuwa mzuri zaidi. Nina imani na kila msimamizi wa uchaguzi na kanuni imetueleza inasema Waziri kwa wakati wowote anaweza akatoa miongozo kanuni iko wazi muda wowote. Katibu anaweza akatoa mwongozo mimi natamani sana mlioteuliwa mwende vizuri mpaka mmalize vizuri kwa mujibu wa kanuni zetu,"alisema.

Aliwasisitiza wasimamizi wa uchaguzi kujua kanuni za uchaguzi huo na muda wa wenyeviti wa mitaa,vijiji na vitongoji na wajumbe wengine wanapaswa kukoma kwenye uongozi.

**UKOMO WENYEVITI**

"Kanuni inakueleza lini siku ya wale wenyeviti wanatakiwa ukome utawala wao. Haiwezekani mwenyekiti wa kijiji bado mwenyekiti wa kijiji mpaka siku

INAENDELEA UK. 8

# HABARI KITAIFA



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wakipita jirani na ujenzi unaoendelea wa Barabara za mpishano (Ubungo Interchange), katika eneo la Mataa ya Ubungo, jijini humo, jana. **PICHA: JOHN BADI**

## Bashe aibua wizi bil. 123/- ushirika

**Na Happy Severine,**
MWANZA

NAIBU Waziri wa kilimo, Hussein Bashe, amesema ripoti ya ukaguzi ya Shirika la Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika (Coasco), imebaini upotevu wa Sh. bilioni 123 kwenye vyama vya ushirika.

Bashe aliyasema hayo jana wakati akifungua kikao cha wadau wa Bodi ya Pamba Tanzania kinachofanyikia kwenye ukumbi wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) jijini Mwanza. Kutokana na kubainika kwa wizi huo, Bashe alisema wahusika wote wa wizi huo watachukuliwa hatua kali. "Hapa nina kabrasha, nitawapatia wakuu wa mikoa wote na nitamkabidhi kiongozi wa tume. Kwa ripoti ya Coasco, ushirika kumetokea upotevu wa Sh. bilioni 123 na nisema hapa hatua kali zitachukuliwa kwa wahusika wote," alisema. "Hizi ni pesa za wakulima, wote waliohusika katika huu upotevu watachukuliwa hatua kali. Wakuu wa mikoa tutawapa majina ya Amcos (vyama vya ushirika vya msingi) gani wanahusika na mnatakiwa kuchukua hatua," aliongeza.

Naibu Waziri Bashe pia alisema ushirika uliopo kwa sasa unahitaji mabadiliko makubwa kwa kuwa hauwezi kutatua matatizo ya kilimo hasa kwenye pamba. Kwa mujibu wa Bashe, mfumo wa ushirika wa sasa unatakiwa kubadilishwa kutoka kuhudumia wakulima na kuwa ushirika wa kibiashara.

Nao wajumbe wa mkutano huo kutoa mikoa mbalimbali, walielezea kusikitishwa na ripoti hiyo na kuelezea hofu yao kubwa ya kutoviamini vyama vya ushirika.

Baadhi ya wajumbe hao, walisema ni aibu kubwa kuendelea kuona vyama vya msingi vinazidi kupoteza imani kwa wakulima na wadau, hivyo serikali inapaswa kuliangalia hilo kwa macho mawili.

## Magari chakavu yapigwa 'stop' kubeba nyama

**Na Gidion Msabula,**
TUDARCO

BODI ya Nyama Tanzania, imepiga marufuku magari yenye kutu kutumika kubeba nyama kwa kuwa ni kosa kisheria.

Marufuku hiyo ilitolewa juzi na Kaimu Msajili wa Bodi hiyo, Imani Sichalwe, wakati akizungumza katika maonyesho ya teknolojia za uchakataji wa nyama jijini Arusha.

Alisema ili kuhakikisha nyama inakuwa katika ubora wake pamoja na kulinda afya za watumiaji ni lazima ibebwe kwenye vyombo salama na si ndani ya magari yenye kutu ambayo yanaweza kusababisha madhara makubwa kwa walaji.

Sichalwe alisema katazo hilo si kwa madereva wa magari hayo pekee bali hata kwa wamiliki wa mizigo na wanaobeba kwenye vyombo vingine na kwenye mifuko ya sandarusi kubeba mgongoni. Mkurugenzi wa Jiji la Arusha, Ismail Kulanga, aliahidi kushirikiana na machinjio ya nyama kuhakikisha yanakuwa katika hali ya usafi muda wote na mazingira ya kuridhisha. Naye Mwenyekiti wa Chama cha Wachinjaji Nyama Mkoa wa Arusha, Alex Lasika, aliiomba serikali muda zaidi kwenye katazo la matumizi ya vigogo wakati wa kukata nyama kwa kuwa inatumiwa na wengi na hawajaweza kununua mashine.

## Azaki zaibuka na ilani za uchaguzi

**Na Salome Kitomari**

ASASI zisizo za kiserikali (Azaki), zimeibuka na ilani yenye vipaumbele 10 vya wananchi kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 na wa serikali za mitaa utakaofanyika Novemba, mwaka huu.

Wakizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, wawakilishi wa azaki hizo, walisema ilani hiyo ni mwendelezo wa ilani ya uchaguzi ya asasi hizo kwa ajili ya serikali za mitaa na uchaguzi mkuu iliyotolewa mwaka 2015.

Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Onesmo Ole Ngurumwa, alisema vipaumbele hivyo vinatokana na mafanikio na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Ilani ya mwaka 2015.

"Kwa kuwa viongozi wa azaki za Tanzania wameamua kwa dhati kujenga jamii inayozingatia misingi ya uhuru, haki, udugu na amani, wameamua kuandika Ilani hiyo kwa niaba ya azaki na wananchi kwa ujumla, kwa madhumuni ya kuhakikisha uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu unafanyika kwa kuzingatia sheria na matakwa ya wananchi," alisema.

Alisema lengo ni kuhakikisha Tanzania inaongozwa na serikali inyofuata misingi ya demokrasia, utawala wa sheria na utawala bora.

"Kama ilivyokuwa katika Ilani ya awali, nia hasa ya Ilani hii ya sasa ya Azaki ni kutoa mwongozo kuhusu namna ambavyo vyama vya siasa, wagombea wa uchaguzi, Tume za Taifa za Uchaguzi (Zanzibar na Tanzania Bara), vyombo vya usalama, serikali, Azaki na wananchi wote kwa ujumla wanatakiwa kushiriki chaguzi," alisema.

Alisema lengo ni kuhakikisha uchaguzi unafanyika katika hali ya amani na utulivu, uhuru na kufikia malengo yao ya kuwachagua viongozi wanaowataka.

"Ilani hii ya pili ya Azaki imechagizwa na maazimio ya wawakilishi wa Azaki kutoka nchi nzima katika mkutano uliofanyika Julai 4, 2019," alibainisha Ole Ngurumwa.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la New of Hope Tanzania, Clemence Mwombeki, alisema ilani ya mwaka 2015 ilibainisha vipaumbele vinne vya katiba mpya, sera ya uchumi wa kitaifa, usimamizi wa rasilimali za umma na haki za binadamu na utawala Bora.

"Tathmini ya azaki imeona kuna mafanikio katika uboreshaji wa elimu kwa kuakisi hali ya watu wa kipato kidogo, huduma za afya ikiwa ni pamoja na kujenga au kupanua vituo vya afya sehemu mbalimbali hapa nchini," alisema.

Kwa mujibu wa Mwombeki, kuna ulinzi na usimamizi mzuri wa rasilimali za umma iliyosaidia kuleta ongezeko la ukusanyaji wa mapato ya ndani kutoka vyanzo mbalimbali.

Lingine ni uanzishaji na uendelezaji wa miradi mikubwa ya kiuchumi kwa ufanisi wa hali ya kuridhisha (tofauti na miaka mingine).

"Miradi hii ya kimkakati na kiuchumi ni pamoja na ujenzi wa reli ya kisasa, upanuzi wa uwanja mkubwa wa ndege wa Dar es Salaam na ununuzi wa ndege na kuanzisha safari nje ya nchi, ujenzi wa barabara na miundombinu mingine kama Reli ya Standard Gauge (SGR), alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Taarifa kwa Umma, Deus Kibamba, alitoa wito kwa wananchi kusoma ilani hiyo na vyama vya siasa na wadau wengine kuifanyia kazi kuanzia kwenye uchaguzi wa Novemba.

Aidha, Azaki ziliwaomba viongozi wa serikali na taasisi mbalimbali ikiwamo Nec na Zec kutilia maanani mapendekezo yaliyopo kwenye Ilani, ili kuwa na viongozi wanaotekeleza kwa kuzingatia maslahi ya nchi.

Pia, wamewataka viongozi wa dini kuendelea kuhubiri amani kwa waumini wao na kujiepusha na kutamka kauli zenye mwelekeo wa kupendelea mgombea au chama kwenye nyumba za ibada.

# Bodi yajipanga Kuzalisha tani milioni korosho

**Na Beatrice Moses**

BODI ya Korosho Tanzania imejiwekea lengo la kuongeza uzalishaji kutoka tani 313,000 kwa mwaka 2017/18 hadi tani milioni moja ifikapo mwaka 2023/24.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi hiyo, Francis Alfred, akizungumza na gazeti hili jana, alisema malengo hayo yamewekwa baada ya kubaini kuwapo ongezeko la mahitaji ya korosho kwenye soko la ndani na nje ya nchi.

Alisema malengo hayo yakifanikiwa, yataongeza tija miongoni mwa wakulima kutoka kilo 10 za korosho ghafi hadi kufikia kilo 35 kwa mti kwa mwaka.

"Pia tumeongeza idadi ya mikoa inayolima korosho kutoka mikoa mitano iliyokuwapo mwanzo hadi 17 katika maeneo mbalimbali nchini," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema kuongezeka kwa ubanguaji wa korosho nchini kupitia viwanda vya ndani, kumeibua changamoto kwa wanunuzi wakubwa wa korosho ghafi wa viwanda vya nje ya nchi.

"Kutokana na changamoto hiyo, tumeandaa mpango wa kuwezesha viwanda vya ndani kupata malighafi kwa mwaka mzima ili kufanya kazi kwa ufanisi zaidi," alisema.

Kwa mujibu wa Alfred, hatua hiyo inalenga kuongeza ubanguaji wa korosho zinazozalishwa nchini kutoka asilimia 24 kufikia asilimia 60 ifikapo mwaka 2023/24.

Kuhusu mkutano wa Septemba 30, mwaka huu, ambao ni wa kila mwaka, alisema upo kisheria kwa wadau wa korosho na utatumika pia kujadili uboreshaji wa sekta hiyo ndogo ili kufikia malengo.

"Mkutano unawahusisha wadau wote wa korosho hapa nchini wajumbe 400 wanatarajiwa watahudhuria," alisema.

Alisema mkutano huo unafuatiwa na mwingine mkubwa utakaofanyika Novemba 7-9 katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam

"Tutakuwa na Mkutano mwingine mkubwa wa kimataifa (African Cashew Alliance- ACA) utakaohusisha wadau wa korosho kutoka maeneo mbalimbali Afrika na duniani," alisema.

Mkurugenzi huyo aliongeza kuwa mkutano huo utakuwa na manufaa makubwa katika kukuza tasnia ya korosho nchini na kuitangaza nchi kwa ujumla.




Mkurugenzi wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF), Anna Kulaya (kulia), akizungumza katika mdahalo wa kuelekea mabadiliko katika sheria ya kimila ya mirathi na mkutano mkuu wa shirika hilo, ulifanyika jijini Dar es Salaam jana. Kutoka (kulia) ni Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika hilo, Naomi Kaihula, Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Augustine Mahiga na Mwanzilishi wa WiLDAF, Dk. Judith Odunga. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mpango autwisha zigo uongozi IFM

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mipango, amelitaka Baraza la Uongozi la Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) kusimamia utoaji mafunzo ya ubunifu wa mabadiliko ya teknolojia katika kuongoza sekta ya fedha kidigitali ili kukabiliana na wimbi la mafisadi na wezi.

Pia ameutaka uongozi huo kufanya tathmini kama elimu inayotolewa na chuo hicho inakidhi malengo ya kukuza uchumi wa viwanda ifikapo mwaka 2020 na kufikia kipato cha kati mwaka 2025.

Dk. Mpango aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizindua Baraza la Uongozi wa IFM na kusema ni muhimu elimu inayotolewa ikakidhi matakwa ya mabadiliko ya teknolojia.

"Huduma za kifedha mitandaoni zimeanza kunyumbuliwa kidigitali na hata kuna sarafu za mitandaoni ambazo zimeanza kutumiwa. Wezi na mafisadi nao wamejielekeza kwenye mfumo wa digitali, hivyo ni muhimu kutoa elimu inayoendana na mabadiliko ya teknolojia," alisema Dk. Mpango.

"Kwa maoni yangu, hakuna chaguo bali ni muhimu mafunzo yanayotolewa na chuo yawe ya ubunifu kwa vijana wa Kitanzania ili kuelewa mabadiliko hayo ya kuongoza sekta ya fedha kidigitali. Mwangalie upya uhasibu wa vitabu na miamala ya fedha, benki na bima, masoko ya mitaji, dhamana na amana," alisema.

Pia alisema analiachia kazi baraza hilo kutathmini kwa ukweli na uwazi ili kufahamu kama chuo kinatimiza lengo lake la kuanzishwa mwaka 1972.

"Serikali inaamini lengo la kuanzishwa kwake na inaamini yanasimamiwa vizuri kwa maslahi ya taifa letu," Dk. Mpango alisema.

Dk. Mpango aliahidi kuwa serikali itaendelea kukisimamia chuo hicho ili kutoa elimu bora inayokidhi kujenga uchumi wa viwanda na kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaojiunga na chuo hicho.

Naye Mwenyekiti wa Baraza hilo, Dk. Benson Bana, alisema watahakikisha wanasimamia malengo ya kuanzishwa chuo hicho lakini pia kuhakikisha elimu inayotolewa inakidhi kukuza uchumi wa taifa.

Alisema chuo hicho kinatoa elimu ya usimamizi wa fedha na kuzalisha wataalam wanaokidhi vigezo vya kimataifa.

# Ofisa wa CRDB kortini tuhuma uhujumu uchumi

**Na Hellen Mwango**

OFISA wa benki ya CRDB Tawi la Ubungo, Andrew Babu (27), na wafanyabiashara watatu, wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam wakikabiliwa na tuhuma za uhujumu uchumi ikiwamo kula njama, kughushi kadi ya kutolea fedha (Tembo Card), wizi na kutakatisha zaidi ya Sh. milioni 100.

Mbali na Babu, washtakiwa wengine ni William Sige (52), Justina Boniphace (49) na Alli Tutupa (35) wote wakazi wa Dar es Salaam.

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Augustina Mmbando na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon.

Simon alidai kuwa kati ya Oktoba, 2018 na Aprili 19, mwaka huu, washtakiwa wote kwa pamoja walikula njama kutenda kosa la wizi.

Katika shtaka lingine ilidaiwa kuwa Oktoba 29, mwaka jana, katika benki ya CRDB tawi la Ubungo, Babu peke yake kwa nia ya kulaghai au kudanganya, alighushi saini ya Charles Kihamia katika fomu ya maombi ya 'Tembocard'.

Pia mshtakiwa Babu anadaiwa Novemba 6, mwaka jana, alighushi saini ya Kihamia katika kitabu cha usajili kwa madhumuni ya kuonyesha kuwa imewekwa na Kihamia huku akijua si kweli.

Mshtakiwa Babu anadaiwa Novemba 5, mwaka jana alighushi saini ya Kihamia katika usajili wa kadi ya visa ya Tembo, kwa madhumuni ya kuonyesha kuwa imewekwa na Kihamia huku akijua si kweli.

Aidha, Novemba 6, 2018 anadaiwa alighushi saini ya Kihamia katika kitabu cha usajili wa uelekezaji kwenye fomu ya maombi kwa madhumuni ya kuonyesha kuwa imewekwa na Kihamia wakati akijua kuwa si kweli.

Mshtakiwa Babu pia anadaiwa, Oktoba 29, 2018 katika benki ya CRDB, alitoa fomu ya kughushi ya maombi ya 'Tembocard' ofisa wa benki hiyo aitwaye Omary Mduyah kwa lengo la kuonyesha kuwa imetolewa na kutiwa saini na Kihamia huku akijua ni uongo.

Katika shtaka la mwisho, ilidaiwa kati ya Novemba 7, 2018 na Aprili 29, 2019 washtakiwa kupitia kadi ya dhahabu ya Visa, walijipatia sh. 106,267,907 kutoka kwa Charles Kihamia kupitia kadi yake hiyo huku wakijua kuwa fedha hizo ni mazao ya makosa tangulizi ya kughushi na wizi.

Washtakiwa hawakuruhusiwa kujibu kitu chochote mahakamani hapo kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi.

HABARI KITAIFA



Mkurugenzi wa Miradi wa kampuni ya Mazoka Resources Pty, Dk. Joas Kabete, akitoa mada kwenye kongamano la watafiti wa madini, linaloendelea katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Matumizi nishati mbadala changamoto

**Na Romana Mallya**

MWITIKIO wa matumizi ya nishati mbadala kwenye mashirika na taasisi za serikali na binafsi ni mkubwa huku changamoto ikibaki kwa mwananchi mmoja mmoja kuachana na matumizi ya mkaa wa kawaida.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Uongozi na Maendeleo ya Ujasiriamali (IMED), Dk. Donath Olomi, aliyasema hayo jana kwenye mafunzo ya wajasiriamali wenye kampuni ambazo zinazalisha nishati mbadala ya mkaa, majiko na mashine za kutengenezeza nishati hiyo.

Wajasiriamali hao wametokana na shindano la biashara lililoandaliwa mwaka jana na Ofisi ya Makamu wa Rais na kufadhiliwa na kampuni ya Shell Exploration and Production Tanzania huku IMED ikipewa kazi ya kutoa mafunzo.

Dk. Ulomi alisema shindano hilo lililenga kutafuta wazalishaji wa nishati mbadala ya mkaa kwa wingi ili jamii, mashirika na taasisi mbalimbali ziachane na matumizi ya mkaa.

"Upo mwitikio mkubwa wa mashirika, taasisi na kampuni mbalimbali kutumia nishati mbadala lakini wananchi mmoja mmoja bado changamoto. Wanahitaji elimu zaidi ambayo kampuni hizi zimekuwa zikiwafikia na wakati mwingine kuhamasisha kwa kugawa majiko bure," alisema.

Alisema mkoa wa Dar es Salaam kwa mujibu wa takwimu, matumizi ya mkaa wa kawaida ni wa asilimia 90 na umeongezeka kutokana na kasi ya ukuaji wa miji.

Mkurugenzi huyo alisema kutokana na changamoto hiyo, waliona kuna haja ya kutafuta mbadala na sasa nishati mbadala licha ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, inatoa ajira na kuunga mkono azma ya Rais John Magufuli nchi kuwa ya viwanda. "Kwa siku mbili kuanzia jana (juzi) tunaendeleza mafunzo kwa kampuni tatu zilizoibuka na ushindi mwaka jana. Mafunzo haya ni ya miaka mitatu na tunayatoa kila wakati wanafundishwa kwa sasa wanapewa mafunzo ya kiufundi ili kampuni zao zizalishe bidhaa bora zinazokidhi viwango vya kimataifa," alisema.

Alisema kwa sasa kupitia kampuni hizo, wanasambaza nishati mbadala kwenye vyuo kikiwamo Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) ambao wamefunga majiko maalum yanayotumia mkaa huo.

Kwa mujibu wa Dk. Olomi, lengo ya mafunzo hayo ni kupanua soko la nishari mbadala na kuongeza uzalishaji kwa asilimia 400.

Akitoa mada inayohusu viwango vinavyotakiwa kwenye bidhaa hiyo, Ofisa Mwandamizi wa Viwango, Idara Uandisi Mitambo kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Joseph Ismail, alisema mwaka jana shirika hilo liliweka viwango vitano vinavyotakiwa kwenye uzalishaji wa nishati mbadala kwa sababu kulikuwa na changamoto ya ubora.

# Marekani yafungua milango kwa Watanzania

**Kelvin Onnocent na Dotto Lameck**

UBALOZI wa Marekani umetoa ufadhili masomo kwa wanafunzi wanaotaka kwenda kusoma nje ya nchi kutoka katika shule mbalimbali nchini.

Uamuzi huo ulitangazwa jana na Mshauri wa Masuala ya Elimu kutoka Ubalozi wa Marekani, Jackson Oganga, wakati wa maonyesho ya vyuo vikuu vya Marekani yaliyofanyika jijini Dar es Salaam. Maonyesho hayo yana lengo la kudumisha uhusiano wa karibu kati ya Marekani na Tanzania. Alisema faida wanayopata wanafunzi hao baada ya kutembelea maonyesho hayo ni pamoja na kujua vigezo na taratibu za kusoma Marekani baada ya kumaliza kidato cha sita na kuwarahisishia kuomba na kusoma nchini humo.

"Maonyesho haya yanafanywa na wanafunzi wa Kitanzania ambao walisoma Marekani na wamarekani waliosoma vyuo vya Marekani ili kuwakilisha vyuo vyao. Zaidi ya wanafunzi 200 wameitikia wito na kuhudhuria maonyesho haya ili kupata ufafanuzi zaidi jinsi ya kwenda kusoma Marekani," alisema Oganga. Baadhi ya shule zilizoshiriki ni Gills High School, Agakhan, Feza Boys na Feza Girls.

Kuhusu vigezo vilivyotumika kualika shule hizo, alisema ni uwezo na uhakika wa kufanya vizuri katika masuala ya elimu.

"Sana sana tumelenga kuchukua wanafunzi kuanzia kidato cha nne, tano na cha sita sababu wao ndio tunaamini wamekaribiana na mazingira ya kwenda vyuo vikuu," alisema Oganga. Mshauri huyo aliwasihi wazazi na jamii kwa ujumla kuhudhuria maonyesho hayo kwa ajili ya watoto wao ili kuongeza uelewa.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, Mwanafunzi wa kidato cha tano katika Shule ya Sekondari ya Shabani Robert, George Charles, alisema yamewasaidia kutafuta uwezekano wa kusoma vyuo mbalimbali vya nchi za nje katika sekta mbalimbali za kielimu na michezo.

# Masoko yakwamisha mapato halmashauri

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

KUKOSEKANA kwa masoko ya uhakika ya tumbaku katika mwaka wa fedha wa 2018/19 kumechangia kushuka kwa mapato ya ndani katika Halmashauri ya Ushetu, Kahama mkoani Shinyanga.

Zao hilo kwa miaka ya nyuma ndio lilikuwa likiipatia Sh. bilioni 1.2 za mapato ya ndani halmashauri hiyo tofauti na ilivyo kwa sasa lilivyoingiza Sh. milioni 700.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ushetu, Matomora Michael, aliyasema hayo juzi katika kikao maalumu cha baraza la madiwani la halmashauri hiyo kilichofanyika kwa lengo la kujadili taarifa za mwisho wa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, mwaka huu.

Matomora alisema kwa mwaka huu halmashauri yake ilikusanya asilimia 56 ya mapato ya ndani tofauti na miaka iliyopita ilipokuwa ikikusanya mapato mengi zaidi. Alisema kuwa hali hiyo imetokana na baadhi ya wanunuzi kuacha kununua tumbaku ya ziada kilo milioni 2.5.

Alisema kuwa changamoto hiyo ya kutonunuliwa zao hilo itaendelea kuwatafuna katika mapato ya ndani kwa kuwa ndio msingi mkubwa mpaka sasa wa halmashauri hiyo tangu kipindi cha nyuma.

Mkurugenzi huyo alisema viko vyama mpaka sasa ambavyo bado tumbaku yao haijanunuliwa huku msimu wa kusia mbegu za tumbaku ukiwa umeshaanza, hivyo kuwawia vigumu wakulima kupanda mbegu mpya ilihali tumbaku nyingine iko ndani.

Matomora alisema kutokana na hali hiyo, halmashauri imeshajizatiti katika kuhamasisha wananchi kulima korosho, zao ambalo tayari limeishaanza kulimwa kwa mwaka wa pili sasa.

Diwani wa Bukomela, Kurwa Shoto, alisema kutonunuliwa tumbaku yao wengi wao waliuza na hawajalipwa na kampuni huku wengine wakiwa bado na tumbaku ndani na kwamba hali hiyo inawavunja nguvu wananchi na wakulima kuendelea kulima zao hilo.

Shoto alisema kutokana na baadhi ya kampuni kuacha kununua tumbaku msimu ujao, kuna baadhi ya vyama vya msingi ambavyo vimekosa uzalishaji kwa msimu wa mwaka 2019/20.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Yanga, Azam, Malindi hakuna lisilowezekana

**TIMU** tatu kutoka nchini, leo zinatarajia kupeperusha bendera ya Tanzania katika mechi za marudiano za mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika.

Wawakilishi hao si wengine, bali ni Yanga ya jijini Dar es Salaam ambayo inashiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, na leo itashuka ugenini Ndola, Zambia kuvaana na wenyeji wao, Zesco FC. Katika mchezo wa kwanza wa mashindano hayo yanayosimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), uliochezwa Septemba 14, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa, mabingwa hao wa zamani wa Ligi Kuu Tanzania Bara walilazimishwa sare ya bao 1-1. Kwa upande wa Azam FC ya jijini itateremka mjini Bulawayo, Zimbabwe kuvaana na Triangle United katika mchezo wa Kombe la Shirikisho Afrika ikiwa na kumbukumbu ya kufungwa bao 1-0 katika mechi ya kwanza iliyochezwa majuma mawili yaliyopita kwenye Uwanja wa Azam Complex.

Bendera nyingine ya Tanzania, inatarajiwa kupeperushwa nchini Misri kwa Malindi FC watakapokuwa wanashuka dimbani kuwakabili wenyeji Al Masry, hata hivyo Wazanzibar hawa watakuwa na kibarua kigumu cha kuhakikisha wanasonga mbele katika mashindano hayo.

Hii ni kutokana na Malindi FC kupokea kichapo cha mabao 4-1 kutoka kwa Waarabu hao katika mechi ya kwanza nyumbani, na ili isonge mbele katika mashindano hayo, italazimika kupata ushindi wa kuanzia mabao 4-0.

Nipashe inapenda kuwakumbusha wachezaji, viongozi na mashabiki wa klabu hizo tatu za Tanzania kuwa kwenye soka na ndani ya dakika 90, lolote linaweza kutokea.

Yanga, Azam FC na Malindi, huu ni muda wa kuonyesha kwamba hakuna kinachoshindikana mahali ambapo kuwa nia na malengo ya kufanya vizuri.

Ushindi, au matokeo chanya yanaweza kupatikana kwenye uwanja wa nyumbani hata ugenini. Huu ni wakati wa kuonyesha kwamba timu zetu hazikupata tiketi ya kushiriki michuano hiyo kwa kubahatisha. Kikubwa ni kila mchezaji anapokuwa au anapopoteza mpira, kupambana na kuhakikisha anatekeleza majukumu ili kuhakikisha ushindi unapatikana kwa nguvu, mbinu na akili kwa kuwa tunaamini makocha wameshatekeleza wajibu wao na kilichobaki ni kwa wachezaji dimbani.

Kama mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba waliweza kuwavua ubingwa vigogo Zamalek wakiwa nyumbani kwao Cairo nchini Misri, kwa nini Yanga ishindwe "kupindua meza" kwa Zesco ambayo inajivunia kutopoteza mchezo wowote wa kimataifa kwenye uwanja wake wa Levy Mwanawasa?


Historia au rekodi, zinawekwa ili zivunje, Yanga huu ni wakati mwingine wa kupambana na kupata matokeo mazuri, ambayo si yatawafurahisha mashabiki wenu tu, bali pia yataipa heshima nchi kwa kuendelea kushiriki katika mashindano hayo makubwa katika ngazi ya klabu barani Afrika.

Sisi tunaamini Yanga ina uwezo wa "kupindua meza" huko Ndola na kurejea nyumbani kifua mbele kwa kutinga hatua ya makundi. Kamwe wachezaji wa Yanga wasiingie uwanjani wakiamini kwamba hata wakipoteza mchezo wa leo, basi wataangukia kwenye mashindano mengine ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Ni vema kikosi cha Yanga, kikaingia kwenye Uwanja wa Levy Mwanawasa kikiwa na zaidi ya nguvu waliyokuwa nayo Botswana wakati wanacheza mechi ya marudiano dhidi ya Township Rollers, ambayo ilimalizika kwa kupata ushindi wa bao 1-0 na kusonga mbele. Ukweli huo pia unawezekana kwa Azam FC na Malindi, ambao wanahitaji kupata ushindi mnono na hatimaye kusonga mbele katika michuano hiyo ya Kombe la Shirikisho Afrika licha ya kwamba walipoteza mechi zao za awali.

Kila la kheri Yanga, Azam FC na Malindi FC. Mungu ibariki Tanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Zahera, Ndayiragije kama wamefanya hivi ushindi upo

Na Focus Nicus

**LEO** ni mtindo wa "Kupindua Meza Kibabe" pale wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa Yanga, Azam FC na Malindi FC ya Zanzibar watakaposhuka dimbani nchini Zambia, Zimbabwe na Misri kupeperusha bendera ya nchi.

Yanga inayoiwakilisha Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika itashuka katika Uwanja wa Levy Mwanawasa mjini Ndola, Zambia kuvaana na Zesco.

Wakati huo Azam ikibeba jukumu la kuhakikisha bendera ya Tanzania inapepea vema kwenye Kombe la Shirikisho Afrika itakaposhuka dimbani Bulawayo, Zimbabwe kuivaa Triangle FC kama ilivyo kwa Malindi FC ambayo itakuwa na jukumu zito la kulipa kipigo cha mabao 4-1 ilichokipata kwenye dimba la Amaan dhidi ya Al Masry ya Misri.

Kwa upande wa Yanga inahitaji ushindi wowote ama sare ya zaidi ya bao moja ili kuweza kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo kutokana na mechi ya awali Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam kulazimishwa sare ya bao 1-1.

Lakini kwa Azam yenyewe inapaswa kushinda ili kuweza kusonga mbele kufuatia mechi ya awali katika Uwanja wake wa Chamazi kukubali kipigo cha bao 1-0.

Ninaamini kwa maandalizi yaliyofanywa na wawakilishi wetu hao kupindua matokeo ugenini ni jambo linalowezekana pasi na shaka.

Jeuri ya matumaini hayo ninaipata si tu kwa sababu ya maandalizi bali pia ujasiri na rekodi ya timu hizo na makocha wao kushinda ugenini.

Hii ni kutokana na ukweli kwamba Yanga iliweza kupindua matokeo ugenini Botswana kwa kushinda bao 1-0 dhidi ya Township Rollers baada ya sare ya 1-1 Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam katika mchezo wa raundi ya awali ya michuano hiyo.

Hivyo, ni wazi itashuka dimbani leo ikiwa inajiamini na ujasiri mwingi wa kuweza kupindua matokeo kutokana na rekodi yao hiyo.

Aidha, kwa upande wa Azam kikubwa ninafahamu rekodi nzuri ya Kocha Mkuu wa timu hiyo, Etienne Ndayiragije aliyeiwezesha timu ya Taifa, Taifa Stars kupindua matokeo ugenini dhidi ya Kenya, Harambee Stars.

Wakati huu Ndayiragije akikaimu nafasi ya Kocha Mkuu wa Stars, alikiwezesha kikosi hicho kutinga raundi inayofuata ya kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), kwa kuitoa Harambee Stars kwao kwa mikwaju ya penalti 4-1 baada ya sare tasa nyumbani na ugenini.

Lakini pia ikumbukwe kuwa Azam itashuka dimbani ikiwa inajua haina cha kupoteza jambo ambalo litawafanya kuongozwa na falsafa ya kushambulia zaidi hivyo presha kubwa kuwa kwa wenyeji watakaokuwa wakitaka kulinda ushindi wao wa awali.

Si hivyo tu, bali pia makocha wa timu hizo, Mwinyi Zahera wa Yanga na Ndayiragije wote wameshawasoma wapinzani wao na wanajua nini cha kufanya ili kuweza kuibuka na ushindi leo.

Kikubwa zaidi ninachokitarajia kukiona kama Zahera na Ndayiragije wamewaandaa wachezaji wao kufanya kushambulia mwanzo mwisho ili kuwafanya wapinzani wao kujilinda zaidi na kutoruhusu kushambuliwa, ushindi lazima upatikane.

Lakini pia hilo litawezekana tu kama Zahera na Ndayiragije watakuwa wamewaelekeza wachezaji wao hususan mabeki na viungo kukabia dimba la kati, lakini pia wakicheza kitimu zaidi kwa kuzuia na kushambulia.

Ninaamini makocha wameyafanyia kazi hayo na kilichobaki ni wachezaji kutekeleza majukumu yao uwanjani, hivyo kinachotakiwa kwa wadau wa soka na Watanzania wote ni kuwaombea wawakilishi wetu hao na kuwatakia kila la kheri kupata ushindi leo ili bendera ya Tanzania iendelee kupepea katika michuano hiyo ya ngazi ya juu kwa klabu barani Afrika.

HABARI KITAIFA

# TBS yafunda wajasiriamali ubora bidhaa

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limetoa elimu kuhusu fursa wanazopata wafanyabiashara na wazalishaji ambao bidhaa zao zimekidhi viwango.

Pia TBS imehamasisha wajasiriamali kuthibitisha ubora wa bidhaa zao bure pamoja na kuzipatia majibu changamoto wanazokumbana wadau wao.

Elimu hiyo ilitolewa wakati wa mikutano ya mashauriano kati ya serikali, wafanyabiashara na wawekezaji kwa ajili ya kusikiliza changamoto zinazowakabili kwenye mikoa ya Ruvuma, Mtwara na Lindi kuanzia Septemba 24, mwaka huu na kumalizika jana.

Ufunguzi wa mkutano Songea, ulifanyika chini ya uenyekiti wa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme na kuhudhuriwa na Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, Naibu Waziri wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Sima.

Wengine waliohudhuria ni Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, Waziri wa Nchi (Uwekezaji), Angellah Kairuki na wakuu wa wilaya zote za mikoa hiyo.

Akitoa mada kwa nyakati tofauti kwenye mikutano hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Yusuf Ngenya, aliwaeleza washiriki hao kuhusiana na mabadiliko ya sheria ya fedha ya mwaka 2019 ambayo yameleta mabadiliko katika Sheria ya Viwango Na: 2 ya mwaka 2009.

Kutokana na mabadiliko hayo, Dk. Ngenya alisema shirika hilo kwa sasa inatekeleza baadhi ya majukumu ambayo awali yalikuwa chini ya iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA) ambayo kwa sasa inajulikana kama Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA).

Alisema kutokana mabadiliko hayo majukumu ya kudhibiti ubora na usalama wa chakula na vipodozi yanafanywa na TBS.

Kuhusu fursa zinazotolewa na shirika hilo kwa wajasiriamali nchini, alisema ni pamoja kuthibitisha ubora wa bidhaa wanazozalisha bila malipo kwa miaka mitatu lengo likiwa ni kuwawezesha kupanua soko la bidhaa zao na kuwaondolea vikwazo vya kibiashara.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, serikali imeanzisha utaratibu huo ili kuwasaidia

wajasiriamali kuzalisha bidhaa zenye ubora.

Alisema kuwa endapo wajasiriamali hao watathibitisha bidhaa zao itawasaidia kuzalisha bidhaa endelevu ambazo zitakuwa na soko kila mahali ikiwamo masoko ya kikanda.



Ofisa Viwango Mwandamizi wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Joseph Ismail (kushoto), akitoa mada kwa washindi wa shindano la vinara wa mkaa mbadala lililoandaliwa na Ofisi ya Makamu wa Rais mwaka 2018, wakati wa mafunzo ya kiufundi ya kuwawezesha kuzalisha bidhaa zenye ubora ili kukidhi viwango vya kimataifa, yaliyoandaliwa na Taasisi ya IMED, jijini Dar es Salaam jana. Washindi hao ni watengenezaji wa mkaa mbadala, mashine za kutengenezea mkaa huo na majiko yake. **PICHA: JOHN BADI**

## Mwanafunzi atoweka kitatanishi nyumbani

**Na Gidion Msabula,** TUDARCo

MWANAFUNZI wa Kidato cha Pili katika Shule ya Sekondari Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam, Emmanuelina Rwerengela (17) (pichani), amepotea katika mazingira ya kutatanisha.

Mwanafunzi huyo mkazi wa Upanga mtaa wa Alykhan nyumba namba 289, amepotea tangu Septemba 20, mwaka huu.

Mama wa mwanafunzi huyo, Godebertha Kajukana, akizungumza na gazeti hili, alisema alitoka nyumbani kwao akiwa amevaa sare za shule akienda shuleni na hakurudi tena.

Alisema wametoa taarifa kituo cha Polisi Selander Bridge na kufungua jalada namba SBR/RB/2072/2019.

Aidha, mama huyo amewaomba watakaomwona binti yake wawasiliane na familia kupitia namba 0754362595.



# Shule yapongezwa mafanikio ya kitaaluma

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE ya St. Anne Marie Academy ya jijini Dar es Salaam, imepongezwa kutokana na mchango wake katika elimu na kupewa cheti pamoja na shule mbalimbali nchini kutambua mchango huo.

Vyeti hivyo vilitolewa jana Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, kwa shule mbalimbali zilizofanya vizuri zaidi.

Hafla hiyo iliyofanyika katika ukumbi wa PTA viwanja vya Sabasaba na ilihudhuriwa pia na Ofisa Elimu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Hamis Lissu na wakuu wa shule mbalimbali za umma na za binafsi.

Cheti cha St. Anne kilipokewa na mkuu wake, Gladius Ndyetabura, ambaye aliishukuru serikali hasa Mkoa wa Dar es Salaam kwa kutambua mchango wake kwenye maendeleo ya kitaaluma.

Ndyetabura alisema pongezi walizopata kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, zitawapa motisha wa kuendelea kufanya vizuri zaidi kitaaluma na kamwe hawawezi kubweteka.

Alitaja siri ya mafanikio ya shule yake kuwa ni kufundisha kwa bidii na kufuatilia maendeleo ya kitaaluma ya wanafunzi wake na kwamba mwaka huu wanatarajia kufanya vizuri zaidi kwenye matokeo ya darasa la saba.

"Kusimamia nidhamu ya wanafunzi na kushirikiana na wazazi ni moja ya siri za mafanikio hya shule hii na pongezi tulizopata ni motisha kwamba tunatarajia kufanya vizuri zaidi ya hapa," alisema

Ndyetabura alisema kwenye matokeo ya darasa la saba mwaka 2018, St Anne Marie ilikuwa ya kwanza kwa Wilaya ya Ubungo, ya kwanza kwa Mkoa wa Dar es Salaam na ya sita kwenye ngazi ya kitaifa.

"Tumekuwa tukifanya vizuri mwaka hadi mwaka kwenye matokeo ya wilaya, mkoa na kitaifa na kutokana na maandalizi mazuri tuliyoyafanya kwa wanafunzi wetu mwaka huu tunatarajia kufanya vizuri sana kwenye matokeo ya darasa la saba," alisema.

Aliwashukuru wazazi wa wanafunzi kuwa wamekuwa chachu ya ushindi wa shule hiyo kutokana na ushirikiano wanaotoa kwa uongozi wa shule hiyo kuanzia shule ya msingi hadi sekondari.

Ndyetabura aliwashukuru pia walimu wa shule hiyo kwa namna wanavyojituma usiku na mchana kuhakikisha wanafunzi wanaofanya mtihani wanapata alama za juu.

# Apigia debe bima afya wachimbaji madini

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

MWENYEKITI wa Kamati ya Bunge ya Madini, Dunstan Kitandula, ameutaka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kutengeneza mpango wa kutoa bima ya afya kwa wachimbaji wadogo.

Kitandula alitoa rai hiyo juzi alipotembelea banda la NHIF kwenye maonesho ya pili ya teknolojia bora ya uwekezaji katika sekta ya madini yanayoendelea mkoani hapa.

Alimtaka Meneja wa Mfuko huo Mkoa wa Geita, Elias Odhiambo, kutengeneza mpango wa kutoa bima hiyo kwa wachimbaji wadogo kwa kuwafuata kwenye maeneo yao ya kazi, migodi isiyo rasmi na inayomilikiwa kisheria ili kuhakikisha kundi hilo linapata matibabu kwa uhakika.

Kwa mujibu wa Kitandula anahitaji kuona kundi hilo linapatiwa bima ya afya kwa kuwa bila kuwa na afya njema haliwezi kuchangia pato la taifa. Aliutaka mfuko huo kujielekeza haraka kwa wachimbaji hao .

"Rai yangu kwenu NHIF hakikisheni mnatengeneza mpango huo haraka. Muwafuate wachimbaji wadogo kwenye maeneo yao ya kazi migodini wapate bima kupitia mfuko huu kwani wana changamoto kubwa kwenye afya wanapopatwa na majanga," alisema.

Odhiambo alimhakikishia mwenyekiti huyo kuwa mfuko huo uko kwenye mpango wa kuanza kutoa bima kwa mtu mmoja mmoja na kwamba utaratibu huo utakapokamilika watawafikia wachimbaji hao.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Maabara ya Kupima Madini, Mhandisi Simon Shinshi, aliiomba serikali kutoa elimu juu ya sheria mpya ya madini ya mwaka 2018 kwa wachimbaji wadogo.

Alisema baadhi ya wachimbaji hawatambui mabadiliko ya sheria hiyo ya madini na kuongeza kuwa hatua hiyo itaondoa migogoro kwenye maeneo yao ya kazi baina ya wachimbaji na serikali pamoja na wadau na uwekezaji hasa kwenye migodi ya wachimbaji wadogo.

Pia aliwataka wachimbaji wa madini wakubwa, wadogo na wa kati kufika kwenye maonyesho ya pili ya teknolojia ya uwekezaji sekta ya madini yanayoendelea kwenye kiwanja cha CCM mkoani hapa kujionea zana mbalimbali za teknolojia ya kisasa katika upimaji wa madini na uchimbaji.



Wanaharakati wakisheherekea wakati wa uzinduzi wa Ilani ya uchaguzi ya wanawake katika Tamasha la 14 la TGNP Mtandao, kwenye viwanja vya Mabibo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MUHIDINI MSAMBA**

# Askofu aongoza mazishi rubani mwanafunzi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

ASKOFU Dk. Solomon Masangwa wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kaskazini Kati, jana aliongoza ibada ya mazishi ya aliyekuwa mwanafunzi wa urubani, Nelson Olotu (25), aliyefariki dunia kwa ajali ya ndege Septemba 23, mwaka huu, eneo la Seronera, Serengeti mkoani Mara.

Katika ajali hiyo, pia mtoto wa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Tanzania, Jenerali Venance Mabeyo, Nelson Mabeyo, ambaye alikuwa rubani wa ndege namba 5H-AAM ya kampuni ya Auric Air, alipoteza maisha.

Akizungumza katika ibada hiyo iliyofanyika katika Usharika wa Sasi, Mtaa wa Ilmeshorori, Askofu Dk. Masangwa aliwapa pole wazazi na ndugu wote walioguswa na msiba huo na kuwataka kuwa watulivu katika kipindi cha majonzi.

"Binadamu siku zetu za kuishi hapa duniani fupi na zimejaa dhiki, hivyo hakuna ajuaye siku wala saa ya kifo kitakapompata. Kutokana na fumbo hili inatupasa kila mmoja kukesha tukiomba," alisema.

Alisema ajali za ndege zinasababishwa na mambo mbalimbali kuanzia inaporuka, ikiwa angani na inapotua, hivyo ni suala la kumwachia Mungu.

"Baadhi ya sababu hizo ni makosa ya rubani, matatizo ya kiufundi, hali ya hewa, vyuma, wakati wa ndege kupaa na wakati wa kutua. Mambo hayo husababisha ajali na katika hili hakuna wa kulaumiwa," alisema.

Aidha, alisema katika mazingira hayo, ni vigumu kumlaumu mtu yoyote kwa sababu hata rubani akijitahidi kukwepa ajali, bado mazingira ya ajali yanaweza kuwapo.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqarro, alitoa salamu za pole kwa niaba ya serikali na kusema kazi ya Mungu haina makosa.

"Huyu Nelson angemaliza safari ya masomo yake angetusaidia sana serikali na taifa lakini makusudi ya Mungu lazima yatimizwe na tumwachie yeye (Mungu)," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, alitoa pole na kusema hakuna mwenye jibu kwa nini mtu mwenye umri mdogo kama walivyo vijana hao waliofariki dunia katika ajali hiyo na katika kipindi hiki ambacho wazazi wao walikuwa wakiwahitaji kuliko kipindi chochote. "Mahali salama na pekee ni kujikabidhi mikononi mwa Mungu,"alisema.

Katibu wa Chama cha Marubani nchini, Khalid Liqbal, alisema Olotu alikuwa mpole, mnyenyekevu, msikivu na mwenye kupanga kujifunza zaidi.

Pia alisema vifo vya vijana hao Nelson Olotu na Nelson Mabeyo ni pigo kubwa kwa taifa na sekta ya anga.

## Fedha uchaguzi mitaa kaa la moto

INATOKA UK. 2

ya kuchukua fomu bado anajiita mwenyekiti wa kijiji. Kwa hiyo msimamizi wa uchaguzi lazima atafsiri itakapofika Oktoba 22, mwaka huu, kuna tukio gani linafuata hapo kwa mujibu wa suala zima la ukomo,"alisema.

Jafo alisema Makatibu Tawala wa Mikoa wao ni waratibu wakuu wa uchaguzi katika halmashauri watambue kuwa wana kazi kubwa sana kuhakikisha unafanyika vizuri.

Aliwasisitiza kuhakikisha wanaratibu vizuri uchaguzi huo ili wananchi waweze kushiriki katika uchaguzi wakiwa na imani kuwa viongozi wao wameandaa uchaguzi mzuri.

Awali, Katibu Mkuu Tamisemi, Mhandisi Joseph Nyamhanga, alisema katika kikao hicho watajadili changamoto zilizopo ngazi ya mikoa na halmashauri ili kuwa na uelewa na mwelekeo wa pamoja wa maandalizi ili kufanikisha uchaguzi huo kwa kiwango kikubwa.

Alibainisha kuwa Ofisi hiyo imeshakamilisha maandalizi yote muhimu ya uchaguzi huo na nyaraka mbalimbali zimeandaliwa na kusambazwa ikiwamo kanuni na muongozo wa uchaguzi huo.

Pia alisema ofisi hiyo imeratibu upatikanaji wa fedha na tayari zimeshatumwa kwenye sekretarieti za mikoa yote na anaamini zimeshatumwa kwenye Halmashauri kwa ajili ya maandalizi ya uchaguzi huo.

Alisema inakadiriwa kuwa na vituo vya kupigia kura 110,000, hivyo lazima kuwapo na usimamizi wa vituo.

## Dk. Tenga, wenzake wataka yaishe

INATOKA UK. 2

ya zaidi ya Sh. Milioni 36 kinyume cha sheria.

Kadhalika mahakama hiyo imetaifisha madini hayo kuwa mali ya serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hukumu hiyo ilisomwa jana na Hakimu Mkazi Mkuu Simba baada mshtakiwa huyo ambaye pia ni mwanafunzi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam.

Hakimu alisema kwa kuwa mshtakiwa amekiri makosa yake mwenyewe na kwamba hajaisumbua mahakama, imemkuta na hatia dhidi ya tuhuma hizo.

Kabla ya kutolewa adhabu hiyo, Wakili wa Serikali Jacqueline Nyantori, alidai kuwa kwa sababu mahakama imemtia mshtakiwa hatiani upande wa Jamhuri unaomba itoe adhabu kali ili iwe fundisho. Pia, aliiomba mahakama kutaifisha madini yote kuwa mali ya serikali.

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa Septemba 21, mwaka huu katika Uwanja wa Ndege wa Mwalimu Julius Nyerere, Dar es Salaam, mshtakiwa alikutwa akisafirisha madini aina ya Scapolite yenye uzito wa gramu 996.50, Sperssartite gramu 487, Tanzanite gramu 44, Quarts gramu 126, Citrine gramu 174, blue agate gramu 101.80, Toumarine gramu 16, Aquamarine gramu 14.30 na Supphire gramu 5.04 yote kwa pamoja yakiwa na jumla ya Sh. Milioni 36.5 bila kuwa na kibali.

# Ujasiriamali wamaliza punda, wauzwa nje

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

PUNDA kihongwe wengi wilayani Longido mkoani Arusha , wameibwa na kuuawa kwa wingi kuanzia mwaka 2016 hadi sasa kwa lengo la kupata ngozi zao ili kuzalisha bidhaa za wajasiriamali.

Akizungumza jana kwenye mafunzo yaliyotolewa na shirika lisilo la kiserikali la ASPA linalojihusisha na ulinzi wa wanyama, Ofisa Mtendaji Kata ya Matale, Yohana Moyaseck, alisema, punda wengi waliibwa na kuuzwa nchi jirani wengine Dodoma.

"Punda wameibwa sana mwaka 2016, biashara ilikuwa imeshamiri mno na wameisha ndani ya jamii zetu kwa sasa hakuna tena makundi makubwa ya wanyama hayo," alisema Moyaseck.

Alisema jamii za wafugaji zinashindwa kuhamahama kutafuta malisho ya mifugo, kwa sababu hakuna punda wa kubeba mizigo kwani wameisha kutokana na wizi na kuchinjwa na wajanja hao.

Aliwaambia kuwa wameibwa kutokana na jamii kutowathamini, kuwaacha wakizurura ovyo bila uangalizi kama wanavyofanya kwa wanyama wengine wafugwao. "Punda hawana uangalizi,kama jamii tumechangia kuibwa na kuuawa, wameachwa wakizurura, hivyo kuibiwa kwao ni kwa urahisi sana," alisema Meyaseck.

Aidha, aliitaka serikali kuboresha sheria ya wanyama wafugwao na kumpa kipaumbele punda, kwani hata huduma za kiafya hawazipati ikiwamo chanjo pamoja na kuogeshwa( dipu).

"Punda hawathaminiwi. Hali zao ni mbaya na hii ni kutokana na ukosefu wa elimu ndani ya jamii ,wengi wao huamini punda hana haki kama wanyama wengine, serikali itusaidie kuweka mkazo katika sheria,"aliomba Meyaseck.

Alifafanua kuwa kutokana na wizi wa punda kushamiri, jamii kwa kushirikiana na viongozi wa mila wamepitisha sheria, mtu yeyote atakayekamatwa kwa wizi atapigwa faini ili iwe fundisho kwa wengine.

Alisema sheria hiyo inambana mtu anayeiba punda mmoja kutozwa faini ya ng'ombe watano na hiyo sheria imeanza kutumika sasa. " Punda hawa hawaendi machungani kuchungwa kama mifugo mingine,wanazurura kujitafutia chakula na maji. Watu wanawakumbuka nyakati za kubeba mizigo tu," alisema.

Daktari wa Mifugo Tarafa ya Engarenaibor, Lothi Laizer, alisema wanyama waliosahaulika na jamii ni pamoja na punda lakini paka na mbwa ambao wanapatiwa chanjo sawa na wanyama wengine.

"Engarenaibor tunatoa kinga ,tena mimi nikienda kwenye kuwatibu wanyama hao siwaoni ninatambua wanafugwa katika familia hivyo sitoi chanjo, hadi waletwe walikofichwa," alisema Laizer.

Ofisa Elimu Ustawi wa Wanyama wa Shirika la ASPA lenye makao makuu jijini Arusha, Diana Msemo, aliwataka viongozi hao waliotoka kata

mbalimbali za pembezoni mwa wilaya hiyo, kuwa mabalozi wazuri katika ulinzi wa punda.




Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya ulinzi ya SGA, Eric Sambu, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati wa kuadhimisha miaka 35 ya kutoa huduma za ulinzi nchini. Kulia ni Meneja wa Wateja na Mawasiliano wa kampuni hiyo, Aikande Makere. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wenye bucha walilia magogo

**Na Allan Isack ,** ARUSHA

WAKATI mwisho wa kutumia magogo kukata nyama kwenye mabucha ni Jumatatu ijayo, chama cha wauza nyama jijini Arusha, (Wanjamuco), kimeiomba

serikali iwaongezee muda wa kununua vifaa vya kisasa vya kukatia kitoweo hicho.

Hatua hiyo inayoweza kutafsiriwa kuwa ni kuiomba serikali iwaruhusu waendelee kutumia magogo, inakuja kwa maelezo kuwa vifaa vya kisasa huuzwa ghali.

Hayo yalisemwa jana na Mwenyekiti wa Wanjamuco, Alex Lesika, wakati alipokuwa kwenye maonyesho ya vifaa vya kuchakata nyama, yaliyofanyika katika viwanja vya machinjio ya nyama ya Jiji la Arusha (Arusha Meat) yaliyoenda sanjari na utoaji wa elimu kwa wauzaji wa nyama. Alisema muda uliopangwa na serikali wa kuwa na vifaa hivyo unamalizika Septemba 30 mwaka huu, ila idadi kubwa ya wauzaji wa nyama wameshindwa kukamilisha ununuaji wa vifaa hivyo, ikiwamo kuwa na mabucha ya kisasa yenye fremu za chuma aluminium kutokana na vifaa hivyo kuuzwa kwa bei kubwa.

Alisema kuwa pamoja na kwamba walishawahi kuongezewa muda kipindi cha nyuma, changamoto kubwa inayowakabili ni vifaa hivyo kuuzwa bei kubwa.

Waliiomba serikali kuwatazama kwa jicho la huruma na kuwaongezea muda hadi Machi, 30 mwaka ujao, ili kila mmoja wao awe anatumia vifaa hivyo.

Kaimu Msajili wa Bodi ya Nyama Tanzania ,Imani Sichalwe, aliwataka wafanyabiashara hao, kuzingatia muda uliopangwa wa ukomo wa matumizi ya magogo ya miti kwenye mabucha.

Alisema kuwa serikali hatoacha kuwachukulia hatua wauzaji wa nyama, kuanzia wiki ijayo Septemba 30.

Alisema watakaokaidi kutumia magogo ya plasitiki kwa kisingizio kuwa yanauzwa kwa gharama kubwa watakumbana na mkono wa sheria.

Alikumbusha kuwa awali serikali iliweka ukomo wa matumizi ya magogo ya miti kwenye

mabucha ifikapo Januari 31, 2019 na baadaye iliongeza muda hadi Septemba 30 huku ukarabati wa machinjio ukiwekewa ukomo Disemba 31 mwaka huu.

Katika hatua nyingine Sichalwe alisema bodi ya nyama imeyafungia mabucha 12 ya nyama, baada ya kufanya ukaguzi wa mabucha 235 jijini Arusha na kubaini kuwa yanaendeshwa kinyume na taratibu.

## Serikali yawakemea wabakaji wanafunzi

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Longido, amewakemea watu wanaowabaka wanafunzi na kuwapa mimba ututoni pamoja na kukwamisha kufikia ndoto zao za kusoma.

Mkuu huyo wa wilaya Frank Mwaisumbe, alisema hayo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, alipokuwa akizungumza katika mahafali ya ya Shule ya Msingi ya Arusha Alliance iliyopo jijini hapa.

Mwaisumbe alisema serikali haitavumilia kuona vitendo hivyo vikiendelea na itawachukulia hatua kali za kisheria wale wote watakaobainika kujihusisha na vitendo hivyo dhidi ya wanafunzi.

"Waacheni wanafunzi wasome kwa manufaa yao ya baadaye na ni kwa nini kwanza uwafuate watoto wadogo, ilihali wako watu wazima ambao wako na akili timamu na hata wanaohitaji kuolewa na kuanzisha familia na kulea watoto ,"alisema Mwaisumbe,

Aliwasihi wanafunzi kuzingatia maadili mema waliyofundishwa shuleni hapo na kuacha kujihusisha na makundi maovu mitaani, ikiwamo ngono na kutumia mihadarati

"Jibidiisheni katika masomo na kujiendeleza kielimu kwani elimu mliyoipata hapa ni mwanzo tu wa safari ya kimasomo, ambayo iko mbele yenu, kwani mtatakiwa msome hadi vyuo vya elimu ya juu, ili muweze kutimiza ndoto mlizojiwekea,"aliwasihi Mwaisumbe.

Awali akimkaribisha mgeni rasmi, Mwalimu mkuu wa shule hiyo Silas Msuya, alisema kuwa shule hiyo ilianzishwa mwaka 2007, ikiwa na wanafunzi 18 ambapo mpaka sasa wapo 800.

Aliongeza kuwa katika mahafali hayo wamehitimu wanafunzi 133 na kwamba wameandaliwa vyema kielimu na kimaadili, ambapo aliwasihi kuwa mabalozi wazuri wa shule hiyo pindi wawapo majumbani wakisubiri matokeo.

Aliwasihi wanafunzi hao waliohitimu elimu ya darasa la saba katika kipindi hiki kifupi cha kusubiria matokeo, kuwasaidia wazazi kazi za nyumbani na wasijiunge na makundi mabaya yatakayo waharibia ndoto zao.

"Nawasihi wazazi na walezi kuwa karibu na watoto wenu, katika kipindi hiki kifupi watakachokuwa nyumbani wakisubiria matokeo yao. Mwalee katika misingi ya kimaadili, kuwahimiza kujisomea vitabu mbalimbali na kumtanguliza Mungu kwa kila jambo wanalolifanya,"alisisitiza Msuya.

# DED Hai awavaa wahusika kadhia ya umeme sokoni

**Na Godfrey Mushi,** HAI

SIKU chache baada ya Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya kuagiza kukatwa umeme katika majengo ya halmashauri hiyo, kutokana na kushindwa kulipia huduma hiyo kwenye soko kuu la walaji la Bomang'ombe, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, amewageukia waliosababisha kadhia hiyo.

Yohana Sintoo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, akizungumza na Nipashe, alisema ofisi yake tayari imechukua hatua za kulipa deni la Sh. 280,000 lakini itawawajibisha waliohusika kutengeneza deni la miezi miwili bila sababu za msingi.

"Tumesharudisha umeme katika soko la walaji la tangu jana na katika majengo ya halmashauri pia umeme ulioagizwa na mheshimiwa DC Mkuu wa Wilaya wetu ukatwe tumesharudisha. Isipokuwa nitachukua hatua kwa watendaji wangu ambao wameleta balaa hiyo,"alieleza

Juzi, mkuu wa wilaya hiyo aliagiza kukatwa umeme katika majengo hayo ambayo pia ofisi yake ipo ndani, kwa kile alichoeleza kuchukizwa kwake na Shirika la Umeme (Tanesco) kukata huduma hiyo kutokana na deni linalodaiwa katika soko kuu.

Wakati anatoa agizo hilo Ole Sabaya alisema: "Ded -Mkurugenzi Mtendaji na watu wako mnakuja kukusanya fedha kwa miezi mitatu mfululizo, mnasahauje kulipa ankara kupitia fedha hizo? Hili nalo mnataka Rais aambiwe?

"Mimi na wewe tuwaombe radhi hawa wananchi ila wakati huo huo nakuagiza Meneja wa Tanesco ukate umeme Ofisi ya Mkurugenzi na uwashe hapa sokoni na alipe deni hilo na pia alipe bili ya miezi sita ijayo."

Akisisitiza kuwashwa kwa umeme huo katika soko la walaji, Ole Sabaya alieleza umeme huo unapaswa kuwaka kwa kuwa deni hilo haliwahusu wafanyabiashara wanaokatiwa umeme.

Zaidi, Ole Sabaya alisema hayuko tayari kufanya kazi kwenye ofisi ambayo haina huduma ya umeme na hayuko tayari kuona wananchi wanatozwa kodi ambayo hairudi kulipa deni la umeme.



Mratibu wa shirika lisilo la kiserikali la wanawake wanaopambana na Ukimwi mkoani Kilimanjaro (KIWAKUKKI), Dk. Adella Materu, akisoma risala kwa mgeni rasmi wakati wa mahafali maalumu ya wakulima wanaotumia mfumo wa jitihada shirikishi za kuleta mageuzi ya kilimo vijijini (RIPAT), katika eneo la Mamsera wilayani Rombo mkoani Kilimanjaro juzi. Mafunzo hayo na mashamba darasa yameratibiwa na shirika hilo, kwa ufadhili wa shirika la DMCDD la Denmark kwa kushirikana na washirika wenza wao waitwao PULS. **PICHA: JAMES LANKA**

# Viongozi waagizwa kusaka milioni 60

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, ameitaka Halmashauri ya Wilaya ya Hai, kutafuta mahali popote kiasi cha Sh. milioni 64 za kuunganisha umeme kwenye mradi wa kukoboa mpunga unaozalishwa katika skimu ya umwagiliaji ya Mijongweni.

Mghwira alitoa maelekezo hayo jana kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, wakati wa kikao cha mashauriano cha Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Kilimanjaro.

Kikao hicho kilihudhuriwa na Wakurugenzi na wakuu wa wilaya za Same, Mwanga, Rombo, Moshi, Hai na Siha.

Akiwa katika kikao hicho, Mghwira alisema ametoa agizo hilo kwa sababu lengo la mradi huo ni kuongeza thamani ya mpunga kwa kuukoboa, kupanga mchele kwa viwango na kufungasha katika vifungashio vinavyokubalika kimataifa.

Alisema kukamika kwa mradi huo, pia kutatoa fursa mbalimbali zitakazowainua kiuchumi wakulima waliopo katika mradi huo.

Katika mradi huo Sh. milioni 86.5 zimetolewa na serikali kuu, wahisani, Halmashauri ya Wilaya ya Hai,mfuko wa jimbo na nguvu za wananchi.

Mradi huo una jumla ya hekta 776, ambapo hekta 285 zinalimwa mpunga na hekta 140 zinapandwa mahindi na nyingine 81 eneo la kulima migomba na mboga.

Skimu hiyo maarufu kwa jina la 'Musa Mwijanga' ilianzishwa mwaka 1933 kwa ajili ya kuinua kipato cha wakazi wa ukanda wa tambarare.

Ili kuboresha mradi huo, serikali kuu na wahisani walitoa Sh. milioni 50, Halmashauri ya Wilaya ya Hai ilichangia zaidi ya Sh. milioni 20.6 wakati Mfuko wa Jimbo ulitoa Sh. milioni tano na jamii ilichangia Sh. milioni 10.9

Pia, katika kikao hicho, Katibu wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro, Jonathan Mabihya, alitoa wito kwa Tanesco kufikisha umeme mkubwa katika mradi huo na kuanza uzalishaji kama ulivyokusudiwa ikiwa ni utekelezaji wa ilani ya uchaguzi.

## Tanesco kutumia nguzo za zege

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

KATIKA jitihada za kukabiliana na kuanguka ovyo nguzo za umeme katika maeneo chepechepe, Tanesco itaanza kutumia nguzo za zege, hatua itakayochukuliwa wakati wowote kuanzia sasa.

Mhandisi wa kitengo cha miundo mbinu ya usafirishaji wa mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Tanga, Yared Ngalaba, alisema tayari wameanza mchakato wa kujenga nguzo za zege kwenye maeneo chepechepe na sehemu ambazo ardhi ina maji maji.

Kwa mujibu wa Ngalaba, mchakato huo utaanza rasmi kwa kubadili nguzo 20 zinazosafirisha umeme wa msongo wa kilovolti 66 kutoka kituo cha kuzalisha umeme Nyumba ya Mungu kilichopo Wilaya ya Mwanga hadi katika kituo cha kupoozea umeme cha Kiyungi, Moshi.

Alisema Tanesco imeanzisha kampuni maalum ya kutengeneza nguzo za zenge kwa ajili ya kukabiliana na nguzo za miti zinazooza na kuanguka katika maeneo yenye unyevu na maji maji.

Tatizo la nguzo kuanguka katika maeneo chepechepe husababisha umeme kukatika kwenye maeneo mbalimbali kutokana na Nyumba ya Mungu kuwa mchangiaji kwenye gridi ya taifa.

Aidha, Ngalaba alisema Tanesco ina zaidi ya nguzo 500 zilizopo katika maeneo yenye maji maji na kwamba nguzo hizo zinahitaji kubadilishwa na kujenga nguzo za zege ambazo zinadumu kwa muda mrefu na gharama zake ni bei nafuu. Alisema nguzo za chuma zina gharama kubwa zikifuatiwa na nguzo za miti ambazo zinahitaji kubadilishwa mara kwa mara kutokana na kuoza na kuanguka na kwamba ili shirika hilo liondokane na gharama hizo ni lazima zikajengwa nguzo za zege kwa kutumia mawe,kokoto,mchanga na saruji.

Alisema shirika hilo lina nguzo zaidi ya 463 zinazosafirisha umeme kutoka Nyumba ya Mungu hadi Kiyungi na kwamba zilijengwa toka mwaka 1967 na kwamba zimekuwa zikibadilishwa mara kwa mara kutokana na baadhi ya nguzo kuoza na kuanguka.

Mwaka 2018 shirika hilo lilibadilisha zaidi ya nguzo 80 ili kuzuia nguzo zisidondoke mara kwa mara na kusababisha umeme kukatika ovyo huku akitoa wito kwa wananchi wenye tabia ya kulima chini ya nyaya za umeme kuacha mara moja kwa ajili ya usalama wao na wa gridi ya taifa.

Aidha, alitoa wito kwa wananchi wanaoishi karibu na nguzo za chuma kuacha tabia ya kuchimba mawe,kokoto, mchanga na kuiba vyuma zikiwemo nati na bolti.

Baadhi ya watu wasio waaminifu wamekuwa wakiiba vifaa na kwenda kuuza chuma chakavu, jambo ambalo kwa mujibu wa Tanesco linaitia serikali hasara kila wakati kutokana na gharama za kuirudisha.





Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde, akizungumza na wazazi wa Kata ya Chang'ombe, katika hafla ya ufunguzi wa majengo ya madarasa ya Shule ya Msingi Changombe B, jijini Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wananchi waomba alama za mipaka

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKAZI wa Mtaa wa Ndachi Sheri Mbili jijini Dodoma, wameiomba halmashauri ya jiji kuweka alama za mipaka ili kutenga mashamba yao na maeneo mengine kwa lengo la kudhibiti wavamizi.

Walitaka alama hizo kuwekwa kwenye mashamba yaliyofanyiwa uhakiki ili kukomesha vitendo vya uvamizi wa maeneo yao, vinavyofanywa na watu wanadai kuwa wana hati miliki .

Ombi hilo walilitoa juzi jijini hapa baada ya kuwakamata watu wakiwa na vifaa vya upimaji ikiwamo mashine ya GPS, katika mashamba yao wakipima moja kati ya mashamba ya wananchi bila kutoa taarifa kwa uongozi wa serikali ya mtaa huo.

Mmoja wa wakazi hao Iddy Omary, alisema mgogoro huo wa ardhi umeibuka kutokana na mamlaka za jiji kushindwa kuweka alama hizo katika sehemu ambazo tayari zimefanyiwa uhakiki.

"Hii yote inasababishwa na kukosa alama za mipaka.Hawataki kuja kutuwekea 'bikoni' ili tuyatambue maeneo yote na kuondokana na watu wa namna hii,"alisema Omary. Aidha, aliiambia Nipashe kuwa kutowekwa kwa alama hizo kunaweza kuwa chanzo cha uvunjifu wa amani kwani kumekuwapo na baadhi ya watu ambao wamekuwa wakivamia katika maeneo hayo na kudai kuwa ni wamiliki halali.

"Tayari jiji lilishafuta hati za mashamba lakini bado tunaona kila siku watu wanakuja na wataalamu wa ardhi kuja kuendelea kupima wakati, sisi tayari tulisha fanyiwa uhakiki na kampuni nyingine iliyoletwa na mkurugenzi wa jiji,"alilalamikia Omary.

Mkazi mwingine wa mtaa huo, Sophia Ally, aliiomba serikali kulifanyia kazi suala hilo haraka ili kuepusha usumbufu ambao umekuwa ukijitokeza pamoja na viashiria vya uvunjifu wa amani wa kugombea ardhi.

"Hivi sasa baadhi ya watu wamekuwa wakijihusisha na vitendo vya uvunjaji wa nyumba ambazo zimejengwa katika eneo hili. "Leo hii tumekuja hapa tunakuta nyumba tano zimevunjwa zipo chini halafu tunawakuta hawa wanaendelea na upimaji bila kujitambulisha katika ofisi ya mtaa kwanini watu wasiwavamie na kujichukulia sheria mkononi?"alihoji Ally.

Akizungumza na waandishi wa habari katika eneo hilo mmoja wa maofisa ardhi Gilbert Mkemangwa, alisema walizingirwa na kundi hilo la wananchi wakati wakiwa katika kazi ya kupima ardhi katika moja ya eneo walilopewa na mteja.

Alisema walifika katika eneo hilo wakiwa na vifaa vyao vya upimaji ardhi ili kuweza kubaini eneo la mteja ambalo aliwapa kazi ya kulitambua kama lipo kihalali na halina mgogoro wowote lakini walivamiwa na kupokonywa vifaa vyao ikiwamo mashine ya GPS. "Tukiwa katika harakati za upimaji ndipo tulipozingirwa na watu wakidai kuwa eneo tunalopima ni la wananchi hivyo wakalazimika kuita polisi na kutuweka chini ya ulinzi hadi hivi sasa ambapo mmetuka hapa,"alisema hata hivyo alishindwa kueleza iwapo walijitambulisha na kutoa taarifa .

# Wakulima mbioni kuanzisha jukwaa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imekiagiza chama cha wakulima wa alizeti nchini (SUFA) kuanzisha jukwaa la wadau wa zao hilo kwa ajili ya kutatua changamoto zinazowakabili na kupanua wigo wa kilimo cha alizeti.

Agizo hilo lilitolewa jana na mwakilishi wa Wizara ya Kilimo Idara ya Maendeleo ya Mazao cha Uinuaji Mazao, Pembejeo za Kilimo na Ushirika, Kissa Chawe, katika kikao cha kujadili mapendekezo ya uundwaji wa jukwaa hilo kilichoandaliwa na Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV).

Kissa alisema ni muhimu wakulima kuwa na jukwaa kwa sababu ni sehemu ya kusemea changamoto zinazoikabili sekta ya alizeti.

"Ni vema mkatilia mkazo kuunda jukwaa la wakulima kwa lengo la kuwa na sauti moja ili kutatua changamoto zenu," alisema Kissa.

Alisema wakifanya hivyo itakuwa rahisi kuainisha yote yanayowakabili katika kilimo cha alizeti hapa nchini.

Mwakilishi kutoka SNV Mwanaidi Gurisha, alisema wako mstari wa mbele kushirikiana na SUFA kwa ajili ya kutatua changamoto zinazowakabili wakulima wa zao hilo.

Alieleza kuwa SNV kupitia Mradi wa Transforming Agricultural Markets (TAM), unaodhaminiwa na Shirika la Uingereza la UKAID, imekuwa ikijihusisha na wakulima wa alizeti kuwasaidiana kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili.

Hii ni pamoja na kupanua wigo wa kufanya kazi zinazohusiana na kilimo cha kisasa.

Kwa upande wake, Meneja Mkuu wa SUFA, Stephen Henry, alisema lengo la kikao hiko ni pamoja na kutaka kuungana pamoja katika jukwaa hilo ili kuhakikisha wanakuwa na sauti moja ambayo itabadilisha kilimo hicho kuwa chenye manufaa na tija kwa jamii.

Alisema wakulima wanahitaji kuona kilimo hiko kikiinuka na kuzalisha zao hilo kwa wingi ili kutosheleza mahitaji ya viwanda vya mafuta hayo.

Alisema alizeti ni muhimu kwa ajili ya kuzalisha mafuta hayo hivyo ni vema wakulima na wazalishaji wawe pamoja ili kuendeleza alizeti.

# Mahenge atoa wosia alizeti

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA.

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk.Binilith Mahenge amewataka wakulima kuchangamkia fursa ya kilimo cha alizeti ili kukidhi mahitaji ya viwanda na kupunguza gharama za uagizaji mafuta ya kula kutoka nje.

Dokta Mahenge alitoa kauli hiyo jana alipotembelea kiwanda cha kukamua mafuta ya alizeti cha Zain Oil Mills cha jijini hapa.

Alisema kutokana na kuwepo kwa viwanda vingi vya kukamua mafuta ya alizeti nchini kuna mahitaji makubwa ya malighafi hiyo viwandani, hivyo wakulima wachangamkie fursa ya uzalishaji.

Mkuu huyo wa mkoa aliwataka wakulima nchini kujiingiza kwenye kilimo cha alizeti ili kuipunguzia serikali mzigo wa kuagiza mafuta ya kula nje ya nchi.

"Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi kuagiza mafuta ya kula nje ya nchi lakini uwepo wa uwekezaji wa viwanda vikubwa kama hivi itasaidia kupunguza gharama za uagizaji huo na ninawaomba wakulima wachangamkieni kilimo cha alizeti kutokana na uwepo wa ukika wa soko,"alisema.

Alimshukuru mwekezaji wa kiwanda hicho kwa kuunga mkono juhudi za Serikali ya Rais Dk.John Magufuli ya ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Alisema uwepo wa kiwanda hicho kipya cha kukamua alizeti utanufaisha wakulima kutoka pande zote za ndani na nje ya nchi kupata soko la mazao yao kwa urahisi.

Aidha, aliwataka wakulima wa alizeti kuacha kuchafua mbegu za alizeti kwa kuweka mchanga na mawe ili kuongeza uzito kwenye mzani wakati wa kuuza badala yake wabadilike na kuuza bidhaa safi.

Pamoja na hayo, Dk.Mahenge aliwataka wawekezaji wa viwanda vya kukamua mafuta hayo kushirikiana na watafiti wa kilimo ili kupata mbegu bora zitakazokuwa zinazofaa kuzalisha mafuta mengi.

Mkurungenzi wa kiwanda cha Zain Oil Millis , Salman Gulamali, alisema kiwanda hicho kina uwezo wa kuzalisha tani 100 kwa siku na wamejipanga kununua alizeti ya kutosha kutoka kwa wakulima.

Gulamali alisema wamewekeza zaidi ya Sh. bilioni sita katika kiwanda hicho na wataendelea kuwekeza vifaa zaidi ili kuzalisha mafuta ya kutosha kuhudumia watu wengi.



# Elimu shirikishi yaimarika Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali imesema kitengo cha elimu jumuishi kimeimarishwa na kuwa na uwezo wa kuhudumia wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Simai Mohamed Said , alisema hayo wakati akijibu swali la mwakilishi wa viti maalumu wanawake, Mwantatu Mbaraka , aliyetaka kujua mikakati ya kuimarisha elimu shirikishi katika shule za Unguja na Pemba imefikia wapi.

Alisema mikakati iliyofanyika ni pamoja na kutambua takwimu za wanafunzi wenye ulemavu wa aina mbali mbali ambayo ni 6,101.

Alisema mahitaji muhimu ya elimu kwa wanafunzi wenye ulemavu yameimarishwa ikiwamo maandishi ya nukta nundu yanayotumiwa na walemavu wenye matatizo ya uoni hafifu.

Aidha alisema, mazingira katika shule yameimarishwa na kuwawezesha wanafunzi wenye ulemavu kupata huduma zote muhimu ikiwamo vyoo.

Alieleza jumla ya shule 89 zimefanyiwa marekebisho na kuwapo kwa huduma mbali mbali za mahitaji kwa watu wenye ulemavu.

"Tumeimarisha elimu mjumuishi katika shule zote za Unguja na Pemba kwa kuwatambua wanafunzi wenye mahitaji maalumu,"alisema Naibu Waziri.

Hata hivyo, aliwataka wazazi ambao watoto wao wanaishi na ulemavu wa aina mbali mbali wasiwafiche nyumbani kwani watoto wenye ulemavu wanazo haki zao za msingi ikiwamo kupata elimu kwa hivyo hakuna sababu ya kuwaficha.

"Wapo watoto wenye ulemavu wamepata mafanikio makubwa ikiwamo wasioona, kwa hiyo hakuna sababu ya kuwaficha watoto wetu,"alisema.



Wachuuzi wa vitunguu swaumu, wakiwahudumia wateja wao, katika makutano ya Mtaa wa Mkunguni na Bonde, eneo maarufu kwa biashara ya viungo vya chakula, Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Serikali kumaliza foleni Kidongochekundu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar, inatarajia kujenga jengo jipya kwa ajili ya kuwatibu wanaotumia mihadarati, kisiwani Pemba, kupunguza msongamano katika hospitali ya Kidongochekundu.

Kaimu Waziri wa Afya, Mmanga Mjengo Mjawiri, aliyasema hayo wakati akiwasilisha ripoti ya wizara yake kuhusu utekelezaji wa maagizo ya kamati ya ustawi wa jamii kwa mwaka 2018 /2019.

Alisema, wizara imechukua hatua mbalimbali kupunguza msongamano katika hospitali hiyo ikiwamo kuongeza idadi ya watoa huduma wa ushauri nasaha kutoka watatu hadi sita kwa sasa na kuendeleza ujenzi wa jengo jipya la Kidongochekundu, litakalowahudumia kwa kuwapa tiba ya methadone.

Aidha, alisema, kukamilika kwa ujenzi huo kutatoa nafasi kwa huduma nyingine zinazohusiana na maradhi hayo ili zipatikane katika hospitali hiyo ikiwamo ya ushauri nasaha.

Aliliambia Baraza la Wawakilishi kuwa ujenzi wa hospitali hiyo upo katika hatua ya mwisho na majengo mawili madogo yamefikia hatua ya kuwekwa linta na yanatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2019/2020.

Kwa upande wa nyumba za madaktari, alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya China inatarajia kujenga nyumba za wafanyakazi katika eneo la Hospitali ya Abdallah Mzee kisiwani Pemba. Alisema mkataba wa ujenzi wa nyumba hizo umeshatiwa saini Julai 30 mwaka huu ambapo kazi inatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2020/2021.

Alieleza kuwa hivi sasa wizara imekodi nyumba kwa ajili ya makaazi ya madaktari katika kisiwa cha Pemba ili kuwahudumia kwa mpango wa muda mfupi.

Alisema, kwa upande wa Unguja tayari wizara imeshakamilisha ujezi wa nyumba za wafanyakazi zenye kuchukua familia mbili ambapo hali ya fedha itakaporuhusu ujenzi utaendelea ili kuwapatia wafanyakazi na watumishi wa afya makazi katika maeneo mengine.

Akizungumzia upatikanaji wa dawa alisema umeongezeka na kufikia asilimia 90 mwaka 2018/2019 kutoka asilimia 50 mwaka 2015/2016 kwa kupatikana kwa dawa za saratani, kusafishia figo sukari na presha ambazo zimekuwa zikipatikana katika hospitali zote na vituo vya afya kwa Unguja na Pemba.

# Jamii yahimizwa kushiriki chanjo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKE wa Rais mstaafu , Salma Kikwete, amesema kufanikiwa kwa kampeni ya chanjo ya surua, rubella na polio ni hatua itakayopunguza kuenea kwa maradhi hayo ambayo huathiri maisha ya watoto wa taifa hili.

Akizungumza kwa niaba ya Waziri wa Kazi,Uwezeshaji,Wazee, Wanawake na Watoto, Maudline Cyrus Castico, alisema wakati wa uzinduzi wa kampeni ya chanjo hiyo uliofanyika katika Kijiji cha Mkwajuni Kaskazini Unguja, alisema kuwa watoto ambao hawajapatiwa chanjo hizo wana hatari kubwa ya kuambukizwa maradhi hayo, kupata ulemavu na hata kifo.

Alieleza kuwa takwimu za magonjwa hayo duniani zinaonyesha kuwa wagonjwa wameongezeka kwa kasi ambapo kwa Zanzibar idadi ya watoto wanaougua magonjwa hayo imepungua hadi kufikia 28.

Alisema kutokana na hali hiyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina lengo la kupunguza vifo vya watoto vinavyosababishwa na maradhi hayo kwa theluthi mbili ifikapo mwaka 2022.

Aidha, aliwataka wazazi kushiriki kikamilifu katika kampeni za chanjo katika vituo vilivyopangwa na kuwahakikishia kuwa dawa zinazotolewa kukinga maradhi hayo hazina madhara yoyote na zimethibitishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Naye Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya Halima Maulid, aliwataka wananchi walipe umuhimu suala la chanjo kwani inasaidia watoto katika ukuaji mzuri wa afya zao.

Aidha, alisema kuwa serikali imekuwa ikichukua jitihada kwa kushirikiana na mashirika ya Umoja wa Mataifa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia (UNICEF) ili kuwakinga watoto na maradhi mbalimbali yanayowasumbua na kutishia afya zao.

Kwa upande wake mwakilishi kutoka Shirika la UNICEF Maha Damaj, alisema mpango wa kuwapatia chanjo watoto unalengo la kuwakinga na athari ya maradhi mbalimbali yakiwamo ya polio na surua.

Wakizungumza baada ya uzinduzi wa kampeni hiyo,wananchi wa kijiji hicho waliipongeza serikali na kuahidi kuwa watahakikisha wanawapeleka watoto wao kuweza kupatiwa chanjo hiyo.

Asha Juma ni miongoni wa wakazi wa kijiji hicho,alisema kuwa baadhi ya watu walikuwa wakivumisha kuwa chanjo hizo zina madhara ambapo mtoto anayepatiwa chanjo hiyo hawezi kupata kuzaa.

Alisema jambo hilo si kweli na si kweli kuwa chanjo huleta ugumba.



**ALI KIBA** Soma UK.16

JUMAMOSI SEPTEMBA 28, 20



# ‘KIJIWE NONGWA’
## CHAZUA NONGWA SHILOLE, ROSTAM MOTO WAZIDI...

Soma UK.15

BASI SAWA



## Q Chief amshukuru Harmonize

MWANAMUZIKI Q Chief amemtaja Harmonize kama msanii wa kipekee nchini kwa kumsaidia kurudi katika gemu.

Amesema kabla ya kutoa nyimbo na mwanamuziki huyo ambaye amejiengua WCB alikuwa akifanya kazi kwa malipo madogo lakini sasa thamani yake imepanda.

"Harmonize amekuja kuwakumbusha watu kuwakumbuka wasanii waliosahaulika, ameamua kujitoa kwa ajili yangu ili kuniona naendelea," amesema Q Chief.



# 'KIJIWE NONGWA'
## CHAZUA NONGWA SHILOLE, ROSTAM MOTO WAZIDI...

KIJIWE kimesanuka! Ndivyo unaweza kusema, kwani hali si shwari ndani ya muziki wa Bongofleva baada ya wasanii wa kundi la Rostam na mwanadada Shilole, kutolena povu katika mitandao yakijamii.

Mtafuruku huo ambao umezidi kushika kasi kutokana na pande zote mbili kurusha maneno makali umesababishwa na wimbo mpya unaotwa 'Kijiwe Nongwa' kuonekana kuwagusa baadhi ya watu. Kati ya watu waliotajwa katika wimbo huo ni Shilole na Mume Wake, japo wasanii hao hawakutaja majina yao lakini ni dhahiri umewalenga kutokana na maudhui na dhana halisi katika sehemu ya shahiri lake.

Katika vitu ambavyo Shilole anasema kimemuuma ni pale katika wimbo huo kumtaja mume wake Uchebe kuwa sawa na mdudu Chawa.

"Roma na Stamina ni kaka zangu na wao wananiita mimi dada yao, lakini kwa hili kumuita mume wangu Chawa limevuka mipaka lazima niwashikishe adabu," amesema Shilole.

Katika kuonesha kwamba amekerwa, Shilole aliposti video fupi katika ukurasa wake wa Instagram kipande cha wimbo wake mpya ambao amewashambulia marapa hao kwa maneno makali.

"Hapa ni mwanzo tu kuonesha mimi siguswi kama wanavyotaka, nimetoa salamu na ujumbe wenyewe unakuja hivi karibuni," ameongeza.

Hata hivyo, Roma na Stamina wamesema hawana ugomvi na Shilole kwa sababu yeye ni kama dada yao, na kilichomo ndani ya wimbo wao ni kama mabishano yanavyotokea katika vijiwe vya vijana tu.

"Sisihatuna ugomvi na Shilole, hatukumlenga ila tulichoimba ni majibishano yanayotokea kwenye vijiwe vya vijana," Roma alijitetea.

Malumbano hayo yanazidi kuwaka moto katika mitandao ya kijamii kutokana na mashabiki wa pande mbili kuvutana kuhusu maudhui wa wimbo huo. Baadhi wanaona marapa hao hawakufanya kosa lolote na wanaomtetea Shilole wanataka waombe radhi ili kuonesha uungwana.



## Rosa Ree apagawisha Uganda

RAPA Rosa Ree, anameanza safari ya kuvuka mipaka ya nchi kufanya kolabo na wanamuziki tofauti kwa lengo la kukuza kipaji chake.

Msanii huyo anaingia katika orodha ndefu ya wasanii waliofanya kazi na wenzao wa Uganda, baada ya wiki hii kutoa ngoma kali akimshirikisha mwimbaji wa nchi hiyo Spice Diana.

Hata hivyo mwanamuziki huyo yupo mbioni kukamilisha kazi na wasanii Apass, Fik Famaika na Ghetto Kids.

## INSTA-TWITTER





**Usiniletee** za kuleta.
Za kuleta ndiyo zinakuwaje aisee-
**Idriss Sultan.**



**Hakuna** kitu kinaumiza kama kuachwa na mpenzi uliopanga kumuomba hela kesho yake-
**Kiwewe.**



## Nedy Music akumbukia msoto wa zamani

MKALI katika Bongo Fleva, Nedy Music amesema haikuwa kazi rahisi kwake kufanikiwa katika muziki kama asingethubutu kujaribu kile anachoamini anaweza.

Amesema wazazi wake hawakutaka yeye kufanya muziki kwa kile walichoamini hataweza kumudu maisha yake ya baadae.

"Nakumbuka hata nilipokuwa nikienda THT sikufahamu kama nitatoka kimuziki, lakini kutokana na uthubutu wangu nilifanya vizuri na hadi sasa nasimama kama Nedy Music," amesema.



# ALI KIBA
## ATAMANI WASANII WAPIGE KITABU

MWANAMUZIKI Maarufu Afrika Mashariki, Ali Kiba, amesema elimu ni jambo pekee linalofanya wasanii kuwa na maamuzi sahihi.

Akizungumza hivi karibuni Kiba amesema suala la elimu haliwezi kuepukika katika fani zote ili kuondokana na wizi ni kudanganywa wakati wa kuingia mikataba.

Amesema ni jukumu la watu kusaidia kuboresha elimu kwa kuwekeza vifaa na majengo kwa lengo la kuwapata wasanii na watu waliosoma vizuri.




@burudanitele

**>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

## INSTA-TWITTER

Tuffolow/ Tu-tag
@burudanitele



**Eti** ni kweli ukisali kwa kingereza ujue una matatizo machache?-**Tundaman.**



**Wale** waliokuwa wanaogopa movie za kichawi Kipindi cha utoto sasa hivi ndio wachawi.
Na wale walikuwa wanawaogopa wavuta bangi, sasa hivi wao ndio wavuta bangi. Waliokuwa wanaisema sanaa ya bongo sasa hivi wanataka wapewe hata scene moja
**Mkude Simba.**



**Muache** kutuuliza mswali, umemkaje? Umelalaje? Umekula? Tuulizane maswali ya biashara, gari lako umeweka mafuta? Umelipia king'amuzi chako? Hayo mambo ya umekula, tumachieni sisi wenyewe na madada wa kazi-**Maimatha Jesse.**

# Kuumbe!



# ZAIDI YAKE

## ZARI KILA KUKICHA ANANOGA

ALIYEKUWA mpenzi na mama watoto wa mwanamuziki staa, Diamond Platnumz, Zari amejipambanua kwamba kifedha bado yupo vizuri na kwamba hawezi kujuta kuachana na baba watoto wake huyo.

Kila kukicha akitumia ukurasa wake wa Instagram, Zari maarufu kama The Boss Lady, anatupia picha tofauti akionesha jinsi anavyokula maisha na kutumia vyema fedha zake.

Zari ambaye ni mfanyabiashara mwenye mafanikio, amekuwa akijiaminisha kwa mashabiki wake kwamba yeye mwenyewe anaweza kupata nyumba nzuri ya kuishi, kula vizuri na kumiliki magari ya kifahari bila kutegemea mwanamume.

Mrembo huyo wiki hii hakuiacha hivihivi kwani wakati akifurahia siku yake ya kuzaliwa alitupia picha ya mjengo wake mpya aliounua nchini Afrika Kusini kama zawadi yake.

Kupitia ukurasa wake huo, Zari ameandika maneno ya kumshukuru Mungu kwa kumuongezea miaka.

Ujumbe huo umepokelewa kwa maoni tofauti katika mitandao ya kijamii, huku wengi wakimpongeza mwanamke huyo na kumtakia maisha marefu na yenye furaha.


Katika ukursa wake huo Zari aliandika, "Asanteni kwa wote ambao mmeniletea zawadi kuelekea "Birthday" yangu, nimejizawadia mwenyewe nyumba mpya, nashukuru kwa baraka za kuona naongeza mwaka mwingine, sina cha kukulipa Mungu. Asante kwa neema zako".

Miaka 39 iliyopita, tarehe kama ya leo Septemba 23, ndiyo siku mwanamama huyo Zarina Hassan mwenye asili nchini Uganda alizaliwa na jana Septemba 22 aliwaalika ndugu, jamaa na marafiki katika sherehe za awali kwa ajili ya kupata chakula na vinywaji nchini humo.

# SI WCB TU

## Wengine walitoka sasa wanawika

**Na Adam Fungamwango**



HABARI ya mjini kwa sasa ni juu ya msanii Harmonize, jina lake halisi likiwa ni Rajab Kahali, kujiondoa kwenye kundi ya WCB na kuamua kufanya kazi kivyake.

Mashabiki wa muziki wa kizazi kipya kwa sasa wamekuwa na mitazamo tofauti, kila mtu akiongea lake juu ya msanii huyo kuondoka chini ya usimamizi wa WCB, ambayo ndiyo iliyomuibua kutoka kusikojulikana na kumpa umaarufu mkubwa.

Ikumbukwe kuwa Harmonize alianza kuvuma mwaka 2015 alipotoa ngoma yake kali 'Aiyola'.

Hapo kila mtu alimfahamu, kabla ya 2016 kutoa ngoma mbili 'Bado', na 'Matatizo'.

Amedumu kwenye kundi hilo kwa miaka minne na sasa ameamua kufanya kazi kivyake.

WCB ni kundi linalojumuisha wasanii wanaofanya kazi chini la lebo hiyo, pamoja na studio inayoitwa Wasafi records.

Baadhi ya wasanii waliobaki sasa ni Lavalava, Rayvanny, Queen Darlin, Mbosso na wengineo.

Hii siyo mara ya kwanza kwa wasanii kuondoka kwenye makundi yao ya awali yaliyowatoa chini na kuamua kujitegemea wenyewe. Hawa ni baadhi ya wasanii waliokuwa kwenye makundi mbalimbali na baadaye kuamua kufanya kazi kivyao.

### Profesa Jay

Kwa sasa ni Mbunge ya Jimbo la Mikumi. Kabla ya kuwa Mbunge alikuwa tayari ni staa mmoja wa waanzilishi wa muziki wa kizazi kipya. Alikuwa kwenye kundi la Hard Blasters Crew (HBC) na alijiunga mwaka 1989.

Mwaka 2000 kundi hilo lilitoa albamu ya 'Funga Kazi' iliyokuwa na ngoma moja kali iliyoitwa 'Chemsha Bongo' iliyoleta mapinduzi makubwa kwenye muziki huo.

Mh. Joseph Haule, maarufu kama Profesa Jay, alijiengua kwenye kundi hilo na kufanya muziki kivyake kwa staili yale ya 'hip hop' ambako aliendelea kufanya vizuri hadi leo, licha ya kwamba ni Mbunge, lakini bado hajaacha masuala yake ya muziki.

### Inspekta Haroun

Ni msanii, mwimbaji wa staili moja inayoitwa 'rap katuni'. Inspekta Haroun ambaye jina lake lingine alilopachikwa na mashabiki ni 'babu', ni mmoja wa wasanii maarufu hapa nchini japo kwa sasa hasikiki kivile kama zamani.

Alitika katikati ya miaka ya 2000 kwa ngoma zake kali kama 'Asali wa Moyo', 'Mtoto wa geti Kali' na nyingine nyingi. Huyu pia ni mmoja wa wasanii alianzia kwenye kundi, lakini baadaye wakayoyoma kivyao.

Huyu kwanza alikuwa kwenye kundi la Gangwe Mob akiwa na Luteni Kalama. Baadaye kundi hilo liliungana na TMK Wanaume na kuwa kundi moja.

Kama kawaida ya wasanii wengi, alipoona anaweza kusimama mwenyewe kwa miguu yake aliamua kujitoa na kufanya kazi kivyake.

### AY

Sina haja ya kumzungumzia sana msanii huyu, kwani ameshavuka kutoka kuwa msanii wa kitaifa na kuwa msanii wa kimataifa.

Ni mmoja wa wasanii wa mwanzo kabisa wa rap na hip hop nchini. alianza kuwika akiwa kwenye kundi lililokuwa na nguvu kubwa nchini, East Coast Team (ECT) lililokuwa na wasanii wengi waliokuja kupata umaarufu mkubwa nchini.

Naye pia anakuwa kwenye orodha ya wasanii walioibuliwa na lebo au kundi na kuamua kujitafutia mkate wake wa kila siku kivyake.

### Kassim Mganga

Kwa sasa ni maarufu sana kwenye nyimbo za mduara. Mganga anakumbukwa kwa ngoma yake iliyohiti sana 'Awena'.

Huyu alianza kupata umaarufu akiwa kwenye kundi la Tip Top Connection. Baadaye kama kawaida, na yeye pia akaamua kuondoka kama vile mtoto anapoamua kuondoka kwa wazazi wake, baada ya kujiridhisha kuwa anaweza kujitegemea na kujitafutia mwenyewe.

### Rich Mavoko

Huyu kidogo yuko tofauti na wenzake wote. Mavoko alianza kupata umaarufu akiwa nje ya kundi la WCB. Katika hali iliyowashangaza wengi mwaka 2016, aliamua kuingia kwenye kundi hilo, na kutumia lebo yao na kufanya kazi na wasanii walio kwenye kundi.

Kwa bahati mbaya, badala ya kuwa juu kama wenzake, akawa kama anashuka kimuziki.

Mwaka jana, 2018 ndipo alipoamua kujitoa rasmi na sasa ameamua kufanya shughuli zake mwenyewe.

# Vijimambo

1. Wanasema eti mimi chizi. Watanzania bwana kwa figisu! - Majuto Magazeti, Miyomboni Iringa.
2. Duuh! Jamani kazi kwanza, kuselifika baadae - Bahati, Kiwalani DSM.
3. Hii mitandao ya kijamii inatutesa. Kwa hii selfii kila mtu atakomenti 'nice' - Agatha Mbale, Moro Town.
4. Natafuta picha ya kutupia 'whatsap' - Dullah Dimoso, Tabata DSM.
5. Kijana hiyo simu imepitwa na wakati, ipeleke makumbusho - Oiso, Nyaishozi Tegeta DSM.
6. Ukisikia uchizi taslimu, basi ndio huo. Simu ya mezani na selfii! - Mama Nah, Manzese DSM.
7. Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.
8. Yes, hapa sasa pozi limekubali, ngoja nijifotoe sasa - Samwel Sungi, Utemini Singida.
9. Hii simu vipi, mbona sioni sehemu ya kujiselfisha? - Msabaha J. Msabaha, Mikindani Mtwara.
10. Lazima baby wangu aikubali hii picha, si selfii ya kitoto - Beneali Moussa Beneali, Migombani Zenji.
11. Hii inaitwa 'ekotite', muulizeni Kofi Olomide anaifahamu sana - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
12. Kweli ushamba mzigo. Wewe, sio kila simu unaweza kujiselfisha nayo - Mariam Beneali, Migombani Zenji.
13. Ha ha haaa, usitake ncheke mie! Hebu rudisha simu ya watu ofisini - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
14. Hapo 'chacha'! Disco limeingia watu wa kabila lileee! Mtajuta kuijua selfii - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
15. Mnashangaa nini? Mie sijiselfishi kama nyie, mie fundi simu jamani - Dully, Kiembesamaki Zenji.
16. Ukitaka kugombana naye, mwambie kuwa hiyo simu haiselfishi - Antar, Makumbusho Kijitonyama DSM.
17. Hapa sasa mademu wote wa 'bush stars' wangu - Nahoja Mazengo, Mbande Chamazi DSM.
18. Wewe! Hebu acha ushamba wako bwana, unawaabisha Wairinga wenzip - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
19. Hiyo selfii yako inanitia homa kwa kicheko - Bimkubwa Ausi Juma, Michenzani Unguja.
20. Hilo ndio tatizo la Wahehe wakishaingia mjini - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
21. Kaa hivyo hivyo, baada ya 'masaa' kadhaa utaona sehemu ya kupigia picha inajionyesha - Judi, Mbezi Mwisho DSM.
22. Watu wa kizazi hiki, kweli wamedata. Haya bhana na selfii yako bandia - Mama Nah, Manzese DSM.
23. Kweli ushamba zigo la miba. Tangulini simu hiyo ikatumika kwa selifii? - Judi, Mbezi Mwisho DSM.
24. Hiyo ni sawa na kuosha mchele kwenye mto wa maji mengi. Utapata taabu sana - Semeni Mpanjira, Kilwa.

**SMS Bomba ya Leo:**
Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.

## PICHA MPYA



**TUMA MESEJI - 0773 477 311**




# Ugomvi wa wazazi unavyotesa watoto

**Na Adam Fungamwango**

WAGOMBANAPO mafahari wawili ziumiazo ni nyasi. Huu ni msemo wa Kiswahili wenye maana kuwa wanapogombana watu ambao wenye uwezo unaofanana, basi wale walio chini yao ndiyo watakaoathirika.

Mtunzi wa filamu ya 'Denti' amejaribu kuliangalia hili ndani ya jamii na kuja na kitu kama hiki kwa ajili ya kuelimisha.

Mara nyingi wanapogombana wazazi, wao hawaathiriki sana na ugomvi huo kwa sababu kila mmoja ana mtazamo wake au malengo yale, lakini watoto ambao wanawategemea baba na mama kuwa kitu kimoja, kukaa pamoja na kuwalea ndiyo wanaoteseka na athari zao huonekana mapema zaidi kuliko hata za wanaogombana wenyewe.

Waliocheza filamu hii ni Blandina Chagula aliyecheza kama mke wa Deo, Slim Omari ambaye ndiye Deo mwenyewe, Gladyness Steve aliyecheza kama Linda, Afsa Omari Thageo Alexander na wengineo.

Inaanza kwa kuonyesha kuwa Deo na mkewe wakigombana kiasi cha kupigana. Binti yao Linda anashuhudia ndondi hizo, lakini anaonekana kuumizwa mno na tabia ya wazazi wake ambao kila kukicha wao ni kubishana, ugomvi na ngumi.

Mawazo kichwani wanamfanya hadi kutofanya vema darasani. Walimu wanashangaa kwani awali alikuwa denti mwenye akili nyingi.

Linda analieleza tatizo la wazazi wake kwa rafiki yake wa jirani. Hakuna rafiki mwema, kwani anamshauri kujisahahulisha mambo hayo kwa kunywa pombe, na anasa. Anakataa kufanya hivyo. Lakini kila kukicha ni afadhali ya jana. Mwisho anaamua kuungana na rafiki yake. Linda anabadilika tabia. Anaanza kunywa pombe, kufuta sigara na kufanya ngono zembe.

Siku moja mama yake anaondoka na kurudi usiku wa manane na kuomba afunguliwe mlango. Mumewe Deo anakataa na kumwambia akalale huko huko alikotoka. Anampiga marufuku Linda kwenda kumfungulia mama yake.

Hali inazidi kumchanganya Linda, ikawa ni tabia yake akitoka shuleni anapitia kwa wanaume zake kwa ajili tu ya kuondoa msongo wa mawazo kwa sababu ya matatizo ya nyumbani kwao.

Siku moja anaamua kwenda anakokutana na rafiki zake, lakini hawakuti. Anajaribu kwenda kijiwe kingine anakutana na mvulana anayemtongoza ili kufanya naye mapenzi. Akakubali, lakini wakati wanaingia chumbani tu, anakutana na wavulana wengine wawili ambao wote wanambaka.

Hali hiyo inazidi kumchanganya Linda na anaamua kutokwenda kabisa shule. Kama kawaida wazazi wa Linda wanaanza kugombana kutokana na kubadilika kwa tabia ya binti yao kila mmoja akimtuhumu mwenzake.

Walimu wake wanaamua kumsaka kwa sababu hafiki shule na nyumbani hakai sana. Wanamfuma kwa mpenzi wake akiwa hajiwezi kwa kutumia madaya ya kulevya.

Walimu anamchukua na kumpeleka hospitalini ili apate matibabu. Wanawasiliana na wazazi wake, lakini wanapokutana hospitalini kazi ni ile ile tu, ugomvi.

Walimu wanawaamua na kuwakalisha chini wakiwaambia kuwa ili kuokoa maisha ya mtoto wao, asiendelee na tabia aliyonayo, ni wao kuyamaliza yote na kuishi kwa amani nyumbani, vinginevyo wanampoteza mtoto wao. Wakaahidi kubadilika tabia mbele ya walimu wa binti yao



# NUSURA ABAKWE

## CARD B ASIMULIA YOTE YALIYOFICHWA

RAPA mwenye utata mwingi wa Marekani, Cardi B, amefichua siri kuwa aliwahi kunyanyaswa kingono na mpiga picha wakati wa utengezaji wa video ya moja wa nyimbo zake.

Card B alitoa siri hiyo wakati akizungumza katika makala maalum ya kituo cha WETV na kutaka mashabiki wake kujadili suala hilo pamoja.

Mwanamuziki huyo ambaye ni mama na mke mara nyingi amekuwa akiwataka mashabiki wake kujadili masuala mbalimbali ikiwamo mambo yake ya uhusiano.

Katika toleo la kwanza ya makala hiyo, Card B alielezea namna alivyokumbana na vitendo vya kulazimishwa kufanya ngono na mpiga picha huyo wakati wakifanya kazi ya uchukuaji wa vipande vya video yake,

"Sitaweza kusahau jinsi nilivyokwenda kuchukua picha katika hili jarida , mpiga picha alijaribu kuwa karibu na mimi, sawa alitaka kuwa kwenye hili gazeti? Aliuliza na kisha akaendelea "Alitoa nje sehemu zake za siri, nilipatwa na kichaa .

"Nikajisemea huu ni uwendawazimu" akaongeza kueleza.

Mesema baada ya tukio hilo alikwenda kuripoti kwa mhariri wa jarida hilo naye alionekana kushangazwa.

"Nikasema Ohoo Mungu wangu ni nini? Nilichanganyikiwa," alisema na kuongeza "Unajua kuchanganyikiwa? Nilimwambia mmiliki wa jarida lazima anisimamamie upande wangu,"

Miezi michache iliyopita Cardi B alitawala katika mitandao ya kijamii baada ya kuhusishwa na kikundi cha watu wanaofanya vitendo vya kihalifu. Hata hivyo mwimbaji huyo aliomba radhi kutokana na kitendo chake hicho.

# Khafii ajipa moyo kurudi Uingereza



PAMOJA na kukabiliwa na adhabu kali kufuatia kuondoka eneo la kazi bila ruhusa, mshiriki wa Big Brother Nigeria (BBNaija), Khafii, amejipa moyo kwamba suala hilo litaisha baada ya kurudi kwenye ajira yake.

Mshiriki huyo ambaye amejipatia umaarufu baada ya jeshi la polisi la Uingereza kutangaza kumtafuta Khafii baada ya kuondoka nchini humo bila ruhusa na kwenda kushiriki shindano hilo.

Kulingana na Linda Ikeji, ofisa huyo wa polisi alisema kila kitu kitajulikana pale atakaporejea Uingereza na kukabiliana na tuhuma hizo.



## Haya ndio matumizi ya fedha bwana!

STAA wa muziki wa Nigeria, Davido na mchumba wake Chioma wamefanya kufuru baada ya kwenda madukani kununua nguo za mtoto na kutumia mamilioni ya pesa.

Chioma kwa sasa amebeba ujauzito wa msanii huyo na wiki hii aliamua kufanya manunuzi kwa ajili ya kujiandaa ujio wa mtoto huyo ambaye amebakiza miezi kadhaa kuzaliwa.

Katika ukuraza wa Instagram wa Chioma, aliweka picha mbalimbali ikimuonesha akiwa anafanya manunuzi hayo ambayo gharama zake zimewaacha midomo wazi mashabiki wao.

## Mwingine akamatwa kifo cha Mac Muller

RYAN Reavis amekuwa mtu wa pili kukamatwa kwa tuhuma ya kuhusika na kifo cha mwanamuziki wa Marekani Mac Miller.

Kulingana na mtandao wa TMZ, mwanaume huyo mwenye miaka 36 alikamatwa baada ya shirika la upelelezi la Marekani, FBI na DEA kumlenga katika kifo cha utata cha msanii huyo kilichotokea mwaka 2018.

Uchunguzi unaonesha katika chumba cha mwanamuziki huyo kulikutwa na dawa za kulevya pamoja na misokoto kadhaa ya bangi





## Adekule akamilisha Albam yake kivingine

MKALI wa muziki wa Nigeria, Adekunle Gold, wiki hii ametambulisha wimbo ambao utakuwepo katika albamu yake mpya atakayoitoa hivi karibuni.

Kulingana na ukurasa wake wa Twitter, amewaandikia mashabiki wake kuwa "tayari na projekti yangu hivi karibuni,"

Albamu yake ya mwisho ilikuwa ikifahamika kama About 30 ambayo aliitoa mwaka 2018. Wimbo wake huo mpya 'Young Love,' unaashiria ujio wa albamu hiyo upo karibuni.

## CDQ, Flavour watambulisha 'Akwaaba'

WASANII wa muziki kutoka Nigeria, CDQ na Flavour wametambulisha singo yao mpya Akwaaba itakayojumuishwa katika albam ya TBA.

Wimbo huo ambao una ladha ya Afrobeats unetayarishwa na Nastercraft chini ya lebo General Records.

Wimbo huo unafuatia baada ya 'Onye Eze 3.0 Cypher' ambao CDQ aliutambulisha wiki chache zilizopita.





Na John Juma
0716217615

MIONZI YA SHERIA

# Haki yako ipo hata ukitimuliwa

KISHERIA kuna sababu nyingi ambazo zinachangia mwajiriwa kufukuzwa kazi au mkataba wa ajira yake kubatilishwa. Ubatilishaji wa mkataba wa ajira unafanyika baina ya mwajiri na mwajiriwa. Msingi wa mambo hayo umejengwa katika sura ya 366 ya Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya mwaka 2004.

Mkataba wa ajira, kama ilivyo mingine kwa mujibu wa sheria, inazaliwa siku unaposainiwa, inaishi pale unapotumika lakini kama kiumbe hufa. Ndivyo ilivyo kwa binadamu na viumbe hai vingine vyote.

Mkataba kuzaliwa kama tulivyosema ni mara baada ya mwajiriwa na mwajiri kuweka saini zao hapo ndipo wanapouanzisha punde utekelezaji unapoanza kuchukua hatua na kifo ni pale tu yanapoanza kujitokeza baadhi ya mambo au masuala yanayoainishwa na sheria kwa lengo la kuubatilisha. Aidha zipo, taratibu maalum za kumaliza au kuua mkataba wa ajira na hii ni katika mazingira yote, iwe kwa hiari na yale ya kumaliza kwa kulazimika kulingana na sababu mbalimbali.

Kumalizika au kukoma mkataba wa ajira kwa hiari au kufikia ukomo wa kazi kulingana na wepesi wa kutekeleza majukumu ya kazi yenyewe .

Kanuni ya 4 (1)-(7) na ya 5 (1)-(5), zote za Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Kanuni za Utendaji Bora za mwaka 2007 zinaeleza kuwa hakuna shida kama ilivyo kumaliza kukoma mkataba wa ajira kwa kulazimika kutokana na sababu mbalimbali za kinidhamu.

Katika mahusiano kazini jambo mojawapo linalomfukuza mtu kazi au kusababisha kukoma mkataba wa ajira ni utovu wa nidhamu, hii ni moja kati ya sababu za msingi zinazoweza kumpelekea mwajiriwa au mfanyakazi kupoteza ajira yake.

Kimsingi, kanuni hizo zinaelekeza kuwa ni sahihi kumfukuza mfanyakazi kwa sababu za kinidhamu lakini haimaanishi kuwa mwajiri amtafutie mwajiriwa kisa cha kuzusha au kupika ili kumuondoa kazini.

Kinachosisitizwa hapa, ni lazima sababu hizo ziwe zimejitokeza na kuthibitika kweli na ziweze kuthibitishwa pale itakapotakiwa kufanyika hivyo.

Ujenzi wa hoja kwa kushikilia mkazo kuwa nilisikia au nahisi, zitasababisha tuhuma hizo kukosa mashiko mbele ya msuluhishi, hakimu au jaji kutegemeana na shauri hilo lilipofika.

Kanuni ya 8 (1)(d) na 12 (1)-(5), zote za Ajira na Mahusiano Kazini na Kanuni za Utendaji Bora za mwaka 2007, sanjari na kifungu cha 37 (2), Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, 2004 Sura ya 366 zote zinasisitiza ukweli na uthibitisho wa madai yanayotolewa.

**ANGALIZO**

Sheria inaelekeza kuwa mwajiriwa au mfanyakazi kufukuzwa kazi mara moja, bila ya hata kupatiwa barua ya onyo kwa kosa la mara ya kwanza au "summary dismissal".

Kwa utaratibu huu hupelekea mwajiriwa, au mfanyakazi kupoteza haki zake za msingi kama kiinua mgongo. Kifungu cha 42 (1)-(4) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya mwaka 2004 Sura ya 366 inaeleza.

Hivyo basi, ni kosa kwa mwajiri kumfukuza mfanyakazi utaratibu wa mara moja, yaani "summary dismissal". Labda ifanyike hivyo katika mazingira ambayo sheria inaruhusu waziwazi kufanya hivyo. Na siyo kinyume chake. Kifungu cha 41 (1)-(7) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya 2004 sura ya 366 inaeleza.

**HAKI YA KUSIKILIZWA**

Kila mtu ana haki ya kusikilizwa kabla ya hatua kuchukuliwa ni haki ya asili ambayo haiwezi kuondolewa na mtu au mamlaka yoyote ile. Kwa maana hiyo hata kosa la mwajiriwa liwe la ukubwa wa kiwango gani ni lazima mhusika apatiwe nafasi ya kutoa utetezi wake.

Atajitetea na kutakiwa kuwasilisha utetezi wake kwanini asichukuliwe hatua za kinidhamu. Kanuni ya13 (1)-(13) Kanuni za Ajira na Mahusiano Kazini, 2007 inaeleza.

Ni kosa kwa mwajiri au mkuu wa kazi kumfukuza mfanyakazi bila ya kwanza kumpatia nafasi ya kumsikiliza au kujitetea. Hii siyo hiari ya mwajiri kuamua kumpatia mwajiriwa haki husika. Hii ni kwa sababu haki yenyewe ipo kwa mujibu wa sheria, hivyo utekelezaji wake ni lazima.

**HAKI YA MALIPO, STAHIKI**

Kifungu cha 44 (1)(a) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya mwaka 2004 sura ya 366 kinaelekeza miongoni kati ya haki za msingi alizonazo mwajiriwa ambaye atafukuzwa kazi kutokana na sababu za kinidhamu ni pamoja na kulipwa mshahara au ujira wake.

Mshahara utalipwa kwa kuzingatia tarehe ya mshahara wa mwisho mpaka siku ambayo mwajiriwa amefukuzwa, kama tarehe ya mwisho ya kupokea mshahara itakuwa Juni 30, 2019 Kisha mhusika atafukuzwa Julai 17, 2019; pesa itakayotolewa ni kwa kuzingatia siku ambazo mhusika amefanyakazi. Yaani jumla ya siku 17 kuanzia Julai mosi hadi 17. Yenyewe ni haki ya msingi, wala isipuuzwe ili kulinda maslahi ya pande zote mbili.



Na Reubeni
Lumbagala

KALAMU YA MWALIMU

# Mchango wa wadau umsaidie binti kielimu

MOJA ya wadau muhimu katika elimu ni taasisi ya HakiElimu ambayo inashirikiana kwa karibu na serikali katika kuchagiza maendeleo ya sekta ya elimu kwa maendeleo endelevu.

Hivi karibuni, shirika hilo la kiraia lilifanya utafiti na kuzindua ripoti kuhusu "Changamoto za Elimu ya Mtoto wa Kike".

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dk. Leornard Akwilapo, katika uzinduzi wa utafiti huo anaahidi kushirikiana na wadau wote katika kuzitafutia ufumbuzi changamoto za mtoto wa kike na kuleta ustawi bora wa maisha yao.

Dokta Akwilapo anasema "ripoti ya utafiti ninayoizindua leo ni mfano hai wa kile ninachokisema kuhusu mchango wa sekta binafsi kwani inahusu changamoto zinazosababisha wasichana kushindwa kuendelea na masomo na kuvuka kuingia hatua nyingine."

Anasema utafiti huo unaendana na lengo la serikali la kuhakikisha kuwa wasichana wanaoandikishwa katika Elimumsingi wanamaliza safari yao ya elimu kwa mafanikio makubwa.

Mtoto wa kike kama kundi maalum katika jamii, anastahili kuendelezwa hivyo upo umuhimu wa serikali kwa kushirikiana na wadau wengine wa elimu kuzitafutia ufumbuzi wa kudumu changamoto za elimu ya mabinti ili wapate elimu katika mazingira bora ili kufikia matarajio ya kielimu.

Ni lazima utafiti wa kina ufanyike ili kuzitambua na kuzipatia ufumbuzi changamoto za elimu ya mtoto wa kike zilizopo katika mazingira maeneo mbalimbali ya nchi yetu na kutoa mapendekezo ya namna ya kukabiliana nazo

Taasisi ya HakiElimu inatekeleza mpango mkakati wake wa mwaka 2017-2021 ambapo pamoja na mambo mengine, unaihusisha serikali pamoja na wadau wengine kuhakikisha watoto wa Tanzania wakiwamo watoto wa kike wanapata elimu bora bila vikwazo.

Serikali kama mdau nambari moja katika kuzitafutia ufumbuzi changamoto za elimu ya mabinti imeonyesha njia kwa kuwachukulia hatua za kisheria wote wanaoshiriki vitendo vya kukatisha ndoto za kielimu za mtoto wa kike.

Mathalani, kuwapeleka mahakamani wanaume wanaowapa mimba wanafunzi waliopo shuleni. Yeyote anayeshiriki vitendo vya kimapenzi na wanafunzi adhabu yake ni kifungo cha mika 30 jela. Hili limesimamiwa kikamilifu ili kutoa fundisho kwa wale wanaoendekeza udhalilishaji huo.

Aidha, serikali pia imekuwa ikitoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari kuhusiana na umuhimu wa kuwapa nafasi watoto wa kike kupata elimu kwani wao wana haki sawa kama ilivyo kwa watoto wa kiume katika kupata haki ya elimu.

Hii ni kutokana na uwepo wa mila na desturi potofu kwa baadhi ya makabila kuwanyima watoto wa kike haki ya kupata elimu na kuishia kuolewa katika umri mdogo.

Vilevile, serikali imepambana katika vita ya unyanyasaji wa kijinsia ambao pia ni changamoto kwa elimu ya mtoto wa kike.

Vita hii ni endelevu, inahitaji ushirikiano na sauti ya pamoja kuanzia ngazi ya familia, jamii hadi taifa katika kuhakikisha wale wote wanaofanya vitendo vya ubaguzi wa kijinsia wanachukuliwa hatua za kisheria kwa maslahi na ustawi wa mtoto wa kike

Sambamba na hili, serikali kwa mwaka wa nne sasa inatekeleza Sera ya Elimumsingi Bila Malipo ambapo takribani bilioni 23 zinatumika kila mwezi katika utekelezaji wa sera hii nchi nzima.

Kupitia utekelezaji wa sera hii, watoto wa taifa hili wakiwamo wasichana wanapata haki ya elimu kwa kugharamiwa na serikali na hivyo wazazi kubaki na mzigo mdogo wa kuwapatia watoto wao mahitaji ya shule.

Wasichana wa shule za msingi na sekondari wamenufaika sana na Sera ya Elimumsingi Bila Malipo kwani baadhi ya wazazi na walezi walikuwa wakijitetea kushindwa kuwasomesha watoto wao kutokana na gharama kubwa za elimu kabla ya kuanza kwa sera hii. Hivyo, sera hii imeondoa kiambaza kilichokuwa kikiwazuia watoto wa kike kupata elimu bora, kwani sasa wanapata elimu bora bila malipo.

Mkurugenzi Mtendaji wa HakiElimu, Dk. John Kalaghe, katika uzinduzi huo anasema "HakiElimu tunatilia mkazo katika kuhamasisha utoaji wa elimu jumuishi yenye ubora na usawa pamoja na elimu kwa watoto wa kike ikiwa ni pamoja na kupunguza na kuondoa unyanyasaji wa watoto shuleni na nje ya mipaka ya shule".

Ripoti hii ya HakiElimu iwe chachu kwa taasisi nyingine katika kufanya utafiti wa changamoto za elimu za mtoto wa kike na kutoa mapendekezo ya namna ya kuondokana na changamoto hizo ili kufikia maendeleo ya haraka kupitia mchango wa mtoto wa kike. Tafakari.

Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.

## WACHEKELEA UFUTA

# Wavuna mara dufu mwaka huu, sasa ni kuzipiku wilaya zote jirani

**Na Sabato Kasika**

WILAYA ya Nachingwea mkoani Lindi, imekusanya na kuuza kilo milioni 8.4 za ufuta katika msimu wa mwaka huu wa kilimo uliomalizika hivi karibuni, kwa kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani.

Mbali na kuuza kiasi hicho cha ufuta, wakulima wamelipwa zaidi ya Sh.bilioni 23, huku halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea ikikusanya fedha za ushuru wa Sh. milioni 698.3.

Bei ya kilo moja ya ufuta iliuzwa kati ya Sh. 2,580 hadi 2,860, kwa kutumia mfumo huo ambao Mkuu wa Wilaya hiyo, Rukia Muwango, anasema amewezesha wakulima kunufaika na kilimo cha zao hilo.

"Yaani msimu huu mkulima alikuwa anaingiziwa fedha kwenye akaunti yake ndani ya siku saba tangu kuuza ufuta kwenye vyama vya ushirika vya msingi, hali ambayo wakulima wengi wameifurahia," anasema Muwango.

Kiasi hicho cha ufuta kilichokusanywa na kuuzwa, malipo ya wakulima na ushuru wa halmashauri kwa mwaka huu, vimekuwa ni mara mbili zaidi ya msimu uliopita wa mwaka jana.

Kwa mujibu wa mkuu huyo wa wilaya, msimu wa mwaka jana, Nachingwea ilikusanya kilo milioni 4.1, na wakulima wakilipwa zaidi ya Sh. bilioni 12. 5, huku ushuru ukiwa ni zaidi ya Sh. milioni 576.7.

"Bei ya kilo moja ya ufuta kwa msimu wa mwaka jana ilikuwa ni kati Sh. 1,651 hadi Sh.1,764, hali ambayo kwa kiasi fulani ni kama wakulima walitaka kukata tamaa, lakini safari hii mambo yamebadilika," anasema.

Muwango anaamini kwamba kilichotokea msimu wa mwaka huu kitawafanya wakulima wengi zaidi kujitokeza kulima ufuta, hasa baada ya kulipwa kwa wakati na tena kwa bei nzuri kuliko ya msimu uliopita.

**KUTUMIA USHIRIKA**

Anasema ufuta uliingizwa kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani tangu mwaka jana na kwamba sasa ni msimu wa pili wilaya ikiendelea kuuza zao hilo kwa mfumo huo uliosaidia wakulima wasinyonywe.

"Mfumo huu ni mzuri, kwani wafanyabiashara wananunua kwenye mnada unaoendeshwa na vyama vya ushirika, tena kwa kushindana na kusababisha bei kupanda kila mwaka na hivyo kuwanufaisha wakulima," anasema.

DC Muwango anasema, miaka ya nyuma wafanyabiashara walikuwa wakienda kwa wakulima na kununua ufuta kwa bei ndogo hali, ambayo ilisababisha wakulima wasinufaike na jasho lao.

"Lakini sasa tumefanikiwa kuwadhibiti hao akina chomachoma na kangomba, ndio maana minada imekwenda vizuri huku wakulima wakinufaika na mfumo wa stakabadhi ghalani," anasema.



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Rukia Muwango, alipozindua msimu wa ufuta wilayani mwake mwaka huu.

Anasema, udhibiti huo ni mkakati wa mkoa ulioshushwa kwa wakuu wa wilaya na kushirikisha maofisa ushirika na viongozi wa vyama kwa kuratibiwa na mrajisi msaidizi wa mkoa, Robert Msunza.

Muwango anasema, kwa sasa Nachingwea hakuna wafanyabiashara wanaofuata wakulima shambani kwa lengo la kuuziwa ufuta badala yake wanakwenda katika vyama vya ushirika kushindana kwenye mnada.

"Elimu imeshatolewa ya kutosha kuhusu madhara ya kangoma na chomachoma na pia wakulima wanajua faida ya mfumo wa stakabadhi ghalani, ambao unakubalika kisheria," anasema.

**CHANGAMOTO**

Pamoja na kuuza ufuta mwingi kuliko wa msimu uliopita, Muwango anasema kulikuwa na changamoto kadhaa zilizojitokeza, ambazo hata hivyo hazikuathiri minada na mauzo ya zao hilo.

"Kulikuwa na changamoto ya awali, ambayo ni vifungashio, yaani viroba maalum vya kilo 50, vilichelewa kuletwa na kusababisha wakulima kila mmoja kuweka katika kifungashio chake," anasema.

Anasema uhaba huo wa vifungashio ulisababishwa na makisio madogo, takwimu hazikuwa sahihi toka kwa wataalam, walisikia makusanyo ya kiasi pungufu tofauti na kile ambacho walima walizalisha msimu huu.

"Hata hivyo, Chama Kikuu cha Ushirika cha Runali kilifanya utaratibu vifungashio vikapatikana vya kutosha na hivyo wakulima kuondokana na changamoto hiyo," anasema.Anasema, ana imani mwaka kesho changamoto zote zilizojitokeza zikiwamo ambazo hakuzitaja, hazitajitokeza tea msimu ujao, kwa madai kwamba watakuwa wamejipanga vizuri kuhudumia wakulima.

**MIKAKATI**

Muwango anasema wilaya yake ni mwisho kwa kilimo cha ufuta, mkoani Lindi, lakini sasa inajipanga kwa kushirikiana na viongozi wenzake ili kuhakikisha inakuwa juu katika uzalishaji wa zao.

"Kilwa inaongoza katika kilimo cha ufuta ikifuatiwa na Ruangwa na kisha Liwale, huku Nachingwea tukijikongoja, lakini kwa hali ilivyo sasa, nina uhakika Nachingwea itakuwa juu katika kilimo cha zao hili," anasema.

Mkuu huyo wa wilaya anasema, anaamini hilo, kwa vile wilaya hiyo kwa sasa inapokea wageni wengi wanaofika kwenye ofisi za serikali za vijijini na kuomba maeneo kwa ajili ya kulima ufuta.

"Ujio wa wageni hao ni dalili tosha kuwa si miaka michache ujayo Nachingwea itakuwa juu kwenye kilimo cha zao na ikibidi tutazipuku wilaya nyingine za Mkoa wa Lindi zinazoongoza," anasema.

Anasema kuongezeka kwa idadi ya wakulima ni ishara kwamba hata uzalishaji wa ufuta utaongezeka zaidi katika msimu wa mwaka ujao, na anawataka wakulima waendelee kuandaa mashamba yao.

Anasema wageni wengi wanatoka wilaya za Mtwara, ambako ufuta haustawi kwa wingi, na kwa kuwa sote ni Watanzania, basi hatuna budi kuwakaribisha ili mradi hawavunji sheria," anasema.

**WAKULIMA**

Simon Milanzi ni mmoja wa wakulima wilayani Nachingwea ambaye anasema msimu huu alilima ufuta kiasi kidogo tu kwa ajili ya matumizi yake ya nyumbani baada ya kuchoshwa na bei ya mwaka jana.

Lakini ameshangaa kuona msimu huu hali imebadilika, wakulima wa ufuta wakifaidika, na sasa anasema anajipanga ili kuhakikisha anaandaa mashamba ya kutosha kwa ajili ya kulima ufuta mwingi na kuuza mwaka ujao.

"Mfumo wa stakabadhi ghalani kwenye ufuta umesimama vizuri, hivyo ninajiandaa kuandaa mashamba ya kutosha ili kuhakikisha ninalima ufuta wa mwingi kwa ajili ya kuuza msimu ujao," anasema

Kwa upande wake Fikira Ponera anasema alilima ekari tatu za ufuta, lakini changamoto ya hali ya hewa ikasababisha apate mavuno kidogo, hata hivyo anafafanua kuwa hawezi kukata tamaa.

"Hakuna jambo unaloweza kufanya kwa mteremko tu, hivyo siwezi kukata tamaa na badala yake nitaendelea kulima ufuta, kwani ndilo zao lenye tija na linaloweza kuinua maisha yangu," anasema Ponera.



Viroba vyenye ufuta vikiwa vimeandaliwa kwa ajili ya kupimwa kwenye mizani. **PICHA: MAKTABA.**

**MAKALA**

## UCHAGUZI 2020

# Ni zamu ya wanaume kuwasimamia wanawake, lengo ni tarakimu 50/50

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NIUKUMBUSHE msemo wa wahenga wa `nguo ya Ijumaa hufuliwa Alhamis,' walimaanisha kwa lolote maandalizi ya mapema ni muhimu.

Kwa kuliona hilo Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (Tamwa) Zanzibar, wakishirikiana na Shirika la Kuwawezesha Wanawake la UN Women, kimeanza mandaalizi ya kuihamasisha jamii kuwapa nafasi ya uongozi wanawake katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Kutokana na ushiriki mdogo wa wanawake katika vyombo vya kutunga sheria kama Bunge na Baraza la Wawakilishi, Tamwa imenza kuwaandaa mapema ili ifikapo 2020 wanawake wengi wagombee nafasi hizo.

**MIKAKATI**

Miongoni mwa mikakati inayofanyika ni kuunda timu ya wanaume wa mabadiliko ambao wanaelimisha jamii kuhusu nafasi na umuhimu wa uongozi kwa wanawake.

Asha Abdi, Kaimu Mkurugenzi wa Tamwa Zanzibar, anasema timu ya wanaume wa mabadiliko wanapita katika shehia mbalimbali Unguja na Pemba kutoa elimu kuhusu nafasi ya uongozi kwa wanawake.

Anasema, elimu hiyo wanayoitoa si kufanya kampeni ya kuwapata wanawake ambao watagombea katika uchaguzi mkuu sivyo kwani wakati wa kampeni haujafika, ila kinachofanyika ni kuihamasisha jamii iukubali uongozi wao.

Anaeleza kuwa wanafanya maandalizi ya mapema ili kuondoa mitazamo hasi kwamba wanawake hawawezi kuwa viongozi au wabunge majimboni.

Asha anaeleza zaidi kuwa jamii imetawaliwa na mfumo dume unaopelekea ushiriki mdogo wa wanawake katika ngazi za maamuzi iwe bungeni au barazani.

"Tunataka tuone wanawake wengi wakijitokeza kugombea nafasi za uongozi majimboni badala ya kuwaachia wanaume pekee,"anasema.

Anasema wanaamini elimu hiyo itaondosha mitazamo hasi kwa jamii dhidi ya wanawake na kuwapa nafasi ya kuwa wawakilishi na wabunge majimboni.

**KUTOKA BARAZANI**

Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma, anawataka wanawake kujitokeza kuwania nafasi za uongozi katika majimbo ya uchaguzi na kuacha tabia ya kuwapigia kampeni wanaume kwa ajili ya kuchukua nafasi hizo.

Anakumbusha kuwa ushiriki wa wanawake katika uongozi vikiwamo vyombo vya kutunga sheria ni mdogo, mathalani, katika majimbo ya uchaguzi.

Anasema katika majimbo ya uchaguzi 54 ya Zanzibar ni wanawake watano waliogombea nafasi ya uwakilishi katika wakati wa uchaguzi Zanzibar ambapo wanawake hao hivi sasa ni wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Aidha nafasi ya ubunge, anaeleza kuwa ni wanawake watatu ndiyo walioshinda na kuongoza majimbo ya uchaguzi kwa upande wa Zanzibar.

"Bado uwakilishi wa wanawake katika kugombea nafasi za uongozi ni mdogo ambapo nafasi zote tumekuwa tukiwaachia wanaume',’anasema Naibu Spika.

Anaeleza kuwa licha ya uwakilishi mdogo wa wanawake katika baraza hilo la wawakilishi, wameonyesha mafanikio makubwa katika kujenga hoja zinazotokana na matakwa ya wananchi katika majimbo ya uchaguzi.

"Tunazo kamati tatu za Baraza la Wawakilishi zinazoongozwa na wanawake ambapo wameonyesha uwezo na ujasiri mkubwa katika kufuatilia mambo mbali mbali na mengi katika wizara na taasisi zake',’anasema Mgeni.

**DINI SI KIKWAZO**

Profesa wa Chuo kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) Professa Issa Haji Ziddy, anawataka wanawake kuwa mstari wa mbele kugombea nafasi za uongozi na hakuna vikwazo kwenye Uislamu cha kuwazuia.

Anasema hata katika maandiko matakatifu kuna mitume wanawake watano mashujaa ambao wametajwa kuwa walifanya kazi kubwa ya kuupigania Uislamu.

Anamtaja aliyekuwa mke wa kwanza wa Mtume Muhammad kuwa alikuwa mshauri wake mkuu na ndiye miongoni mwa watu wa mwanzo kumuunga mkono mtume na kutambua kuwa ni kiongozi wa Mungu.

Aliwataka baadhi ya watu kuacha kuzitumia vibaya aya za Kuran kwa kuzitafsiri kwa malengo na madhumuni yao binafsi.

"Ipo suratul Nisaa aya ya (34) ambayo inatafsiriwa wanaume ni viongozi wa wanawake wakati tafsiri sahihi ni "wanaume ni wasimamizi wa wanawake"anasema Profesa Ziddy.

**WANAUME MABADILIKO**

Mmoja ya viongozi wa timu ya wanaume mabadiliko katika jamii, Suleiman Zimba Khatib, kutoka Kijiji cha Makunduchi, anasema zama zimebadilika na sasa wanawake wameonyesha uwezo mkubwa katika kuongoza.

Anasema hivi sasa nafasi ya pili ya uongozi wa nchi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inashikiliwa na Samia Suluhu Hassan, ambaye ameonyesha mafanikio makubwa na utendaji kazi uliotukuka.

Simba aliwataka wanaume wengine kubadilika na kuachana na tabia za wivu kwa wake zao wakati wanapotaka kuwania nafasi za uongozi ikiwamo ubunge na uwakilishi.

**TISHIO LA TALAKA**

Baadhi ya wanaume ni kikwazo kwa wake zao kuwania nafasi za uongozi na kwamba wapo wanaowatishia kuwapa talaka kama wataonyesha nia ya kujiingiza katika siasa.

"Nilionyesha nia ya kutaka kuwania udiwani lakini mume wangu alinipa vitisho na kuniambia nikijikita katika siasa hiyo ndiyo talaka yangu"anasema Mwatima Vuai mkaazi wa Makunduchi Mkoa wa Kuisni Unguja.

Hali hiyo ya wanawake kupewa vitisho na wanaume pale wanapotaka kuwania nafasi za uongozi, haipo kwa Mwatima pekee bali kadhia hiyo huwakumba wengi visiwani Zanzibar.

Mwatima anaeleza kuwa baadhi ya wanaume wamekua na hofu ya kwamba wanawake wanapokuwa viongozi uchumi wao huimarika na baadhi yao wanadhana kuwa wanawake wapokua viongozi wanaume watadhaurika jambo ambalo sio sahihi.

Aidha, anasema kuwa mwanamke anapokuwa kiongozi hujitahidi kutatua changamoto zinazowakabili wananchi kwani wengi wao wanakua changamoto hizo wameshazipitia.

Mwakilishi wa jimbo la Bumbwini (CCM) Mtumwa Peya Yussuf, aliwataka wanawake wenzake kujenga ujasiri na kuacha kuamini kwamba nafasi za uongozi zimetengwa kwa ajili ya wanaume.

Anasema alipotangaza nia na kuchukuwa fomu kuwania uwakilishi katika jimbo la Bumbwini wapo waliomkejeli na wapo waliomtia moyo na kumwambia anaweza kuwaongoza.

"Nilichukua fomu na kuwania jimbo la Bumbwini na kushinda.....zipo changamoto na vikwazo kwa mwanamke kuwania nafasi za uongozi lakini kamwe tusikate tamaa,"anasema Peya.

**WITO WA UWT**

Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake (UWT) Zanzibar, Tunu Kondo, anasema hakuna vikwazo kwa wanawake kujitokeza kuwania nafasi ya uongozi ikiwamo ubunge na uwakilishi majimboni.

Kondo anasema anashangaa kuona wanawake ni wengi zaidi ya asilimia 51 lakini hadi sasa idadi yao ni ndogo katika vyombo vya kutunga sheria na kufanya maamuzi.



Bahati Chum Haji, mkazi wa shehia ya Magomeni Mjini Unguja akizungumza katika mkutano wa utoaji elimu kwa wananchi kuhusu nafasi za uongozi kwa wanawake ulioandaliwa na TAMWA. **PICHA: RAHMA SULEIMAN.**

## CHEMSHABONGO NA NIPASHE NAMBA (00 13 00)




Dondoo: Kulia
1. Jambazi aliyeachiwa huru badala ya Yesu Kristo
6. Kisiwa kikubwa Afrika
9. Shuhudia kwa macho
10.Dakika 60
11.Kipindi cha jua kali
15. Kua kwa mmea
16.Mapango yaliyoko Tanga
20.Pembe ndogo ya kifaru
21.Kigali ni mji wake mkuu
22.Mmea uzalishao mbao
23.Endapo 24.Paris mji mkuu
26. Ongezeka kimo 27.mahali pa kunywa pombe
28.mwanamke aliyepelekewa posa na ikakubaliwa na wazazi

Dondoo: Chini
1. Mji mkuu wa Mali
2. Hiari ya kufanya jambo
3. Mume
4. Hongo
5. Tunda lenye miba miba
7. Kipande cha mti uliokatwa
8. Bakisha
12.ushahidi
13.Kuwa madhubuti
14. Mji mkuu wa Somalia
17. Kufifia rangi
18. Kutembea kwa kuburuza tumbo
19. Sherehe
25. Osha nguo

### Jibu Na: 12

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| G | R | E | E | N | L | A | N | D | | M | | |
| E | | | P | | | | A | | A | D | H | A |
| R | I | Y | A | D | H | | Z | | T | A | A | |
| E | | U | | H | A | D | I | T | H | I | W | A |
| Z | A | G | R | E | B | | | | E | | A | |
| A | | A | | H | A | L | A | | N | | J | |
| | | Y | | E | R | O | P | L | E | N | I | |
| C | H | U | M | B | I | W | A | | | | | |
| H | | G | | U | | A | R | U | D | H | I | |
| O | M | A | N | | | | E | | I | | L | |
| M | | | E | T | I | | J | A | M | B | I | A |
| B | E | M | B | A | | | O | | B | | K | |
| O | | | O | I | L | I | | P | A | Z | I | A |

# Wajasiriamali wanavyounda, kutengeneza soko la bidhaa



Wajasiriamali wa kundi la Kimbilioletu Inn Pair International, wakizungumza katika mikutano yao jijini Dar es Salaam. **PICHA: MASHAKA MGETA.**

**Na Mashaka Mgeta**

ZIPO falsafa nyingi zinazozungumzia shughuli za biashara, ikiwamo ile ya Chuo Kikuu cha South Dakota kilichopo Marekani ya Kaskazini, inayoeleza kuwa ujasiriamali unahusisha kuzalisha fursa, kupanga na kuanzisha miradi mipya inayokua na kuwa endelevu.

Hatua hiyo haitofautiani na mkakati wa mtandao wa wajasiriamali unaoratibiwa na Kimbilioletu Inn Pair International na kuwajumuisha washirika kutoka sekta tofauti za uzalishaji bidhaa.

Wajasiriamali wamebuni kuwapo mtandao unaolenga kwanza, kubadilishana uelewa na uzoefu wa biashara, lakini pia kutengeneza fursa za soko kwa ajili ya bidhaa zao.

Charles Wilbad ni Meneja Sera na Mipango wa Kimbioletu, anasema hatua ya kuuziana bidhaa kati ya wajasiriamali waliopo kwenye mtandao huo, ni sehemu ya utekelezaji wa mpango bunifu wa kutengeneza masoko ya ndani, kisha kuunganisha nguvu za pamoja kuyafikia masoko ya kikanda na kimataifa.

Wilbad anasema kwa kuanzia, mtandao huo umeanza kuwakutanisha washirika wake wanaozalisha bidhaa mbalimbali vikiwamo vyakula na kuuziana.

"Tumeona tuanze na kujenga utamaduni wa kutathimini, kuuza na kununua bidhaa tunazozizalisha wenyewe, ndio maana leo (wiki iliyopita) tulianza na watengenezaji vyakula na vinywaji," anasema.

Kwa mujibu wa Wilbad, bidhaa za vyakula na vinywaji zilipowasilishwa kwa wanamtandao, walivitumia papo kwa hapo na kushirikishana upungufu uliobainika, kisha kushauri namna bora zaidi ya kuboresha.

"Mpango huu tunautekeleza kama jukwaa la kuelimishana, kufundishana na kukosoana ili kuwezesha bidhaa tunazozizalishaziwe na ubora zaidi wa kumudu ushindi kwenye soko," anasema.

Katika hatua za awali za kushirikishana umuhimu wa mfumo na utamaduni wa kuuza na kununua bidhaa kupitia wanachama wa mtandao, wajasiriamali wanaotengeneza batiki, vyakula na vinywaji vikiwamo vitafunwa, uyoga, usindikaji wa samaki, juisi na vingine vinavyotokana na mazao ya nafaka, walikuwa walengwa katika uuzaji kwenye mkutano uliofanyika jijini Dar es Salaam.

"Tunapoyafanya haya, lengo letu ni kupandikiza mbegu ya kutambua na kulithamini soko la pamoja, namna linavyoweza kutumika kwa biashara na shughuli nyingine za uchumi, tukianzia na ngazi za chini kwenye jamii," anasema Wilbad.

Hamisa Daduka ni mjasiriamali mdogo kutoka Mango, Manispaa ya Temeke jijini Dar es Salaam, anayejishughulisha na utengenezaji wa juisi, akijiunga kwenye mtandao huo ili pamoja na mambo mengine, kupata fursa pana zitakazomwezesha kukuza biashara zake.

Anasema juisi anayoitengeneza ilikuwa miongoni mwa bidhaa zilizowekwa kwenye orodha ya mauzo na kujadiliwa na wateja, hivyo kumfanya anufaike kwa kiasi kikubwa katika kuiboresha.

"Watu wamekunywa juisi yangu, wameifurahia pia wamenielekeza jinsi ya kuboresha zaidi ili kulihimili soko la ushindani, ninafurahi kuwa sehemu ya mtandao huu," anasema Hamisa.

Mjasiriamali huyu anasema miongoni mwa mapendekezo aliyopewa ni namna ya kuweka kiwango sahihi cha sukari kulingana na aina ya matunda anayoyatumia kutengeneza bidhaa hiyo.

Anaeleza kuwa alianza kujihusisha na biashara ya kutengeneza na kufungasha karanga kabla ya kuongeza uzalishaji wa juisi huku akitegemea soko lake la ndani ambalo ni wateja wa Temeke hususani maeneo ya Mango.

Anasema miongoni mwa mambo aliyojifunza baada ya kushiriki kwenye mtandao huo ni utambuzi wa matumizi ya nembo ya biashara inayopaswa kusajiliwa kwenye orodha ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (Brela).

Kwa upande wake, mjasiriamali anayezalisha uyoga kupitia kikundi cha Patano chenye 'kuendesha' mradi wa Green Pastures, Henry Mwazanduru, anasema mfumo wa kuwagawa wanachama wa mtandao huo kwenye makundi mahususi, unatoa mwanya zaidi wa kujuana, kubadilishana ujuzi na uzoefu na kutanua wigo wa kushirikiana kibiashara.

"Mie nilipojiunga hapa nilikuwa mzalishaji pekee wa uyoga, lakini sasa tumekutana na wazalishaji wengine na wenye uzoefu mkubwa kuliko sisi, hivyo inatupa fursa ya kujifunza mambo mengine zaidi," anasema.

Kwa mujibu wa mfumo uliowekwa na waratibu wa mtandao huo, wanachama wake wamegawanywa kwenye makundi mahusus kwa kutegemea aina ya bidhaa wanazozizalisha.

Makundi hayo, pamoja na mambo mengine, yanawajumuisha watengenezaji wa bidhaa za viwandani kama batiki na viatu, wazalishaji wa uyoga, ufugaji, wapishi wa vyakula na wasindikaji wa vinywaji.

Lakini masuala la kujumuika pamoja, uzalishaji, usambazaji na masoko yanategemea mitaji iliyo mzizi wa ubunifu, uanzishaji na uendelezaji wa biashara.

Wilbad anasema ni kutokana na ukweli huo, mkutano wa wiki iliyopita ulihusisha mafunzo ya namna ya kupata mikopo na umuhimu wake kwa biashara na uchumi wa nchi.

"Tulipozungumzia mikopo kwa mafunzo yaliyotolewa na wataalamu wa taasisi za fedha, wanachama wetu walielimishwa pia kutambua na kulipa kodi, ili shughuli zao zichangie kasi ya ukuaji wa uchumi.

Mchungaji Amos Mushendwa ni mhamasishaji wa ulipaji kodi aliyeshiriki na kutoa mafunzo hayo, anasema kila jambo linalohusu shughuli za biashara na uchumi, linapata nguvu ikiwa wahusika wataunganisha nguvu zao.

Anasema ni kwa mtazamo huo, shughuli za kiuchumi zinazolenga kuboresha maisha na ustawi wa watu ni muhimu zikahusisha ulipaji kodi ili kuiwezesha serikali kutekeleza majukumu yake yakiwemo yale yanayolenga kuboresha maisha ya wananchi.

Hata hivyo, Mchungaji Mushendwa anayehudumu katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), anasema ushiriki mdogo wa watu hasa wajasiriamali wadogo kulipa kodi, kunachangiwa na uelewa finyu wa manufaa yanayotokana na kodi.

Mtaalamu wa masuala ya uchumi, Dk Bravious Kahyoza amewahi kukaririwa akisema, upatikanaji wa soko la bidhaa kuanzia ngazi ya chini kwenye jamii, ni nyenzo muhimu inayosaidia kukuza biashara.

Hata hivyo, Dk Kahyoza ambaye pia ni Mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, anasema ili kufikia malengo ya uboreshaji biashara na shughuli za uchumi za wajasiriamali wadogo hasa wanawake na vijana, ipo haja ya kuzifanya sera na mikakati inayowalenga, kuwa rafiki na yenye kujenga mazingira ya kuwawezesha kuzifikia huduma kama mikopo.

Mawasiliano: 0754691540

## HABARI KIMATAIFA

# Mugabe kuzikwa nyumbani kwao

**HARARE, Zimbabwe**

MWILI wa Rais wa kwanza wa Zimbabwe, Robert Mugabe, utazikwa nyumbani kwao, baada ya serikali kubadili msimamo wake wa awali kuhusu mazishi yake.

Mugabe alifariki mapema mwezi huu akiwa na miaka 95 na ibada ya mazishi kufanyika katika mji mkuu wa Harare.

Serikali ilikuwa imepinga ombi la familia yake la kumzika kiongozi huyo katika eneo la Zvimba, na kushinikiza azikwe katika makaburi ya mashujaa wa kitaifa.

Familia yake hatimaye ilikubali lakini serikali ikabadilisha msimamo huo Alhamisi wiki hii.

Haikufahamika ni nini kilichosababisha mipango ya awali ya mazishi ya Mugabe kubadilishwa.

Familia ya Mugabe ilikubali azikwe katika makaburi ya mashujaa jijini Harare au Heroes Acre baada ya makubaliano kufikiwa kuwa mnara wa makumbusho utajengwa kumuenzi kiongozi huyo wa kwanza wa Zimbabwe.

Katika taarifa iliyochapishwa Alhamisi wiki hii, Waziri wa Mawasiliano Nick Mangwana, alisema mabadiliko hayo yanazingatia sera ya "kuheshimu uamuzi wa familia ya marehemu".

Mugabe alifariki akiwa nchini Singapore alipokuwa anatibiwa saratani na mwili wake kusafirishwa kurudishwa nyumbani Zimbabwe.

Baada ya kifo chake familia yake ililalamika hadharani kuwa haikushauriwa kuhusu mipango ya mazishi yake ya kitaifa.

Katika taarifa familia hiyo ililaumu serikali kwa kutumia nguvu kupanga mazishi ya Mugabe katika makaburi ya mashujaa kinyume na "matakwa yake]".

Taarifa hiyo aidha , ilisema kuwa ombi lake la mwisho lilikuwa la mke wake , Grace Mugabe, kutoondoka kando ya jeneza lake hadi atakapozikwa.

Familia yake inasemekana kughadhabishwa na jinsi kiongozi huyo alivyong'olewa madarakani na mshirika wake, wa zamani Rais Emerson Mnangagwa, miaka miwili iliyopita, hali ambayo huenda imesababisha mvutano kuhusu mahali atakapozikwa.Mnangagwa alipendekeza kiongozi huyo azikwe Heroes Acre.

Mugabe, alikua Rais wa kwanza wa Zimbabwe baada ya nchi hiyo kupata uhuru mwaka 1980.

Miaka ya awali ya uongozi wake, alisifiwa kwa kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya na elimu kwa waafrika walio wengi

Mugabe alikuwa madarakani kwa karibu miongo minne kabla ya kuondolewa kupitia mapinduzi ya kijeshi mwaka 2017 na wadhifa wake kuchukuliwa na Rais wa sasa Emerson Mnangagwa.

*BBC*



Hawa ni miongoni mwa kundi la wahamiaji 66 waliowasili nchini Rwanda kutoka Libya. **PICHA REUTERS**

# Trump akalia kaa la moto

**WASHINGTON, Marekani**

HATIHATI za kumchunguza Rais wa Marekani Donald Trump zimeingia kwenye hatua nyingine baada ya kubainika kuwa mfichua siri ni ofisa wa Shirika la Ujasusi la Marekani la CIA

Mfichua siri ambaye ushahidi wake umesababisha uchunguzi dhidi ya Rais Trump ni ofisa wa shirika la ujasusi la hatihati za kumshitaki Marekani CIA, kwa mujibu wa vyombo vya habari vya Marekani.

Ofisa huyo ambaye jina lake halijatajwa aliwahi kufanya kazi katika Ikulu yaWhite House, vinasema vyombo kadhaa vya habari nchini humo.

Mfichua siri huyo alisema maofisa wa ngazi ya juu wa Ikulu ya White House walijaribu kuficha vielelezo vya mawasiliano ya simu baina ya Rais Donald Trump na Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky.

Trump alitaka kujua ni nani aliyempatia taarifa mfichua siri huyo,akiongeza kuwa aliyefanya hivyo "anakaribia kuwa jasusi".

Aidha, alishutumiwa kwa kutafuta msaada kutoka nchi ya kigeni kwa minajili ya kumchafua kisiasa mpinzani wake Joe Biden na kutumia msaada wa kijeshi kama nyenzo ya kutaka matakwa yake yatimizwe.

Biden ndiye kinara wa mbio za tiketi ya kugombea urais 2020 kwa chama cha Democrats.

Rais Trump alikiri kuwa alimzungumzia Joe Biden na Zelensky na kuwa alizuia msaada wa kijeshi kwa nchi hiyo wa thamani ya Dola milioni 400.

Lakini , alikanusha kuwa alifanya hivyo kama shinikizo kwa Ukraine ili kumchunguza Biden.

Hakuna taarifa za kina kumhusu lakini wakili wake ameionya kuwa jaribio la kubaini ni nani litamweka hatarini.

Magazeti ya New York Times, Washington Post, na shirika la habari la Reuters yalidai kuwa mfichua siri huyo ni ofisa wa CIA.

Kwa mujibu wa mukhtasari uliotolewa jana na Ikulu ya White House, Trump alimwambia Zelensky juu ya namna ambavyo Joe Biden akiwa Makamu wa Rais alishawishi Ukraine kumtimua kazi Mwendesha Mashtaka wake mkuu, Viktor Shokin, mwaka 2016.

Ofisi ya Shokin ilifungua jalada la uchunguzi dhidi ya Burisma, kampuni ya gesi asili ambayo mwana wa Joe Biden, Hunter alikuwa ni mjumbe wa bodi yake.

Nchi kadhaa za magharibi pia zilikuwa zikishinikiza Shokin atimuliwe kazi kwa madai alikuwa akibariki vitendo vya rushwa.

"Nimesikia mlikuwa na mwendesha mashtaka ambaye alikuwa ni mzuri kweli na alifutwa kazi kwa njia ya uonevu. Watu wengi wanalizungumzia jambo hilo," Trump ananukuliwa akisem kwenye mazungumzo hayo na kuongeza:

"Kitu kingine, kuna mjadala mkubwa kumhusu mtoto wa Biden, kuwa baba yake alizuia waendesha mashtaka na watu wengi wanataka kujua undani wa hilo, kwa hiyo chochote unachoweza kufanya na Mwanasheria Mkuu wa Marekani litakuwa jambo jema.

"Biden alikuwa akijitamba kuwa amezuia uchunguzi angalia utakachokifanya hapo ni jambo baya sana kwangu."

# Wahamiaji Libya watua Rwanda

**KIGALI, Rwanda**

KUNDI la wahamiaji 66 linalojumuisha watu watu walio hatarini zaidi pamoja na watoto walio peke yao limewasili nchini Rwanda kutoka Libya, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kushughulikia Wakimbizi (UNHCR), limesema.

Miongoni mwa watu hao ambao baadhi yao wanatoka mataifa ya Pembe ya Afrika, ni mtoto wa miezi miwili mwenye asili ya Kisomali aliyezaliwa katika kituo cha kuwazuilia wakimbizi nchini Libya.

Msemaji wa UNHCR Kanda ya Afrika Charlie Yaxley, aliiambia BBC nchini Rwanda kuwa shirika hilo litawatafutia stakabadhi za kuomba hifadhi wale ambao wanataka kuishi Rwanda au kuwasaidia wale wanaotaka kurejea makwao.

"Nchini Rwanda tutawapatia chakula, maji , malazi na mahitaji mengine ya muhimu. Tuna watalaamu tisa watakaowasaidia katika kupona kiwewe cha yale waliyoyapitia Libya" Yaxley alisema.

Wahamiaji hawa wataishi katika kituo cha muda kilichopo umbali wa saa moja kwa gari kutoka mjini Kigali.

Akitoka katika kituo cha ukusanyaji wa wahamiaji cha Libya, Daniel, mmoja wa wahamiaji katika kundi lililohamishiwa Rwanda aliiambia BBC wiki iliyopita kuwa wanafurahia kuondoka Libya.

"Tulipokuwa tunaweka sahihi ya kidole gumba tuliona barua inayosema tunaondoka kuelekea Rwanda na tukajihisi ni kama tulikuwa tunatengana na kifo "

Zaidi ya wahamiaji 4,500 wanashikiliwa katika mahabusu baada ya ndoto yao ya kuvuka bahari ya Mediterranean kuelekea Ulaya kukatizwa.

Rwanda ilikubali kuwahifadhi wahamiaji 500 kwa ushirikiano na UNHCR, na Muungano wa Afrika ulitoa hakikisho la usafiri wao wa kutoka Libya kuelekea Rwanda , ili kuwaepusha na hatari ya kushambuliwa kwa roketina kubakwa . Haijafahamika wazi ni kwa muda gani wahamiaji hao watakuwa Rwanda na wana uhuru kwa kiwango gani kuondoka nchini humo

"Wakimbizi watakaotaka kuishi Rwanda daima watapewa ukimbizi ," alisema Olivier Kayumba, Katibu wa Kudumu katika Wizara ya Udhibiti wa Masuala ya Dharura na Masuala ya Wakimbizi .

**BBC**

# HADITHI

# Jumba Jekundu-20

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawatajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.
Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina.
Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**




MWAKA wa pili wa masomo ulimalizika. Kadili alirejea nyumbani kusubiri matokeo ya mtihani wake. Alipokewa vema na mama na dada zake kama kawaida. Rafiki yake Meze naye hakuwa nyuma.

Alikuwa na furaha ya kumaliza masomo. Hakuwa na uhakika kama atakwenda tena kusoma mwaka wa tatu.

Tatizo lilikuwa ni ada. Ilikuwa imezidi uwezo wa mama yake kwa sababu kila anapozidi kwenda juu, ada inaongezeka. Hata hivyo, tayari alishaongea na jamaa yake mmoja kama akimaliza tu mwaka wa pili, aweze kumpatia kazi kwenye kampuni moja ya simu akawe mmoja wa mafundi wa kompyuta na teknolojia na mitandao.

Akili yake ilimwambia kwanza apate kazi na anaweza kusoma mwaka wa tatu akiwa kazini ili kumpunguzia mama yake mzigo.

Aliwasiliana na jamaa yake, ambaye alimwambia aandike barua ya kuomba kazi, na abakie tu kusubiri majibu.

Asubuhi mapema, Kadili aliamka kwenda kwenye meza za magazeti yaliyo kwenye barabara kuu itokayo Magomeni kwenda Sinza Kijiweni, mitaa ya Tandale Kwa Mtogole.

Huwa anapenda sana kwenda hapo hata kama hana pesa za kununulia magazeti. Hapo hupenda kusoma vichwa vya habari. Mijadala na ubishi wa mambo ya siasa na michezo, huwa pia inamvutia anapokwenda hapo.

Vijana kwa wazee hukusanyika na hapo na kuzua ubishani. Ukikuta hoja za kisiasa, au ubishani wa mpira utapenda.

Wakati mwingine hupitisha muda wa asubuhi hapo hadi wakati wa mchana anapoamua kurejea nyumbani.

Siku hiyo alikuwa na pesa ya kununulia gazeti. Alipenda mno gazeti linaloongoza nchini Tanzania, Nipashe. Baada ya kusikiliza mada za hapa na pale alirejea nyumbani na hakuwa na hakupata muda wa kulifungua.

Alipomaliza kunywa chai na kuviteketeza tumboni mwake vitumbua vitatu, alihisi kitu kama usingizi.

Kabla ya yote aliona kwanza apitie kwanza habari mbalimbali muhimu. Alifanya kama alivyokusudia.

Alipomaliza kusoma hadi kwenye kurasa za michezo alifunua tena ndani ili kuangalia habari mbalimbali na matukio.

Alikutana na picha moja ambayo awali hakuitilia maanani, kutokana na akili yake kuelekea zaidi kusoma habari muhimu za kitaifa.

Alitaka kuhakikisha kuwa kile alichokiona ni sahihi. Aliona kama anafanisha. Chini ya picha kuna maandishi.

Aliyasoma ili kuthibitisha kile alichokiona. Hakukuwa na tofauti yake ya maelezo na picha yenyewe.

Juu ya picha kulikuwa na kichwa cha habari. Nacho pia kilisadifu kile alichokiona.

Kijasho chambamba kilimtoka. Hakuamini. Alitaka kile anachokiona kiwe ni ndoto au tamthilia na si tukio halisi.

Moyo wake aliongezeka mapigo. Wakati mwingine yalionekana kupiga katika hali isiyo ya kawaida. Yalipiga zaidi ya mara moja, juu ya muda wake wa kawaida.

Mikono ilianza kucheza, na kukosa nguvu hata ya kuendelea kulishika gazeti, likaanguka.

Akainama kivivuvivu na kuliokota tena. Alifungua tena pale pale. Akaangalia kana kwamba ndiyo anatazama kwa mara ya kwanza.

Ilikuwa ni picha ya watu wawili. Mwanaume na mwanamke. Watu hao wawili walionekana wanatoka ka kanisani kufunga ndoa. Tayari wameshakuwa wanandoa.

Mwanaume alionekana ni mtu mzima aliyemkadiria kuwa na miaka inayokaribia 60. Alikuwa amevaa suti ilivyomkaa vema. Alionekana ama ni mtu tajiri au mwenye madaraka fulani serikalini.

Wa pili ambaye ni bibi harusi, alikuwa ni msichana asiyezidi miaka 25. Alikuwa ni msichana mrembo. Na urembo wake uliongezeka maradufu na vikorombwezo vya mapambo alivyopambwa na wataalam wa kupamba. Picha hiyo kwa hali ya kawaida ilipendeza sana. Ingempendeza yoyote ile ambaye angeiangalia.

Mtu mmoja tu ambaye hakupendezwa na picha hiyo. Ni kadili.

Hakupendezwa kwa sababu moja tu. Bibi harusi aliyeolewa alikuwa anamfahamu. Ni Edina.

"Edina umeolewa?" Ni kama alikuwa anaiuliza picha iliyokuwa kwenye gazeti la Nipashe.

Moyo ulimkereketa kuona Edina ameshaolewa. Pamoja na kwamba hajawahi hata siku moja kumuambia msichana huyo kuwa anampenda mara zote tatu walizokutana 'Blue Star Hotel' na kucheza muziki.

Licha ya ukweli kuwa kwa uwezo wake na ufukara alionao asingeweza kuthubutu kummiliki msichana aliyetoka kwenye familia ya urajiri uliotopea Edina. Pamoja na kutekea na mateso yote aliyoyapata ndani ya jumba jekundu. Licha ya mkwara mkali kutoka kwa Madame Pauline mama mzazi wa Edina. Pamoja kiapo alichoapa mbele ya mama yake kuwa aachane na mawazo ya msichana huyo wa kitajiri kwani anaweza kuuawa, badala yake aangalie zaidi masomo yake. Bado Kadili ni mwanaume aliyekamilika. Mwanaume mwenye matamanio na wivu. Moyo wake uliondokea kumpenda Edina, licha ya changamoto zote hizo.

**"Binti yangu bado mdogo, halafu kifaa cha nguvu. Si unamuona? Huyu si msichana wa kuolewa na mtu kapuku kama wewe. Kula yako na vaa yako shida huyu unamuweza wewe? Hapa unaponiona, kichwa kinaniuma, maana wanaume kibao wenye wadhifa na pesa zao wametuma washenga kutaka kumuoa binti yangu, yaani sijui nimkubali nani nimuache nani. Halafu kanatokea kajitu kama wewe nako...**

Hivyo picha hiyo ilimuumiza mno Kadili.

"Binti yangu bado mdogo, halafu kifaa cha nguvu. Si unamuona? Huyu si msichana wa kuolewa na mtu kapuku kama wewe. Kula yako na vaa yako shida huyu unamuweza wewe? Hapa unaponiona, kichwa kinaniuma, maana wanaume kibao wenye wadhifa na pesa zao wametuma washenga kutaka kumuoa binti yangu, yaani sijui nimkubali nani nimuache nani. Halafu kanatokea kajitu kama wewe nako, eti nako kanajitia kutaka kupimana ubavu na watu hao," Alisema na kuonekana kama kuutua mzigo mzito uliokuwa kwenye kifua chake.

Kuna mawaziri, mapofesa, madaktari na wafanyabiashara wakubwa nchini mpaka watoto wa vigogo wanataka kumuoa Edina, hadi marubani wa ndege. Lakini kwa sababu ni lazima aolewe na mtu mmoja, nimetuliza kichwa ili nione kati ya hao nani anaweza kuwa mtu sahihi kwa binti yangu ili asiende kupata tabu kwa sababu mimi mwenyewe mama yake nimemzaa na kumlea kwa mapenzi makubwa. Amelelewa kitajiri na hajawahi kupata shida yoyote."

Kichwa cha Kadili kilirudisha kumbukumbu nyuma na maneno ya Madame Pauline alipokuwa akitamba na kujinasibu ndani ya jumba jekundu yalijirudia kwenye ubongo wake.

"Sasa ndiyo tayari Madame Pauline ameikamilisha kazi yake aliyokuwa anaisema ya kumuozesha binti yake." Kadili alijisemea mwenyewe kimoyomoyo.

Habari hiyo mbaya hakutaka mama yake ajue. Aliamua iwe siri kwa sababu itaonekana ni kama anaendelea kuzifuatilia habari za msichana huyo wakati ameshakatazwa. Akakumbuka jinsi alivyokalishwa chini na kukanywa juu ya habari za huyo binti.

"Mwanangu mimi na dada zako unatuona. Ni masikini wa kutupwa. Tunakuhitaji wewe ili uje utukomboe. Nakuomba sana tena sana, nenda kasome. Usijiingize kwenye mambo mengine ambayo yanaweza kusababisha masomo yako yashuke au kuhatarisha maisha yako, kama lilivyotokea hili." Hayo yalikuwa ni maneno ya mwisho ya mama yake kabla hajaondoka kurejea masomoni katikati mwa mwaka na ilikuwa baada ya kutekwa na mabaunsa wa mama Edina, Madame Pauline.

Kuanzia wakati huo, Kadili alionekana kutokuwa kwenye hali nzuri, japo mwenyewe alijitahidi mno kuficha hali hiyo.

"Vipi leo mwanangu, unaumwa?" Mama aliuliza.

"Kwani vipi mama, mbona mzima tu."

"Naona kama hauko vizuri. Nimekuzaa mwenyewe. Nakujua. Kama kuna kitu kinakutatiza mimi najua na hata ukiwa na furaha najua tu, hata kama ukitaka kunificha furaha au huzuni uliyonayo mwanangu."

"Hapana mama uchovu tu."

**Itaendelea Jumamosi**

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### VIWANJA / MASHAMBA

**VIWANJA/NYUMBA.,** Hekari 25 zinauzwa Kisongo Arusha @Mil12. Heka 100 @Mil 8 Meserani Arusha. Kisongo.20x20 mil 3.3, 20x40 mil25. Nyumba inauzwa Usariver self ya bedroom4 mil70, hati ipo. Wasiliana na 0755 907 520.

**NYUMBA INAUZWA,** NYUMBA INAUZWA SINZA LION KUELEKEA KWA MWAIBULA NYUMA YA DEFRANCE HOTEL, BLOCK E PLOT No. 665, 288 SQM. MAWASILIANO: 0713 525954 / 0787 822000.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**
**KAGERA LILILOPO BUKOBA**
**MAOMBI NA: 223/2010**

**SALAH SAVED KAKWEZI ............MDAI**

**DHIDI YA**
**1, MARICK CONSTANTINE KATISEKI**
**2, DAVID MUSHANA ......WADAIWA**
**KWA: MARICK CONSTANTINE KATISEKI NA DAVID MUSHANA.**
**(POPOTE PALE MLIPO)**

**Mnaarifiwa/ unaarifiwa kuwa Maombi Na:** 223/2010 yamepangwa kutajwa tarehe 01.10.2019 mbele ya mwenyekiti wa baraza , R.Mtei saa 2:00 asubuhi.

Hivyo, unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/ mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa baraza hili leo tarehe 27.08.2019

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
BUKOBA

115436902

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Kampuni ya **TEXAS HARDWARE** inatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba T 500 DNU, ENGINE namba 51528081572810, CHASIS Namba WMA24SZZ2BW159754.

Kwa atakae iona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kwa Kumb. **MWA/NY/RB/334929/2019.**

115436502

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

NISHIT JAYANTILAL SHAH ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA IST YENYE NAMBA ZA USAJILI T 209 DKH YENYE RANGI YA SILVER, CHASSIS NAMBA NCP600127432 NA ENGINE NAMBA 2NZ2926180.

KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.

TAARIFA YA POLISI: **KAH/TR/RB/760/2019.**

115436402

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**WUZHOU INVESTMENT COMPANY LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili MC 957 BPB SANLG. Chassis namba LBRSPJB53G9054493. Engine namba 16973326.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **Control No. 991088981142.**

115436302

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**MOMELA THABITI MASASI** amepotelewa na kadi ya pikipiki aina ya SANLG yenye namba za usajili MC 578 BHA.

Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya polisi: **MOR/MOR/RB/196397/2019**

115436202


**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie 0767 223 311

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII


**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO




# RASHFORD
# KUIKOSA ARSENAL

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI Marcus Rashford wa Manchester United, ataukosa mchezo wa Ligi Kuu England dhidi ya Arsenal keshokutwa, Jumatatu.

Rashford alitolewa uwanjani kwenye mechi ya kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya West Ham United wikiendi iliyopita, lakini sasa ataendelea kukosa mechi zaidi, huku Man United wakiwa kwenye majaribu makubwa kuhusu fowadi wake, ikiwamo imewaondoa Romelu Lukaku na Alexis Sanchez na hawajasajili mbadala wao.

Man United ilikuwa na mpango wa kumsajili straika wa Juventus Mario Mandzukic wakati ilipowaacha Sanchez na Lukaku kwenda Inter Milan, lakini dili hilo lilishindwa kukamilika na sasa wanaisoma namba.

Kwa kuwa na huduma yake tu, Man United ilikuwa haina uhakika sana kwenye safu yake ya ushambuliaji, hivyo kwa kitendo cha kumkosa katika mechi hiyo ya Arsenal inawapa wakati mgumu zaidi na kuwafanya wabaki kuwa na tumaini la kumtumia kinda Mason Greenwood pekee kwenye fowadi.

Kocha, Ole Gunnar Solskjaer alisema: "Marcus hajapona. Hayupo vibaya sana, lakini tunaamini atakuwa fiti kabla ya mapumziko ya mechi za kimataifa."

Kutokana na hilo, Rashford mechi anazozitarajia kuzikosa kwenye Ligi Kuu England ni ya Arsenal na Newcastle United, wakati kwenye Europa League hatakuwamo uwanjani katika mechi dhidi ya AZ Alkmaar.

## 'MADRID IMEKOSEA KUMUUZA RONALDO'



**MADRID, Hispania**

RAIS wa zamani wa Real Madrid, Ramon Calderon, amesema hadi sasa hakubaliani kabisa na uamuzi wa kumpiga bei mshambuliaji Cristiano Ronaldo.

Nyota huyo wa Ureno Ronaldo aliachana na Madrid mwaka jana na kwenda kujiunga na Juventus na Calderon anaamini jambo hilo limeacha pengo kubwa kwenye kikosi cha Los Blancos, ambalo halijazibwa hadi sasa.

Calderon alisema: "Hakupaswa kabisa kuondoka. Hakika kilikuwa kitu cha kushangaza kumwachia aondoke.

"Ni ngumu sana kucheza bila ya huduma ya mchezaji yule kama alidumu kwenye kikosi chako kwa muda mrefu na mifumo yote kumtegemea.

"Alikuwa na uhakika wa mabao 60 kwa msimu... hakuna mchezaji mwingine anayeweza kukuhakikishia hilo.

"Pengo lake halizibwi ni kama (Lionel) Messi. Nilishangazwa kwa mengi yaliyotokea, wakati Florentino (Perez) alipokuwa akisema kwamba saini ya Cristiano ni muhimu kwenye timu, lakini imekuwa tofauti."

Ronaldo kwa sasa anatamba huko Juventus, huku klabu yake ya Real Madrid ikiwa kwenye majanga makubwa kutokana na kutokuwa na uhakika kwenye safu yake ya ushambuliaji kuhusiana na wafungaji wake.

## PAYET AFUNGIWA MECHI 4 UFARANSA

**PARIS, Ufaransa**

MSHAMBULIAJI wa Olympique de Marseille, Dimitri Payet amefungiwa michezo minne, kufuatia tukio la kumtusi mwamuzi wakati wa mchezo wa Ligi Kuu ya Ufaransa dhidi ya Montpellier mwishoni mwa juma lililopita.

Payet alionyeshwa kadi nyekundu dakika za mwisho, baada ya kuzozana na mwamuzi baada ya kuchukua maamuzi dhidi ya timu yake, ambayo ililazimishwa sare ya 1-1.

Kamati ya nidhamu ya Shirikisho la Soka Ufaransa (FFF), imepitia ripoti ya mwamuzi Amaury Delerue, na baadaye kujiridhisha kupitia picha za televisheni kuhusu tukio hilo.

Kufuatia adhabu hiyo, Payet atakosa mchezo wa mwishoni mwa juma hili dhidi ya Rennes, na ataendelea kuwa nje ya uwanja dhidi ya Amiens SC na PSG.



# WACHEZAJI ARSENAL WAPIGA KURA KUMCHAGUA NAHODHA



**LONDON, England**

WACHEZAJI wa Arsenal waliombwa kupiga kura ya siri kwa ajili ya kuchagua nahodha wao mpya, Rob Holding amebainisha.

Granit Xhaka amekuwa akivaa kitambaa cha unahodha kwa wiki za mwanzo za msimu huu wa 2019-20, huku kocha, Unai Emery bado akiwa hajathibitisha nani atakuwa nahodha wa kudumu.

Msimu uliopita alitaja kundi la manahodha watano akiwamo, Xhaka na Mesut Ozil, lakini watatu kati yao, Laurent Koscielny, Petr Cech na Aaron Ramsey wameondoka Arsenal.

"Tulipiga kura wiki iliyopita, hivyo tutaona nini kitatokea na kuangalia nani atatajwa," beki Holding amesema akiwaambia waandishi wa habari mara baada ya kushinda mabao 5-0 dhidi ya Nottingham Forest katika mchezo wa Kombe la EFL.

"Tulitakiwa kuandika majina na kumpa kocha. Atayapitia na tutaona nini kitatokea.

"Sijui lini ataamua na kutangaza. Nafikiri ndani ya wiki chache zijazo. Hata hivyo, sina uhakika."

Wachezaji kumchagua nahodha wake si jambo la kawaida, ingawa David Silva alichaguliwa na wachezaji wenzake wa Manchester City kuwa nahodha wakati huu wa mwaka wake wa mwisho klabuni hapo.

Mashabiiki wa Arsenal wamekuwa wakimtaja Holding kama ndiye anayefaa kuwa nahodha mpya kwani alivaa kitambaa hicho mara baada ya Ozil kutolewa nje kwenye mchezo dhidi ya Forest.

"Ningependa kuwa nahodha na kuwa nahodha wa Arsenal si jambo dogo," aliongeza kusema.

"Utakuwa wakati mzuri zaidi kwangu. Tutaangalia nini kitatokea ndani ya wiki chache zijazo. Kama nikipata nitakuwa na furaha kubwa.

"Wakati nilipoambiwa nitakuwa nahodha msaidizi ilikuwa ni heshima. Haraka Mesut alivyotoka nje, nilijua kwamba nitapewa kitambaa cha unahodha."

# Pogba kuondoka Man United Januari

**MANCHESTER, England**

PAUL Pogba ameripotiwa kwamba, bado yuko mbioni kuachana na Manchester United kwenye dirisha lijalo la usajili wa kipindi cha majira ya baridi Januari mwakani.

Ole Gunnar Solskjaer amekuwa na changamoto kwenye kikosi chake hasa eneo la kiungo mkabaji hivyo haitakuwa rahisi kumwachia bila ya kuwa na mbadala wake.

Manchester United wanadai thamani ya kiungo huyo wa Kifaransa kuwa ni Paund 180 milioni, hivyo haitakuwa rahisi kwa Real Madrid na Juventus, ambao wamekuwa wakivutiwa naye kumng'oa Old Trafford.

Kwa mujibu wa The Sun, Pogba hana mpango wa kusaini mkataba mpya wa kuendelea kuitumikia Manchester United kutokana na dhamira yake ya kutaka kuondoka.

Kwenye maandalizi ya msimu huu, Pogba alitaka kuondoka Manchester United, lakini wakiwa Australia inadaiwa walifanya kazi kubwa ya mshawishi kiungo huyo asalie Old Trafford.

Lakini kwa sasa Pogba, ambaye alikosa michezo mitatu kabla ya kurejea kwenye mchezo dhidi ya Rochdale, ameonekana kutaka kuondoka.



# Barcelona yalimwa faini kwa Griezmann

**BARCELONA, Hispania**

KLABU ya Barcelona imetozwa faini ya Euro 300, baada ya kubainika walikwenda kinyume na taratibu za usajili wa Antoine Griezmann.

Kamati ya mashindano ya Shirikisho la Soka Hispania (RFEF), imeendesha kesi iliyomuhusu mshambuliaji huyo kwa muda wa miezi miwili, baada ya uongozi wa Atletico Madrid kuwasilisha malalamiko yao dhidi ya Barcelona.

Atletico Madrid waliilalamikia Barcelona kuvunja taratibu za usajili, kwa kufanya mazungumzo na Griezmann akiwa bado na mkataba na klabu hiyo ya mjini Madrid, jambo ambalo ni kinyume cha kanuni.

Kufuatia uchunguzi wa kina uliofanywa na Kamati ya Mashindano ya RFEF, imebainika ni kweli Barcelona walitenda kosa hilo, hivyo wameadhibiwa kwa kutozwa faini ya Euro 300, na kutakiwa kutorudia tena kosa kama hilo.

Barcelona walimsajili Griezmann kwa ada ya Euro milioni 120 Julai mwaka huu.

## HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HIGUAIN: RONALDO HUYU SI YULE WA REAL MADRID

●●●Tulishacheza pamoja tukiwa Real, miaka mingi imepita, na nimemuona mchezaji mwingine, mtu aliyepevuka zaidi...

**TURIN, Italia**

Gonzalo Higuain amesema mchezaji mwenza wa Juventus, Cristiano Ronaldo amepevuka zaidi tangu wawili hao walipokuwa pamoja Real Madrid.

Mshambuliaji huyo wa Juve, Higuain na Ronaldo wamekutana tena pamoja hapo Turin baada ya wawili hao kushinda mataji matatu ya La Liga wakiwa na miamba ya Madrid kabla ya kutimkia Napoli mwaka 2013.

Higuain hatimaye alijiunga na Juventus mwaka 2016, wakati Ronaldo alitua klabuni hapo msimu wa 2018-19, na kusababisha mchezaji mwenza huyo wa zamani wakati wakiwa Madrid, kuhamia kwa mkopo kwa wapinzani wao wa Serie A, AC Milan na kisha Chelsea msimu uliopita.

Higuain na Ronaldo, ambao walishinda taji la Scudetto katika msimu wao wa kwanza, kwa sasa wapo pamoja tena wakati huu wakiwa chini ya Kocha Mkuu wa Juventus, Maurizio Sarri, na nyota huyo wa zamani wa kimataifa wa Argentina, amemsifu mshindi huyo mara tano wa tuzo ya Mchezaji Bora wa Dunia ['Ballon d'Or'].

"Tayari tulishacheza pamoja tukiwa Real," Higuain, ambaye amevutia akiwa na mabingwa hao wa Serie A msimu huu, aliiambia Fox Sports.

"Miaka mingi imepita, na nimemuona mchezaji mwingine, mtu aliyepevuka zaidi, akiwa na familia.

"Nilifurahia kucheza pembeni yake kabla na ni mwenye furaha kuwa tupo pamoja tena."

Higuain ana mkataba na Juve hadi mwaka 2021 na hajaweka pembeni uwezekano wa kurudi kuitumikia miamba ya Argentina, River Plate.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, alitengeneza jina lake mwenyewe wakati akiwa River, akiibukia katika kikosi cha makinda mwaka 2005 na kuifungia jumla ya mabao 15 kabla ya kutua Santiago Bernabeu kuitumikia Madrid mwaka 2007.

"Nina mwaka huu na ujao uliobaki [hapa Juventus]," Higuain aliongeza. "Sijafunga mlango kwa chochote.

"[Kwa River] kuna kocha mzuri na baadhi ya wachezaji wenza wangu ambao ninamahusiano mazuri nao.

"Watu wa River mara zote wamekuwa wa kuvutia kwangu. Lakini, kwa sasa ninajaribu kufikiri nilipo na kufarahia wasaa wangu hapa katika soka la Italia."

## KWA UFUPI

**POGBA HAJATULIA UNITED**
KIUNGO wa kimataifa wa Ufaransa Paul Pogba, 26, atajaribu kwa mara nyingine kufanya mchakato wa kuondoka Manchester United katika dirisha la Januari. ***(Sun)***

**KENYON KUINUNUA NEWCASTLE**
MKURURENZI Mkuu wa zamani wa Chelsea na Manchester United, Peter Kenyon afungua mchakato mpya wa kuinunua Newcastle United pamoja na ofa mpya ya kumlipa mmiliki Mike Ashley kiasi cha pauni milioni 125. ***(Mail)***

**NEYMAR KIZIMBANI NA BARCA**
MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain, Mbrazil Neymar, 27, ametua Hispania kwa ajili ya kesi yake na klabu yake ya zamani, Barcelona kuhusu kutolipwa bonasi yake ya usajili. ***(Mundo Deportivo)***

**BARCA, ATLETICO KUPINGA DAU**
BARCELONA na Atletico Madrid zote zitakata rufaa kuhusu uamuzi wa kupigwa faini ya pauni 265 kwa kuzungumza na straika Mfaransa Antoine Griezmann wakati akiwa Atletico. ***(Marca)***

**BECKHAM KUWA WAKALA**
NAHODHA wa zamani wa England, David Beckham anajiandaa kuwa wakala wa soka, huku mshambuliaji wa Manchester United, Mason Greenwood, 17, kukiwa na uwezekano kuwa mteja wake. ***(Mirror)***

**DEMBELE AWINDWA UNITED**
MANCHESTER United inataka kumfuata straika Mfaransa Moussa Dembele, 23, katika dirisha la usajili la Januari na tayari imeshatuma mashushu wake kwenda kumuona akicheza katika mechi tatu za Lyon zilizopita. ***(Mail)***

**ELLIOTT KUIGHARIMU LIVERPOOL**
FULHAM inataka kufidiwa takriban pauni milioni saba kutoka Liverpool baada ya kiungo Harvey Elliott, 16, kujiunga na 'Wekundu' hao majira ya joto. ***(Times)***

**DE JONG AITAJA MAN CITY**
KIUNGO wa Barcelona na Uholanzi, Frenkie de Jong, 22, amesema angeweza kujiunga na ama Manchester City au PSG kama asingetua kuitumikia miamba hiyo ya Hispania akitokea Ajax majira ya joto. ***(Star)***

**POCHETTINO ANUKIA OLD TRAFFORD**
MANCHESTER United ipo tayari kufanyia kazi dau la pauni milioni 32 linalohitajika ili kuvunja mkataba wa kocha wa Tottenham, Mauricio Pochettino. ***(Sun)***

**PALACE KUMRUDIA STEPANENKO**
CRYSTAL Palace inazingatia uwezekano wa kumfuata kiungo mkabaji wa Shakhtar Donetsk, Taras Stepanenko, 30, katika dirisha la Januari baada ya kupoteza nafasi ya kumsajili nyota huyo wa kimataifa wa Ukraine kwa pauni milioni nane majira ya joto. ***(Sun)***

**NAHODHA ARSENAL KWA KURA**
WACHEZAJI wa Arsenal wamepewa jukumu la kupiga kura za siri kuamua nani awe nahodha wa klabu hiyo wakati huu kocha Unai Emery akitazama uwezekano wa kutengeneza tena kundi la viongozi watano. ***(Telegraph)***

**ROCHDALE LULU NEWCASTLE**
NEWCASTLE imekuwa ikimfuatilia beki wa Rochdale, Luke Matheson, 16, ambaye alifunga bao dhidi ya Manchester United Jumatano, tangu alipocheza mechi yake ya kwanza mwaka jana. ***(Chronicle)***

# MALINDI PUNGUFU WAIFUATA AL MASRY

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAWAKILISHI pekee wa Zanzibar katika mashindano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika (Caf), timu ya Malindi FC wameondoka visiwani hapa jana kuelekea nchini Misri katika mchezo wake wa marudiano dhidi ya Al-Masry huku ikiwa na wachezaji 16 tu.

Kwa maana hiyo kwenye benchi Malindi itakuwa na wachezaji watano tu wa akiba badala ya saba ambao wanaruhusiwa kisheria.

Akizungumza na gazeti hili msemaji wa timu ya Malindi, Abdalla Thabit, alisema msafara huo umeondoka na jumla ya watu 22 wakiwamo wachezaji 16, kocha mkuu na msaidizi wake, pamoja na viongozi wa timu hiyo.

Alisema hapo awali timu hiyo ilitarajiwa kuondoka Septemba 24, mwaka huu, lakini kutokana na sababu zilizojitokeza ikiwamo kuchelewa kukamilisha hati za kusafiria na visa kwa baadhi ya wachezaji, ndiko kulikochangia kuchelewa hadi jana walipoondoka.

Akizungumzia juu ya uchache wa watu waliondoka katika msafara huo tofauti na ilivyozoeleka kwa timu, alisema changamoto ya fedha ndicho kitu kilichofanya kuondoka kwa watu hao wachache wakati hapo awali walipanga kuondoka na wachezaji 20 pamoja na viongozi watano.

Hata hivyo, alisema kikosi hicho kimejiandaa kwenda kupambana na wapo tayari kukukabiliana na matokeo watakayoyapata.

Timu ya Malindi ilifanya vibaya mchezo wake wa nyumbani baada ya kukubali kupigo cha mabao 4-1 kutoka kwa Al-Masry kwenye mechi ya awali iliyopigwa Uwanja wa Amaan sisiwani hapa, hivyo inahitaji ushindi kuanzia mabao 4-0 ili kuweza kusonga mbele.




Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas (kushoto), akimkabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 23.7, mshindi wa Jackpot Bonasi, Joachim Charles, baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 za Jackpot ya SportPesa wiki iliyopita. **MPIGAPICHA WETU**

# Mshindi mil. 23/- SportPesa awaasa wazazi

**Na Mwandishi Wetu**

Wazazi nchini wameaswa kutowazibia riziki ya kuwa milionea watoto wao kupitia Kampuni bora ya Michezo ya Kubashiri ya SportPesa, imeelezwa.

Rai hiyo imetolewa na Richard Mbele ambaye ni kaka wa mshindi wa Sh. milioni 23.7 za Jackpot Bonasi, Joachim Charles mkazi wa Mbinga, Ruvuma aliyejinyakulia fedha hizo baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 za Jackpot ya SportPesa wiki iliyopita.

"Wapo wazazi ambao wanaamini mchezo huu hauna maana bali ni kupoteza muda tu, mimi nashauri kwamba isiwe lazima kila mtu kucheza, lakini ni vema wazazi wawasapoti watoto wao wenyewe katika kucheza mchezo huu na si kuwakataza kwani riziki mafungu saba hauwezi kujua fungu lako ni lini," alisema Mbele ambaye ndiye alimfundisha mdogo wake kucheza na SportPesa.

**Mwaka Mmoja Fedha Kibao**

Kwa upande wake mshindi wa bonus hiyo, Joachim amesema alianza kucheza mwaka 2018 baada ya kufundishwa na kaka yake na kwamba kuna kipindi alikata tamaa na kusimama kabisa kucheza kabla ya kuja kuendelea hadi aliposhinda fedha hizo.

"Nimeanza kucheza mwaka 2018 ikiwa ni kipindi cha takriban mwaka mmoja hivi baada ya kufundishwa na kaka yangu. Hata hivyo, safari yangu haikuwa rahisi kwani kuna kipindi nilikata tamaa kabisa na nikaacha kucheza, lakini baadaye nilirudi kwa nguvu nikacheza na hadi leo nimeshinda," alisema Joachim ambaye ni fundi wa magari.

**Hakuna Udanganyifu**

Joachim, 25, anawaamsha Watanzania kwa kuwaambia kuwa wasikate tamaa kama wana nia ya kushinda kupitia SportPesa kwa kuwa hakuna suala la kujuana kwani ukiweka bashiri zako na matokeo yakija kama ulivyoweka hapatakuwa na wakukunyima zawadi zako.

"Mimi sina hata mtu mmoja ninayemjua ndani ya kampuni hii, nimeshinda na nimekuja kuchukuwa hela zangu, nawashauri Watanzania wenzangu hasa vijana wasiwe na wasiwasi na Kampuni ya SportPesa kwani hawana ubabaishaji, lakini pia wasikate tamaa pindi mambo yanapokuwa yanakwenda tofauti kwani huwezi jua Mungu amepanga lini ushinde," alisema Joachim.

## Tanzania, Uganda ni kazi Cecafa U-20

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya soka ya Taifa ya vijana ya umri chini ya miaka 20 ya Tanzania Bara (U-20), itakutana na yosso wenzao wa Uganda katika mechi ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (Cecafa U-20) itakayochezwa Jumatatu kwenye Uwanja wa Gulu, Jinja nchini Uganda.

Tanzania Bara imefika hatua ya robo fainali baada ya kumaliza ikiwa kinara wa Kundi B kwa kujikusanyia pointi saba sawa na Kenya, wakati wenzao wa Zanzibar (Karume Boys) wamemaliza wa tatu kwenye kundi hilo huku Ethiopia ikiburuza mkia.

Katika mchezo wake wa mwisho wa hatua ya makundi, uliochezwa juzi, Tanzania Bara iliwapa kichapo cha bila huruma cha mabao 5-0 "ndugu zao" Karume Boys.

**Katika mchezo huo, mshambuliaji chipukizi wa Tanzania, Kelvin John, alifunga hat-trick huku mabao mengine yakipachikwa wavuni na Lusajo Mwaikenda na Novatus Dominic.**

Kocha Mkuu wa timu ya Tanzania, Zuberi Katwila, aliliambia gazeti hili kuwa mchezo huo unatarajiwa kuwa mgumu kutokana na Uganda kuonyesha kiwango kizuri katika mechi zake za hatua ya makundi.

"Kwanza tunamshukuru Mungu tumepata ushindi na kusonga mbele, tunajua Uganda wana kikosi kizuri, tutapambana nayo kuhakikisha malengo yetu yanatimia ya kurudi na ubingwa," alisema Katwila.

Mechi nyingine za hatua ya robo fainali ya mashindano hayo ya U-20 yanayoandaliwa na Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), zitakuwa ni kati ya "ndugu wawili" Sudan dhidi Sudan Kusini wakati Eritrea watawakabili Karume Boys na Burundi itawavaa Kenya.

# BAOBAO QUEENS YASUASUA USAJILI

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limesema ni timu moja ya Baobao Queens ya Dodoma ndiyo haijawasilisha usajili wake kwa ajili ya kushiriki Ligi Kuu ya Wanawake nchini ambayo inatarajiwa kuanza baadaye mwezi ujao, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa TFF, Clifford Ndimbo, alisema zimebaki siku mbili tu kabla ya dirisha la usajili la ligi hiyo inayoshirikisha klabu 12 kufungwa.

Ndimbo alisema wanaamini uongozi wa klabu hiyo kwa kushirikiana na Chama cha Soka Mkoa wa Dodoma (DOREFA), watahakikisha wanakamilisha mchakato huo kwa wakati ili wasikutane na adhabu au kupoteza nafasi ya ushiriki katika ligi hiyo.

"Tunaweza kusema zimebaki saa chache ili kufunga dirisha la usajili la Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, na hadi leo (jana), tunavyoongea, imebaki Baobab Queens tu, tunaamini nao watakamilisha mchakato huu na kuendelea na maandalizi, " alisema kiongozi huyo.


Ndimbo aliwataka wote waliokamilisha usajili kuendelea na maandalizi ili kuifanya ligi kuwa na ushindani zaidi katika msimu ujao na kutoa wachezaji bora watakaoitumikia timu ya Taifa ya Wanawake kwa mafanikio.

JKT Queens ndio mabingwa watetezi wa ligi hiyo ambapo walitwaa ubingwa huo bila ya kupoteza mchezo hata mmoja msimu uliopita.

# Michezo

Jumamosi Septemba 28, 2019

Nipashe

Higuain: Ronaldo huyu si yule wa Madrid

HABARI UK 30



Kikosi cha Yanga

# YANGA: TUPO TAYARI KUPINDUA MEZA LEO

Zahera aapa Zesco ikiwakatia umeme hotelini, Lwandamina asema dakika 90 zitaamua lakini...

**Na Somoe Ng'itu**

TUKO tayari! Hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Yanga Mkongomani Mwinyi Zahera, kuelekea mchezo wa marudiano wa mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Zesco FC unaotarajiwa kuchezwa leo kwenye Uwanja wa Levy Mwanawasa ulioko mjini Ndola, Zambia.

Yanga ambayo kaulimbiu yao kwenye mechi hiyo ni "Kupindua Meza Kibabe", katika mechi ya kwanza iliyochezwa Septemba 14, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1 na hivyo, mshindi wa jumla atakayepatikana leo atafanikiwa kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo inayofanyika kila mwaka.

Akizungumza na gazeti hili jana, Zahera, alisema kikosi chake ambacho kinaburuza mkia katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kufungwa na Ruvu Shooting bao 1-0, kimejiandaa vizuri na mchezo huo wa marudiano na kila mchezaji yuko tayari kucheza katika kiwango cha juu.

Zahera alisema anafahamu mchezo wa leo utakuwa na ushindani kutokana kila upande kufahamiana vema, tofauti na ilivyokuwa wakati walivyokutana katika mchezo wa kwanza Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

"Wachezaji wangu wako tayari kimwili, kiakili, kiufundi tuko tayari, miguu inatetemeka kusubiri muda wa mchezo ufike, tunawafahamu walivyo na wao wanatufahamu tulivyo, tunatarajia utakuwa mchezo mzuri," alisema kocha huyo.

Winga wa timu hiyo, Mrisho Ngasa, alisema wachezaji wote wako katika hali nzuri wakiusubiri mchezo huo ambao unatarajiwa kuwa na ushindani mkali. "Tumefanya mazoezi mazuri, tunajua mchezo utakuwa mgumu na wenye ushindani, tumejipanga kupambana kwa kila hali kuhakikisha tunashinda na kusonga mbele kwenye mashindano haya ya Ligi ya Mabingwa Afrika, tunaomba dua za Watanzania wote ili tutimize malengo," alisema Ngasa.

Kocha Mkuu wa Zesco FC, George Lwandamina, alisema jana kuwa wamejipanga kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika mchezo huo wa marudiano.

Lwandamina akizungumza na waandishi wa habari nchini Zambia, alisema wanafahamu uzuri na ubora wa Yanga ulipo, hivyo wamejipanga kuwakabili kwa nguvu katika dakika zote.

"Tumejiandaa kwa ajili ya kufanya vizuri katika mechi hii ya marudiano, najua haitakuwa mechi rahisi, itakuwa na ushindani, tunahitaji ushindi ili kusonga mbele, hatuna maneno mengi tusubiri dakika 90 zitaamua nani atasonga mbele," Lwandamina alisema.

**NJE YA UWANJA**

Kikosi cha Yanga kimelalamika kuhujumiwa kwa kukosa huduma ya umeme katika hoteli waliyofikia.

Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Yanga, Saad Khimji, alisema kuwa hali hiyo iliwasumbua juzi usiku baada ya kuwasili Ndola, lakini wamewaambia wachezaji wao kupuuza hujuma hizo na kufikiria mchezo huo.

"Tumeelezwa kwamba Zesco ambao wanamiliki shirika la umeme kuwa na tabia hiyo ya kukata umeme katika maeneo ambayo wapinzani wao wamefikia, kiukweli wachezaji walikuwa wanapata tabu, ukikaa ndani joto na ukisema utoke nje baridi," alisema Khimji.

Patrick Sibomana aliifungia Yanga bao kwa njia ya penalti wakati Mzimbabwe Thabani Kamusoko aliisawazishia Zesco katika dakika za lala salama walipokutana jijini Dar es Salaam wiki mbili zilizopita

Wakati huo huo, wawakilishi wengine wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, Azam FC watashuka uwanjani kuwakabili wenyeji wao Triangle United mjini Bulawayo huku wakiwa na kumbukumbu ya kufungwa bao 1-0, hivyo wanahitaji ushindi kuanzia mabao 2-0 ili kusonga mbele.

# Aussems: Tunaongea kwa akili si mdomo

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Kikosi cha Simba kikitua jijini Mwanza jana tayari kwa safari ya kwenda Musoma kesho kuivaa Biashara United hapo Jumapili, Kocha Mkuu wa mabingwa watetezi hao, Mbelgiji Patrick Aussems, amesema "tunaongea kwa akili na si mdomo".

Aussems alitoa kauli hiyo juzi baada ya kuwachapa wababe wao wa msimu uliopita, Kagera Sugar kwa mabao 3-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu iliyopigwa Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba.

Akizungumza baada ya mechi hiyo, Aussems alisema baadhi ya timu, makocha na wachezaji wamekuwa wakiongea sana, lakini wao hawaongei kwa mdomo bali akili uwanjani.

"Unajua baadhi ya timu, makocha na hata wachezaji wanaongea sana kwa mdomo, lakini sisi tunaongea kwa akili," alisema Aussems akizungumzia ushindi huo wa kwanza kwake tangu aanze kuinoa Simba kufuatia msimu uliopita kupigwa nyumbani na ugenini dhidi ya Kagera Sugar.

Kabla ya mchezo huo, Kocha wa Kagera Sugar, Mecky Maxime alinukuliwa na baadhi ya vyombo vya habari (si Nipashe), akidaiwa kusema kuwa endapo Simba itampanga mlinda mlango wao, Aishi Manula, Kagera Sugar itashinda kwa kuwa wanajua namna ya kumfunga, hata hivyo juzi aliikana kauli hiyo akidai alinukuliwa ndivyo sivyo.

Lakini pia watani wa Simba, Yanga wamekuwa wakiwabeza sana 'Wekundu wa Msimbazi' hao kufuatia kutolewa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwenye raundi ya awali, hivyo haijulikani Aussems alimlenga nani moja kwa moja.

"Kikosi kimefika salama jinini Mwanza (jana mchana) kitakuwapo kwa siku moja (hapa) na Jumamosi kitaenda Musoma kufanya mazoezi ya mwisho kabla ya mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Biashara United ambao utapigwa Jumapili kwenye Uwanja wa Karume," ilieleza taarifa ya Simba jana.

Katika mechi hiyo ya juzi mabao ya Simba yalifungwa na Meddie Kagere (mawili) na Mohamed Hussein 'Tshabalala'.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >